**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

**MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA**

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Ali Abdalla Ali | Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini. |
| 2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa | Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni. |
| 3. Mhe. Mgeni Hassan Juma | Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake. |
| 4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi | MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais. |
| 5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani. |
| 6. Mhe. Omar Yussuf Mzee | MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais. |
| 7. Mhe. Haji Omar Kheri | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu. |
| 8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais. |
| 9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais. |
| 10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary | MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni. |
| 11. Mhe. Rashid Seif Suleiman | MBM/ Waziri wa Afya/ /Jimbo la Ziwani. |
| 12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban | MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais. |
| 13.Mhe. Juma Duni Haji | MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Kuteuliwa na Rais. |
| 14.Mhe. Zainab Omar Mohammed | MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais. |
| 15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan | MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni. |
| 16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge. |
| 17.Mhe Dr. Sira Ubwa Mamboya | MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Kuteuliwa na Rais. |
| 18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui | MBM/Waziri wa Biashara,Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni. |
| 19.Mhe. Said Ali Mbarouk | MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando. |
| 20.Mhe. Haroun Ali Suleiman | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi. |
| 21.Mhe. Haji Faki Shaali | MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni. |
| 22.Mhe. Machano Othman Said | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni. |

| | |
|---|---|
| 23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole. |
| 24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) | Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka. |
| 25. Mhe. Zahra Ali Hamad | Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake. |
| 26.Mhe.Mahmoud Thabit Kombo | Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki |
| 27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake. |
| 28.Mhe. Haji Mwadini Makame | Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi. |
| 29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi | Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni. |
| 30.Mhe. Mohammed Said Mohammed | Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae. |
| 31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak | Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake. |
| 32.Mhe. Said Hassan Said | Mwanasheria Mkuu. |
| 33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla | Jimbo la Chonga |
| 34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali | Jimbo la Mkoani |
| 35.Mhe. Abdi Mosi Kombo | Jimbo la Matemwe |
| 36.Mhe. Ali Mzee Ali | Kuteuliwa na Rais |
| 37.Mhe. Ali Salum Haji | Jimbo la Kwahani |
| 38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk | Nafasi za Wanawake |
| 39.Mhe. Asaa Othman Hamad | Jimbo la Wete |
| 40.Mhe. Asha Abdu Haji | Nafasi za Wanawake |
| 41.Mhe. Asha Bakari Makame | Nafasi za Wanawake |
| 42.Mhe. Ashura Sharif Ali | Nafasi za Wanawake |
| 43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 44.Mhe. Farida Amour Mohammed | Nafasi za Wanawake |
| 45.Mhe. Fatma Mbarouk Said | Jimbo la Amani |
| 46.Mhe. Hamad Masoud Hamad | Jimbo la Ole |
| 47.Mhe. Hamza Hassan Juma | Jimbo la Kwamtipura |
| 48.Mhe. Hassan Hamad Omar | Jimbo la Kojani |
| 49.Mhe. Hija Hassan Hija | Jimbo la Kiwani |
| 50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu | Jimbo la Bububu |
| 51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu | Jimbo la Mji Mkongwe |
| 52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub | Jimbo la Muyuni |

| | |
|---|---|
| 53.Mhe. Kazija Khamis Kona | Nafasi za Wanawake |
| 54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | Jimbo la Kitope |
| 55.Mhe. Marina Joel Thomas | Kuteuliwa na Rais |
| 56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) | Jimbo la Mkwajuni |
| 57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma | Jimbo la Bumbwini |
| 58.Mhe. Mohammed Haji Khalid | Jimbo la Mtambile |
| 59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali | Jimbo la Uzini |
| 60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi | Jimbo la Chambani |
| 61.Mhe. Mussa Ali Hassan | Jimbo la Koani |
| 62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | Nafasi za Wanawake |
| 63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi | Nafasi za Wanawake |
| 64.Mhe. Nassor Salim Ali | Jimbo la Rahaleo |
| 65.Mhe. Omar Ali Shehe | Jimbo la Chake-Chake |
| 66.Mhe. Panya Ali Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 67.Mhe. Rufai Said Rufai | Jimbo la Tumbe |
| 68.Mhe. Raya Suleiman Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 69.Mhe. Saleh Nassor Juma | Jimbo la Wawi |
| 70.Mhe. Salim Abdalla Hamad | Jimbo la Mtambwe |
| 71.Mhe. Salma Mohammed Ali | Nafasi za Wanawake |
| 72.Mhe. Salma Mussa Bilali | Nafasi za Wanawake |
| 73.Mhe. Salmin Awadh Salmin | Jimbo la Magomeni |
| 74.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman | Nafasi za Wanawake |
| 75.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha | Jimbo la Mwanakwerekwe |
| 76.Mhe. Subeit Khamis Faki | Jimbo la Micheweni |
| 77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis | Jimbo la Konde |
| 78.Mhe. Suleiman Othman Nyanga | Jimbo la Jang'ombe |
| 79.Mhe. Ussi Jecha Simai | Jimbo la Chaani |
| 80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir | Nafasi za Wanawake |

**Ndugu Yahya Khamis Hamad** **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

**Kikao cha Pili - Tarehe 22 Januari, 2015**

*Kikao kilianza saa 3:00 Asubuhi*

**DUA**

*Mhe. Naibu Spika (Ali Abdalla Ali) alisoma Dua*

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:** Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati kuhusu Mswada wa Maafa.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MASWALI NA MAJIBU**

**Nam. 119**

**Malipo ya Fedha kwa Polisi Wastaafu**

**Mhe. Saleh Nassor Juma** – Aliuliza:-

Kuna taarifa ya Polisi Zanzibar kustaafu kazi, walipostaafu kazi waliandikiwa pesa za malipo za usafiri pamoja na mizigo yao kwa ajili ya kwenda kwao. Kadhia hiyo imetokea Mkoa wa Kaskazini Unguja. Askari hao jumla yao walikuwa watano (5) waliombewa fedha Shilingi 16,000,000/-. Bahati nzuri sana fedha hizo zimepatikana kutoka Makao Makuu ya Polisi ya Tanzania Bara na kuletwa Zanzibar, badala ya kulipwa fedha hizo malipo yalitolewa kwa kila askari Shilingi 60,000 mpaka Shilingi 80,000/-

(a) Askari hao wamekwenda kulalamika kwa Kamishna wa Polisi wa Zanzibar. Je, Kamishna huyo alichukua hatua gani kwa askari wetu hao ambao wametumikia taifa kwa muda mrefu.

(b) Ikiwa kitengo hicho cha polisi kinafanya hivyo wananchi watakuwa na hali gani.

(c) Je, ni kweli kitendo hicho kimetokea kwa askari hao na nini hatma yake waliofanya kitendo hicho.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais** – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 119 lenye vipengele a, b, na c naomba kutanguliza maelezo yafuatayo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kulikuwa na askari waliostaafu kutoka Mkoa wa Kaskazini Unguja, ambapo kila askari anapostaafu hutayarishiwa usafiri wa mizigo pamoja na familia yake hadi Mikoani mwao. Jambo hilo hufanyika kwa kutegemea mstaafu alikuwa na cheo gani, kwa Wastaafu hao malipo yalipaswa kufanyika kama ifuatavyo:-

Kila askari alipaswa kulipwa gharama za mizigo tani 3 kwa gharama ya shilingi 20,000 kwa kila tani kwa masafa ya kilomita 20. Hivyo, kufanya jumla ya shilingi 60,000/- kuwa ndio malipo sahihi ya kusafirisha mizigo hiyo kwa umbali huo. Aidha, kila askari alipaswa kulipwa shilingi 6,000/- ikiwa ni nauli ya usafiri wake. Hivyo, askari hao walipaswa kulipwa jumla ya shilingi 66,000/- kwa kila mmoja.

Mhe. Naibu Spika, baada ya utangulizi huo sasa kwa heshima kubwa naomba kumjibu Mhe. Saleh Nassor Juma swali lake kwa mujibu wa taarifa za polisi kama ifuatavyo:

a) Kama nilivyokwishasema hapo awali katika jibu langu la msingi, Ofisi ya Kamishna wa Polisi aliwaita askari hao na kuwapatia maelekezo juu ya utaratibu wa malipo hayo na wao wenyewe kuridhia.

b) Wananchi hawana haja ya kuwa na hofu wala shaka juu ya chombo chao cha Jeshi la Polisi kupitia ngazi mbali mbali. Kwani kuhusu kadhia hii hatua stahiki zimechukuliwa na hao askari hawana malalamiko tena kwa sasa kutokana na taarifa ya polisi.

c) Ni kweli kitendo cha askari kulalamika kilitokea lakini baada ya kupatiwa maelezo juu ya utaratibu ulivyo askari hao waliridhika.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Askari Wastaafu ni *standby force* ile ya nchi yetu na tunawahitaji sana, na kwa kuwa nchi bado inahitaji ulinzi wa raia na mali zake kiasi ambacho hadi hivi sasa tunatumia hawa askari jamii. Kwa hivyo, ni dhahiri kwamba polisi wastaafu wanahitajika sana.

(a) Hamuoni kwamba askari kumlipia tani 20 za mizigo kwa kila kilomita, kwamba askari anayestaafu ikiwa anatoka Kaskazini mpaka kufika Bukoba kuwa ni tatizo kwa kumlipia tani hizo tu.

(b) Mheshimiwa inasikitisha sana kwamba taarifa tulizonazo ni kuwa, ilikuwa walipwe kiasi kile tulichokitaja cha shilingi 16,000,000/- lakini wakalipwa shilingi 60,000 mpaka 80,000 kwa kila mmoja. Hamuoni kufanya hivi askari mstaafu unamvunja moyo na pale taifa litakapomtaka tena kwa ajili ya kutulindia mali zetu pamoja na sisi raia kwamba watavunjika moyo kiasi ambacho hawataifanya hiyo kazi. Hamuoni kwamba kuna haja ya kuwaongezea kiasi kikubwa cha fedha ili wakapata moyo na hatimaye pale tutakapowahitaji tena kutulinda wakatulinda kama walivyofanya kipindi kile tulipokuwa tukipigana na Uganda. Tuliwachukua na wakafanya kazi nzuri na hatimaye kulipatia ushindi mkubwa sana taifa letu kwa kumtokomeza nduli Iddi Amini.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba askari wetu hawa wastaafu ni askari wa akiba na wana uwezo mkubwa sana wa kusaidia nchi yetu pale matatizo yanapotokea. Ni kweli nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kwamba kiwango hiki ni kidogo kwa askari wetu, lakini kutokana na hali halisi ya uwezo wa nchi ndio maana kikapangwa kiwango hicho. Lakini naomba niseme ushauri huu nitauchukua na kumuandikia rasmi Waziri wa Mambo ya Ndani ili aone ushauri wa Mhe. Saleh Nassor na Waheshimiwa wa Baraza hili kwamba bado kuna umuhimu wa askari wetu hawa kupata kiwango zaidi ya hiki kutokana na hali halisi ya maisha na ukweli ulivyo. Kwa msingi huo nakubaliana na Mhe. Saleh Nassor Juma, ahsante.

**Mhe. Salim Abdalla Hamad:** Mhe. Naibu Spika, swali mama limesema kuwa zilitengwa jumla ya shilingi 16,000,000/- kwa askari hao watano (5), sawa na shilingi 3,200,000 kwa kila askari. Kama taarifa hii ni kweli naamini kuwa hao waliotoa fedha hii walizingatia mahala mbali mbali wanakokaa hawa wastaafu na kutenga fedha hii ambayo badala yake ilifanyiwa marekebisho kama Mhe. Waziri alivyoeleza.

Je, Mhe. Waziri anaweza akatueleza kila askari alikuwa anakaa wapi, anakwenda wapi na gharama yake ni ipi mpaka pesa hii iwe haikuwa sahihi.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Naibu Spika, hatuna taarifa za polisi walizotutaarifu kwamba ni shilingi 16,000,000/- ndio zilizopelekwa katika Jeshi la Polisi kwa nia na dhamira ya kuwalipa askari hawa ambao Mhe. Mwakilishi anaulizia, isipokuwa Jeshi la Polisi lilituhakikishia kwamba, kwa mujibu wa utaratibu wao waliojiwekea ni kwamba askari hao walipaswa kulipwa kiwango hicho ambacho wamelipwa. Kwa sasa hatuwezi kuelewa askari hao kila mmoja alikuwa anakaa wapi, lakini kwa ufupi nilikuwa na taarifa kwamba ni askari kutoka Mkoa wa Kaskazini Unguja kama ambavyo Mhe. Saleh Nassor Juma ameuliza.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo tutachukua hatua za kuwasiliana na Kamishna wa Polisi Zanzibar kutaka uhakika. Kwanza, ni kweli ni shilingi 16,000,000 zimekuja kwa ajili ya askari hao? Pili, nipate taarifa kamili askari hao walikuwa wanatokea sehemu gani na gani ili niweze kumuwasilishia Mhe. Mwakilishi kwa maandishi maelezo aliyoyataka.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Naibu Spika, nashukuru sana na mimi asubuhi ya leo kuweza kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza ambalo dogo sana Mhe. Waziri wangu. Kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kila analoambiwa na wajumbe, Mhe.Waziri ninavyofahamu mimi wizara yake ni moja ambayo inayounganisha pand zetu mbili za Muungano.

Je, Mhe. Waziri haoni ipo haja kwa makusudi ya kuwa na ofisi ambayo inapata *data* za kila siku kutokana na kustaafu askari wetu. Kama ni hivyo, ni lini ataweza kuweka utaratibu huo, kuliko kupewa *data* ambazo anatwambia kwamba mpaka sasa hivi hajazifahamu vizuri.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Naibu Spika, kwanza nimwambie Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, wizara yangu inaratibu mambo ya Muungano kwa upande wa Zanzibar. Lakini wizara yangu sio msimamizi wa moja kwa moja kwa Jeshi la Polisi. Kuna wizara mahsusi inayosimamia mambo ya Polisi na ni Wizara ya Mambo ya Ndani. Kwa hivyo, kama kazi yangu ya kuratibu kila lile ambalo nitashauriwa nitafanya lakini inategemea mipaka ya shughuli zetu za kazi. Kwa ufupi hatuwezi kupata *data* za kila siku kwa shughuli za polisi kwa sababu wizara yangu sio kazi yake, isipokuwa tukitakiwa taarifa yoyote kutoka polisi tutawaulizia na kuziwasilisha katika Baraza hili tukufu.

**Nam. 34**

**Msaada kwa *“Sober Houses”* zenye Kutoa Mafunzo ya**

**Dini na Maadili mema**

**Mhe. Saleh Nassor Juma** – Aliuliza:-

Kwa kuwa *‘sobber houses’* za Mwera Mtofaani na ile iliyopo Chumbuni hapa Unguja zinatoa mafunzo ya Dini ya Kiislamu *(Islamic Oriented Programms)* na kwa kuwa hapa Zanzibar zipo Taasisi na Jumuiya kadhaa za Kiislam ambazo hutoa misaada mbali mbali kwa wananchi wenye matatizo, pamoja na kutoa Mawaidha kwa wananchi.

(a) Je, serikali inatambuwa uwepo wa *‘sober house’* zenye mwelekeo wa Kiislam (*Islamic Oriented Sober Houses*) hapa nchini.

(b) Je, serikali imezisaidia kiasi gani pamoja na kuzishajihisha Taasisi za Kiislam kuzisaidia nyumba hizo za kurekebisha tabia.

(c)

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais** – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa heshima kubwa kabla ya kumjibu Mhe. Saleh Nassor Juma swali lake nambari 34 naomba kwanza nitoe maelezo mafupi yafuatayo:

Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya inatambua kuwepo kwa nyumba ya upataji nafuu kwa kuendesha huduma hizo kwa kutumia taratibu za Kiislamu katika eneo la Uzi, Meli Nne na Mwera, Mtofaani hapa Unguja na hakuna nyuma katika eneo la Chumbuni yenye kutoa huduma hizo.

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako tena naomba sasa nimjibu Mhe. Saleh Nassor Juma swali lake lenye kifungu a na b kama ifuatavyo:

(a)Serikali inatambuwa kuwepo kwa nyumba za upataji nafuu zenye mwelekeo wa Kiislam hapa Zanzibar, na nyumba hizo zimeanzishwa baada ya kupata ridhaa ya Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Uthibiti wa Dawa za Kulevya Zanzibar. Nyumba hizo zinaendana na Mwongozo wa Uendeshaji wa Nyumba za Upataji Nafuu nyengine ambazo tunazo ndani ya visiwa vyetu.

Uendeshaji wa nyumba hizo huendeshwa kufuata hatua kumi na mbili za Kiislam, ambao hutambulika kuwa ni mfumo wa *"Milat Islam"* na hatua hizo zimeletwa hapa Zanzibar kutoka mwaka 2009 baada ya wafanyakazi wa tatu wa tume na kijana mmoja ambaye alikuwa amepata nafuu kwenda kupata mafunzo hayo huko Marekani na baadae kuweza kuyafundisha hapa Zanzibar. Kwa maana hiyo, Serikali ya Mapinduzi kupitia tume inatambua kwa kina huduma hizo.

b) Serikali inazisaidia kwa kuzipatia ruzuku ya shilingi 1,800,000 kila mwaka ya kuendesha nyumba hizo. Pia, imewashajihisha viongozi na taasisi mbali mbali za Kiislamu kuzisaidia nyumba hizo. Vile vile taasisi na viongozi mbali mbali huwa wanatembelea na kuzisaidia nyumba hizo za kurekebisha tabia.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana na yenye ufafanuzi mzuri aliyoyatoa Mhe. Waziri, naomba niulize swali la nyongeza. Kwanza nishukuru kwamba amekiri kuwa serikali inatoa ruzuku kwa nyumba hizi ili ziweze kujiendesha.

(a) Je, ni sababu gani za msingi zinazofanya serikali kushindwa kutoa ruzuku hii kwa kipindi kirefu sana kiasi ambacho hivi sasa wakati wowote wale waathirika wa madaya ya kulevya waliomo katika nyumba hizi wanaweza wakafukuzwa katika nyumba zile kutokana na kushindwa kulipa pango, zikiwemo *Sober Houses* zilizomo katika jimbo langu katika eneo la Mkoroshoni na hili eneo la Uzi.

(b) Kwa sababu amekiri kuwa kuna hizi *Islamic Oriented Sobers* na kwa kuwa serikali inachelewa sana kuwapatia hii ruzuku, ni sababu gani za msingi zinazofanya serikali kushindwa kuzishawishi taasisi za kidini zikiwemo **Shia-ithnashiria,** wakiwemo hawa jamaa zangu wa Zawiyatul-Qadiriyya, wakiwemo hawa *Answar Sunna* kushindwa kuwashawishi na kushindwa kusaidia hata hizi *Islamic Oriented Sobers,* ambazo hawa wana moyo sana wa kusaidia taasisi za Kiislam mbali na afisi ya Mufti ambayo nayo haijanyoosha mkono hata siku moja katika hizi *Islamic Oriented Sobers.* Ni sababu gani za msingi, kwamba nyinyi mnashindwa kuwashawishi hawa.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:** Mhe. Naibu Spika, nikubaliane naye kwamba utoaji wa ruzuku haui mwanzo wa mwaka wa fedha kwa *Sober Houses* zote na hii ni kwa sababu fedha zenyewe zinategemea bajeti ambayo imepangwa ndani ya ofisi yetu. Kwa hivyo, kwa kadiri Bajeti inavyoingizwa hasa hii ya Tume ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya ndivyo ambavyo tunaweza kuzisaidia *Sober House* zetu. Ikumbukwe kwamba huu ni mwaka wa tatu tu ndio Serikali imeanza kutoa ruzuku kwa ajili ya kuzisaidia *Sober House* kwa kuona ugumu wa uwendeshaji wa huduma zenyewe na kuweza kuthamini ile jitihada inayofanywa na taasisi binafsi ambazo, kwa kweli zinatusaidia sana ndani ya jamii.

Kwa hivyo, inategemea kwamba waanzishaji wa *Sober* House hizi ambao wamejitolea waendelee kuwasaidia na kuziendesha *Sober House* hizi na kwamba kwa mwaka huu hii *Sober House* ya Uzi ambayo wameitaja, hii naomba nimuarifu kwamba hii ilipatiwa mgao wake wa ruzuku mapema sana kama kuchelewa kidogo inawezekana ni hii ya Mkuroshoni, lakini ya Uzi wamepatiwa mapema kutokana na hali yao pia ilivyokuwa kidogo tata na ikahitaji kupatiwa uangalizi wa aina yake.

Lakini ikumbukwe sisi wazazi na wananchi wote kwamba watoto wanaokwenda pale ni watoto ni wajukuu zetu ni ndugu zetu, ni niwajibu wetu kama wazazi kuhakikisha kwamba tunawasaidia watoto wale kuwalipia ile fedha ndogo ambayo inatakiwa ilipwe ndani ya nyumba hizi za kupatia nafuu, ili watoto wale waweze kurekebishwa tabia zao.

Kwa sasa tunachokiona sana ni kwamba wazazi wengi inawezekana kwa kuchoshwa na tabia za watoto wao ambao walikuwa wameingia katika tabia ya kutumia madawa ya kulevya, wanakuwa wanamkataa kabisa yule mtoto kushirikiana nae na hili si sahihi; hawa ni watoto wetu na wapaofikia katika hatua ile ni lazima tuwaone kwamba ni wagonjwa kama ambavyo familia inashughulika kumtibu mgonjwa mwengine. Naomba sana wazazi na wananchi tuwasaidie watoto hawa waweze kulipa ile ada ndogo ambayo inalipwa ndani ya *Sober House,* ili waweze kupatiwa matibabu hayo.

Kuhusu suala la pili Mhe. Naibu Spika, ofisi yetu imefanya jitihada kubwa ya kuweza kuzitambulisha *Sober House* hizi sio tu kwa viongozi wa kidini na nataka nimpe taarifa kwamba Mhe. Mufti Mkuu wa Zanzibar tayari ameshazitembelea hizo mwanzoni sana anafahamu uwepo wa taasisi hizo na tulifanya hilo kwa makusudi kwamba yeye anasimamia masuala ya dini na yeye atakuwa na uwezo pia mkubwa wa kushawishi taasisi mbali mbali za kidini kuweza kwenda hapo kwa kushirikiana na sisi ili kuziasidia nyumba hizi, ambazo watoto wetu wapo na kwa kweli amefanya hivyo na naomba tu Mheshimimiwa Mwakilishi siku nyengine unaweza kupewa taarifa za ziada ndani ya *Sober House* hizo.

Lakini kweli bado zipo taasisi nyingi ambazo hazijaunga mkono jitihada za ndugu zetu ambao wamefungua nyumba hizi kwa ajili ya kurekebisha tabia za watoto wetu. Natoa wito kwa taasisi zote za dini na ambazo si za kidini, kuweza kufika kuzitambua *Sober House* hizo ambazo serikali inazitambua na kuzisimamia, ili kutoa misaada kwani kazi inayofanyika hapo ni kubwa na ni ya kuthaminiwa sana.

**Mhe. Subeit Khamis Faki:** Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa *Sober House* hizi ambazo zinafuata mfumo wa Kiislam ni *Sober House* nzuri na kwa kuwa ndugu zetu hao wanaokwenda kubadilishwa tabia wanahitaji kufanyiwa mambo mazuri ili wasahau yale ya nyuma waliyokuwa nayo, na kwa kuwa kamati yetu tulikwenda kuzitembelea *Sober House* hizi karibu na Sikukuu na kwa kuwa wanahitaji kufanyiwa mambo mazuri naomba nimuulize Mhe. Waziri, kuna kitu gani ambacho kinazuia kuwasaidia angalau kipindi kile cha sikukuu kupelekewa vitu ambavyuo vitawafariji, kama kanzu, kofia pamoja na vyakula.

Je, kwa kuwa *Sober House* hizi zinaendana na mwendo wa Kiislam ni Mashekhe wangapi wamepangiwa kwenda kuwawaidhi na kuwapa nasaha ili kuonekana kama huu ni utaratibu umepangwa wa serikali kuwasaidia watu wale ili waweze kubadilisha tabia zao.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:** Mhe. Naibu Spika, nilianza awali kueleza kwamba serikali imeanza kuzisaidia *Sober House* hizi kwa kuzipatia ruzuku ya shilingi milioni moja na laki na nane (1,800,000/=) kila moja na hizi ziko kumi na mbili kwa Unguja na Pemba kila moja tumeanza kuzipatia fedha hizo. Lakini tungependa kufanya zaidi na tuliahidi kwamba kila bajeti tutakuwa tunaongezea kile ambacho tunakipeleka ndani ya *Sober House*. Tunashindwa kufanya hivyo kama ofisi kwa sababu bajeti iliyopo haiwezeshi kuweza kutekeleza hayo.

Ikumbukwe kwamba *Sober House* hizi zipo kumi na mbili Unguja na Pemba. Hizi mbili ndizo ambazo zinaendeshwa kwa misingi wa dini. Lakini nyengine zinafata utaratibu huo huo isipokuwa hazijazingatia sana kuendeshwa kwa masuala ya misingi ya dini.

Wito wangu ni kwamba sisi wananchi wote, wafanyabishara, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Mhe. Naibu Spika, naomba hapa nitambue michango mbali mbali ambayo tayari Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi mbali mbali, nisingependa kuwataja kwa majina wamezisaidia *Sober House* hizo.

Lakini vile vile viongozi mbali mbali Wakuu wa serikali Mhe. Rais, Mhe. Makamu wa Kwanza, Mhe. Makamu wa Pili na wengine Mawaziri mbali mbali wote tuungane pamoja tuendelee kuzisaidia na kama hilo tunaliona na kwa kweli ni muhimu basi tutafute njia ya kuzisaidia. Lakini kwa bajeti ambayo ofisi yangu inapewa, kwa kweli kwa sasa hilo ni gumu kuweza kulitekeleza.

**Mhe. Amina Iddi Mabrouk:** Ahsante sana. Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa vijana walioko *Sober House* ni vijana wetu na lengo kuu la vijana wale ni kuwabadilisha tabia na mwenendo mzima wao, sasa namuuliza Mhe. Waziri;

Wizara yako ina utaratibu gani wa kuwatembelea vijana wale wa *Sober House*. Lakini pia na kuwapa moyo vijana wale ili waendelee na kubadilisha tabia.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:** Mhe. Naibu Spika, anayoyazungumza Mheshimiwa Mwakilishi ni kweli na naomba nimuarifu pamoja na kutoa taaraifa kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu wote, kwamba lile wanalolizungumzia ni moja katika kazi ya kila siku ya Tume ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya Zanzibar. Mara kwa mara inafanya ziara ambazo wanazitolea taarifa kwa ajili ya kuzikagua.

Naomba Waheshimiwa muelewe kwamba hakuna ruhusa ya mtu yoyote kuanzisha *Sober House* bila ya kupewa idhini na Tume ya Uratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya na kunakuwa na masharti ambayo yanawekwa ili kuhakikisha kwamba yale yanayofanyika ndani ya nyumba hizo ndio lengo hasa linalokusudiwa.

Kwa hivyo, ofisi yangu inafanya ziara maalum kwa kuziarifu taasisi zenyewe hizo za *Sober House* kwenda kuzikagua kwamba kweli kwanza hicho kinachofanyika ndicho ambacho kinachotakiwa. Lakini Ofisi yetu inashirikiana na *Sober House* zote pale yanapotokea matatizo ya kuweza kupatiwa madaktari au huduma za afya kwa vijana wetu ambao wamo ndani ya nyumba hizo.

Vile vile, ofisi wakati mwengine inafanya ziara za kushitukiza kwa sababu unaweza ukatoa taarifa unakwenda mambo ukayaona yanawekwa uzuri. Lakini katika hali ya kawaida mambo yakawa hayako mazuri.

Kwa hiyo, naomba tu nikuhakikishie Mheshimiwa na Waheshimiwa wote kwamba watendaji na mimi mwenyewe wote tunafanya ziara na tunakaa na tunazungumza na vijana wetu pamoja na mavalantia wao, yaani wale wanaosaidia kupitia katika huduma hiyo ili kuwapa moyo na vile vile tunawasaidia kwa kila hali na kuwaomba wao wanapotoka hapo pia kuweza kuwashajihisha wenzao katika vijiwe kuweza kujiunga na nyumba hizo, na kuachana na tabia ya kutumia dawa za kulevya ambazo huharibu tabia zao.

**Nam. 79**

**Soko la Nje kwa Bidhaa za Wakulima**

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kabla serikali haijajibu swali namba 79 la Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Naomba nichukuwe nafasi kumpongeza Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwa jinsi anavyojali afya za wananchi wake wa Muyuni kwa kupeleka mwezi uliopita tu madawa katika Hospitali ya Zima Moto pale Kitogani kwa ajili ya wanajeshi wa kikosi hicho cha Zima Moto pamoja na wananchi wa pale. *Halkadhalika* katika kijiji cha Jambiani kuweza kupeleka madawa kwa wingi. Kwa hivyo, nachukuwa fursa hii kumpongeza sana Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwa jinsi anavyojali afya za wananchi wake.

Baada ya maelezao hayo naomba swali lake sasa namba 79 kwa idhini yako Mhe. Naibu Spika, nipate majibu ya Serikali hivi sasa.

Kwa kuwa Serikali imekosa nafasi nyingi za kuajiri wananchi wake na baadhi ya wananchi wameelekeza nguvu zao kwenye kilimo kwa kupanda machungwa, tungule, malimau, ndimu, mananasi n.k.

(a) Je, Serikali imejaribu kufuatilia suala hili, kwa kuwa Waziri ametembelea sana nje ya nchi na ameona *'Super market'* na vitu hivyo vinauzwaje, ni lini atawatafutia wakulima soko la nje.

(b) Kutowapatia soko la nje si kuwadharau wakulima wetu.

**Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko –** Alijibu**:-**

Mhe. Naibu Spika, kabla sijamjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake Nam. 79 lenye sehemu (a) na (b) naomba nianze kutoa maelezo kama hivi ifuatavyo:-

Ni kweli kuwa Serikali haina nafasi za kutosha za kuajiri vijana wake wote wanaomaliza masomo na kwa sababu hiyo baadhi yao wameelekeza nguvu zao katika kilimo cha mazao ya matunda, viungo na mbogamboga kama vilivyotajwa na Mhe. Mwakilishi wa jimbo la Muyuni Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Aidha, nataka nikiri kuwa jukumu la kuwaendeleza ni la Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, ni kweli pia kuwa baadhi ya mazao ya kilimo (matunda, viungo na mbogamboga) yanaweza kupata soko la nje ya nchi.

Hata hivyo changamoto ni kubwa na miongoni mwa changamoto hizo ni uzalishaji wa bidhaa zenye ubora unaokidhi mahitaji ya soko la Kimataifa, uwezo wa uzalishaji kwa maana ya idadi ya bidhaa, usafi na usalama wa bidhaa hasa za chakula na taaluma yenyewe ya masoko kwa ujumla n.k.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa nimjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub kuwa, Wizara yangu imekuwa ikichukuwa juhudi za makusudi za kuwasaidia wajasiriamali wa miradi midogo midogo kama vile wazalishaji wa matunda kama ndimu, viungo na matunda mengine ili waweze kuzalisha bidhaa zenye ubora na kwa wingi unaotakiwa kwa kuweza kupata masoko hasa yale ya nje.

Juhudi ya pili inayofanywa na Wizara yangu katika kuwasaidia wajasiriamali wa mazao ya kilimo na mengineyo kupata masoko ni uandaaji na uratibu wa ushiriki wa wajasiriamali wa Zanzibar katika Maonesho ya Biahsara ndani na nje ya nchi tunawashirikisha kila mwaka kuwapeleka;

i. Maonesho ya Kimataifa ya SABASABA ya Dar es Salaam.
ii. EXPO Milan na EXPO Korea.
iii. Maonesho ya Juakali nchini Kenya.
iv. Uandaaji wa Tamasha la Biashara hapa Zanzibar na tumewapa fursa za kuuza bidhaa zao.
v. Maonesho ya Eid el Fitri - Zanzibar.

Lakini la msingi hapa ni kwamba bado *logistics* za kusafirisha bidhaa kama za matunda na mboga mboga katika bandari yetu ya Zanzibar bado haipo kwa mfano kuwa na makontena ya baaridi ili bidhaa hizo zitiwe kwenye makontena hayo kupelekwa nchi za nje.

Kusafirisha bidhaa za matunda na mboga mboga kwa kutumia usafiri wa anga au ndege ni gharama kubwa na hatutaweza kushindana na bei za bidhaa hizo katika masoko ya nje.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Mhe. Naibu Spika, Kwa kuwa wananchi wa Muyuni katika Shehia ya Bwejuu wameanzisha kilimo cha umwagiliaji maji katika kilimo cha ndimu na kwa kuwa mazao ambayo hayaharibiki haraka katika kusafirisha ni pamoja na ndimu, kwa hivyo Mheshimiwa Waziri asiwe na wasi wasi kwamba ndimu zinaweza zikatimia hata wiki mbili kuzisafirsiha hazijaharibika, na kwa kuwa wanalazimika watu wa Bwejuu kuuza ndumu zao pale Sokoni kila Jumapili katika bei ya chini sana kabisa, jambo ambalo linadhalilisha sana kiasi ambacho hatuwapunguzii umasikini kilimo cha ndumu, na kwa kuwa wananchi wa India katika maeneo ya Taj mahal katika sehemu za huku Bengalu na halikadhalika na sehemu za Dubai, wanapenda sana chatine na achari ya ndimu.

Je, lini Serikali yetu ya Mapinduzi za Zanzibar itawasaidia wananchi wa Muyuni katika Shehia ya Bwejuu ambao wanazalisha ndimu kwa wingi sana kuweza kuwasafirishia ndimu hizi.

**Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko-** Ni kweli ndumu nyingi sana zinatoka katika sehemu za Bwejuu, Uroa, Chwaka na sehemu nyingi za kusini mwa kisiwa cha Unguja, hata upande wa Matemwe zinatoka ndimu nyingi sana.

Soko la ndimu liko zuri sana nchini Comoro bahati mbaya usafiri baina ya Zanzibar na Comoro hauko wa kuaminika. Lakini ndimu zinaweza kufanya vitu vingi sana; tunaweza tukatoa achari ya ndimu, mafuta ya ndimu, na hata siki ya ndimu. Umoja wa wasafirishaji ndimu wote Zanzibar wakishirikiana na Wizara ya Biashara na Masoko, wakishirikiana na *UNDP* hivi sasa wanajenga kiwanda cha kusarifu zao la ndimu.

Imani yangu kwamba katika kipindi kifupi kijacho kiwanda hicho kikianza kazi tutaweza kutoa achari ya ndimu nzuri itakayokubalika kimataifa katika masoko ya nje, mafuta ya ndimu, siki ya ndimu na *juice* ya ndimu. Kwa hivyo, Waheshimiwa jitihada za serikali ndio hizo, mimi naamini katika kipindi kifupi kijacho tutafanikiwa kuondoa tatizo la soko kwa walimaji wa ndimu Zanzibar.

**Mhe. Ali Salum Haji:**Ahsante Mhe. Naibu Spika, mimi nimshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake yenye siha na faraja kwa wananchi wa Zanzibar, kwa jitihada ambazo wameweza kuzionesha katika kuanzisha kiwanda cha usindikaji wa ndimu. Nilitaka nimuulize swali dogo tu la nyongeza Mhe. Naibu Spika.

Kwa kwa kuwa sasa hivi wananchi wa Zanzibar wameweza kupata taaluma ya kilimo kupitia utaalamu wa *green house* na mavuno yaliyo makubwa katika kilimo cha matunda ya aina mbali mbali na hususan katika matunda ya matikiti. Je, Wizara ikiachilia mbali kiwanda cha ndimu ina mikakati gani ya kutosha ya kuweza kuanzisha viwanda vidogo vidogo ili kuwasaidia wakulima wa nchi hii.

**Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko:** Mhe. Naibu Spika, ahsante sana naomba vile vile nimshukuru sana Mhe. Mwakilishi kwa swali lake zuri.

Ni kweli wananchi wamehamasika kuzalisha bidhaa nyingi sana kupitia *green house* na kupitia mtindo wa kufanya *irrigation*, yaani umwagiliaji maji na sisi tunaangalia bidhaa hizi kwa uangalifu mkubwa ili bidhaa hizi zitakapokosa soko ni jukumu la wizara yangu ya kuangalia kuyapatia masoko. Kwa hivyo kwa sasa hivi tumeshaandaa miradi ambayo kwamba itakidhi shughuli za vile vitu ambavyo vinazalishwa kwa wingi. Lakini bado matikiti hayajakuwa mengi sana ya kukosa soko Zanzibar, bado bei ya matikiti ni kubwa ukilinganisha na sehemu nyengine. Lakini ninamuhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba tumejitayarisha kuanzisha mfumo wa viwanda vidogo vidogo kwa mfano ikiwa patazalishwa tungule kwa wingi basi miradi ya viwanda vya tungule vya *tomato sauce* na *chili sauce* tumeshajitayarisha na tunaendelea mbele kukamilisha miradi ya kutengeneza *juice* za matunda kama vile chungwa, embe pamoja na matikiti.

Kwa hivyo, Serikali haijakaa kimya, inafuatilia kwa kina juu ya uzalishaji wa matunda na bidhaa nyengine. Mhe. Naibu Spika, ahsante.

**Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi:** Mhe. Naibu Spika, nashkuru kwa kunipa nafasi hii na mimi kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, ninapenda kumuuliza Mhe. Waziri kwa kuwa asali hivi sasa ni biashara kubwa hapa Zanzibar na kwa kuwa wananchi wa Kangani Tondooni wanafuga mizinga kumi na nane ya asali ambayo mpaka hivi sasa bado hawajapata muongozo wa kuuza. Je, Mhe. Waziri ni lini utawatembelea wananchi hawa ili kwanza kuwapatia taaluma ya uvunaji huo wa asali, na pili kuwapatia soko la kuuzia hiyo asali.

Mhe. Naibu Spika, ahsante.

**Mhe. Naibu Spika:** Swali lipo nje ya utaratibu lakini Mhe. Waziri kama unaweza jibu kwa manufaa ya wananchi wote.

**Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko:** Mhe. Naibu Spika, ninamshukuru sana Mhe. Mwakilishi kwa swali lake zuri.

Mhe. Naibu Spika, mimi binafsi nimetembelea wafuga nyuki wengi Kisiwani Pemba na vile vile nimefanya vikao na Umoja wa Wafugaji Nyuki wa Zanzibar, nimefanya vikao na wafugaji nyuki wanawake, ni kweli *production* ya asali inaongezeka mwaka hadi mwaka na elimu ya mradi inakua mwaka hadi mwaka.

Lakini bado asali inayotoka Zanzibar hasa Kisiwani Pemba bei yake ni kubwa sana. Kwa mfano, lita moja ya asali inayotoka Kisiwa Pemba inauzwa karibu shilingi elfu thalathini na tano mpaka elfu arobaini. Lita hiyo hiyo ya asali inayotoka Dodoma inauzwa elfu kumi na mbili mpaka elfu kumi na tano. Kwa hivyo *competition* ya bei ya asali yetu sisi Pemba na inayotoka Tanzania Bara, *gape* yake ni kubwa sana. Sisi tunaitangaza asali yetu kwamba ni asali ya *spice honey* ili ipate bei nzuri zaidi. Lakini mpaka sasa hivi *competition* ya bei ya asali ni kubwa.

Jitihada za Wizara yangu inaangalia utafiti wa kuona namna tutakavyoweza kuwaelimisha wafanyabiashara wa asali waweze kupanga bei zao vizuri. Asali yao ni ghali na haiuziki ndani ya nchi wala nje ya nchi. Kwa hivyo lazima tuwape taaluma ya kupunguza gharama za uzalishaji ili asali yao iuzike katika masoko ya ndani na nje ya nchi.

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana.

**Na. 15**

**Programu za Kunufaisha Wananchi katika Matamasha ya Michezo**

**Mhe. Saleh Nassor Juma** - Aliuliza:-

Katika kutoa fursa kwa Watanzania kushiriki katika kuangalia mashindanfo ya Kombe la Dunia yaliyomalizika miezi michache iliyopita huko Brazil, Wizara inayoshughulika na michezo Tanzania Bara, ilishajihisha kampuni binafsi mbali mbali kuandaa programu mbali mbali zikiwemo bahati nasibu na hatimae washindi wa bahati nasibu hizo walipata fursa ya kwenda Brazil kujionea mashindano hayo, mfano moja ya programu hizo ni shindano la BRAILIKA 2014.

Je, ni lini Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo ya SMZ, itaandaa utaratibu angalau unaofanana na huo ili Wazanzibari ijapo wachache waweze kwenda kuangalia angalau mashindano ya kombe la klabu bingwa ya Afrika, Kagame *Cup* na hata mashindano ya *CHAN*.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo** - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Na. 15 kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa katazo la Serikali baada ya mapinduzi matukufu ya mwaka 1964, mchezo wa bahati nasibu ni miongoni mwa michezo isiyoruhusiwa kuchezwa hapa Zanzibar. Kwa msingi huo Wizara yangu haiwezi kushajihisha makampuni binafsi kucheza bahati nasibu.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Mhe. Naibu Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba niiulize Serikali swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa kupitia bahati nasibu hizo wananchi wenzetu katika nchi jirani ikiwa hiyo Tanzania Bara hapo hupata fursa ya kuangalia michezo mbali mbali ya kimataifa ya soka na hatimaye kuendeleza michezo katika nchi zao na kwa kuwa Wazanzibari hivi sasa ni wapenzi wa mchezo huo wa soka au kabumbu na timu zetu hazifanyi vizuri katika mashindano mbali mbali na kushindwa kupata wawakilishi katika mashindano hayo.

1) Je, haoni kwamba kusema nchi yetu hairuhusu kucheza bahati nasibu kwa upande mmoja ni kudhalilisha soka la nchi hii.

2) Kama hamupendi kuchezwa bahati nasibu basi ni lini Wizara yako Mhe. Naibu Waziri itatayarisha mashindano makubwa kwa sababu Serikali haitaki kuwapeleka watu kwa sababu ni kucheza bahati nasibu, kama vile ya Afrika, mashindano ya kombe la *CHAN* na hata lile la Kagame ili angalau na sisi tukapata kusuuza macho yetu, kuona hapo uwanja wa Amani au pale Gombani Pemba, Mhe. Waziri.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo**: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi maswali yake mawili kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, ninataka niseme kwamba Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wa mwanzo hatuwezi kuziepuka fikra zake, busara zake na hekma zake na kwenye suala mama nimekueleza kuwa hatuwezi kuchezesha bahati nasibu hapa Zanzibar.

Mhe. Mwakilishi au Waheshimiwa Wawakilishi ninawaomba sana tuzihifadhi fikra za Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi la mwaka 1964, kwa sababu hekma zake ni nzuri na busara zake ni nzuri, tunatakiwa tuzilinde na tuzihifadhi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wawakilishi ninawaomba hekma hizi tuzichukue kwa sababu gani, tukiendeleza bahati nasibu ina mambo mengi sana. Bahati nasibu ina uvunjifu amani, bahati nasibu ina mambo mengi kwenye Serikali yetu hii ya Mapinduzi ya Zanzibar tukiiruhusu yatatokea.

Mhe. Mwakilishi na maswali yako mengine yote uliyouliza, nakuomba sana Mhe. Mwakilishi kwa kushirikiana na wananchi wa Zanzibar wanaotusikiliza, vijana wetu bahati nasibu ni kitu ambacho hakitakiwi kwenye Serikali yetu hii ya Mapinduzi.

Waheshimiwa Wawakilishi, ninawaomba sana tuwe pamoja na Serikali ili tuwe na hekma na busara na kuwaeleza wananchi wetu mambo ambayo yanatakiwa yatendeke kwenye Serikali yetu hii ya Zanzibar.

**Mhe. Naibu Spika:** Swali la pili alikuwa anasema Mheshimiwa kwa kuwa bahati nasibu haipo, sasa je, Serikali lini itaandaa makombe ya kimataifa ili waone badala ya kwenda.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo:** Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la pili. Mhe. Mwakilishi tunakubaliana na wewe lakini Wizara ikae, ipange mikakati thabiti kwa kuweza kuelekea huko. Kwa sababu kama unavyojua Wizara yetu bajeti ni ndogo. Ninawaomba Waheshimiwa Wawakilishi tukisimama hapa muengeze bajeti yetu ili tuweze kufanya mashindano hayo hapa Zanzibar.

**Mhe. Hassan Hamad Omar:** Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru sana. Naomba nimuulize swali dogo tu la nyongeza Mhe. Naibu Waziri linalohusiana na michezo.

Kwanza kabisa niipongeze Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kusheherekea sherehe za mapinduzi. Imetayarisha *Mapinduzi Cup* katika msimu huu, yaliyoanza tarehe mosi mpaka kufikia kelele chake tarehe 13. Kuna timu shiriki zilizoshiriki katika mashindano hayo ikiwemo *Shaba Sport Club* ya Kojani; kuna tetesi kwamba timu kutoka Tanzania Bara na kule Uganda zilikuwa zinapata shilingi milioni mbili *per day* na timu kutoka Visiwani zinapata shilingi laki moja na hamsini.

a) Je, ni sheria gani iliyotumika au kigezo gani timu za Tanzania Bara zikapata pesa hizo kama zilizovyotengwa.

b) Kama ni kweli si kuzidhalilisha timu zetu za Zanzibar kukosa kufanya vizuri.

**Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo:** Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru na naomba kumjibu Mhe. Hassan Hamad Omar ambaye timu yake ya Shaba ilishiriki katika mashindano haya na bahati nzuri imefanya vizuri lakini siyo sana, mwakani wajitayarishe vizuri wanaweza wakafanya vizuri zaidi inshallah, mambo ndiyo kujifunza. *(Makofi)*

Kuhusu suala lake, taarifa hizi sisi bado hatuna na kama alivyosema mwenyewe ni tetesi. Wacha tuzichukue tukazifanyie kazi halafu tutamjibu vizuri au tutamjibu kwa maandishi na Waheshimiwa wengine wapate nafasi ya kujua ukweli ulivyo.

Mhe. Naibu Spika, niseme hivyo tusijibu suala la tetesi bora tujibu ambalo tuna hakika nalo vizuri.

**Mhe. Salim Nassor Ali:** Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru sana na mimi kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, mbali na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri pamoja na Waziri, kwanza nichukue fursa hii kusema kwamba wananchi wa Zanzibar ni wapenzi wakubwa sana wa mchezo wa mpira wa miguu na ukiangalia ni kwamba hivi juzi tumemaliza mashindano ya *Mapinduzi Cup* na ni ushahidi tosha kuona Zanzibar kwamba wanapenda mpira wa miguu, kwa sababu walikuwa wanamiminika kwa wingi katika mashindano yale.

Mhe. Naibu Spika, lakini hivi sasa kuna mashindano yanaendelea ya *CHAN* ya Afrika ambayo yanafanyika katika nchi ya Guinea. Lakini Mhe. Naibu Spika, la kusikitisha ni kwamba kuona televisheni ya *ZBC* hayaoneshi mashindano haya. Je, ni sababu gani ambazo zinazoifanya *ZBC* isioneshe mashinano haya, ili Wazanzibari waweze kuyaona mashindano. Kwa sababu kuna wananchi wengine hawana ving'amuzi vya kuonesha *channel* nyengine.

**Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo:** Mhe. Naibu Spika, ninashukuru na naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake linalohusiana na utangazaji wa mashindano yanayoendelea Guinea.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba *ZBC* haitangazi mashindano haya na haitangazi kwa sababu ili utangaze lazima ujipange vizuri na kwamba tunahitaji mawasiliano mazuri na maingiliano mazuri baina ya *satellite* iliopo Guinea na mitambo yetu ya Zanzibar iliopo hapa Rahaleo.

Sasa taratibu za mawasiliano ya *satellite* iliopo Guinea hayakuweza kufanikiwa vizuri na kwa hivyo walihitaji fedha nyingi ambazo kwa kweli tulikuwa hatujapanga nazo katika bajeti yetu na kwa hivyo kwa maana hiyo hatukuwa vizuri kifedha kwa kujiingiza katika hasara, hatujajipangia kabla. Hivyo Mhe. Naibu Spika, hizo ndio sababu zenyewe.

**MUONGOZO**

**Mhe. Nassor Salim Ali:** Mhe. Naibu Spika, nimesikitika sana na jibu la Mhe. Waziri. Mhe. Naibu Spika, mashindano haya yana kalenda yake na yanafanyika kila baada ya miaka miwili. *ZBC* au Wizara ni kukaa kutafuta wadhamini au *sponsor* kuweza kuonesha mashindano haya lakini kwa majibu yake inaonesha fika au inaonesha wazi kwamba Wizara haijajipanga au haijakuwa *serious* katika kuwahudumia wananchi wake katika kuonesha mashindano kama haya ambayo hufanyika kila baada ya miaka miwili.

**Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo**: Mhe. Naibu Spika, halikuwa muongozo lilikuwa ni swali la ziada la nyongeza ninadhani, sasa jibu lake ni hilo hilo kwamba ilihitajika bajeti Mheshimiwa katika kulikamilisha na kama nilivyosema kwamba tulihitaji fedha ambazo zingetuwezesha sisi *ZBC* kutumia *satellite* ya nchi ya kigeni ya Guinea, ili kuweza kurusha matangazo. Inahitaji fedha nyingi ambazo kwa kweli kibajeti hatuna.

Kwa hivyo, hatuwezi kujiingiza mambo ambayo uwezo wa Serikali mdogo na tuna vipaumbele vingi vya kushughulikia hivi sasa.

Hivyo ni kweli kwamba tuna udhaifu kidogo wa upatikanaji wa fedha na mambo ya ufadhili, ni masuala ya kibiashara ambayo lazima mfadhili ambaye anafadhili jambo aone kwamba yeye katika hilo atafaidika vipi.

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Nassor Salim Ali kwa kuongezea Mhe. Waziri kama wapo wafadhili wa kuweza kutusaidia unakaribishwa Wizarani uwapeleke. *(Makofi)*

Mhe. Waziri ninakushukuru, Katibu tuendelee.

**Na.48**

**Uhaba wa Meli za Mafuta kwa Shirika la Meli**

**Mhe. Saleh Nassor Juma** - Aliuliza:-

Katika miaka ya 70 hadi 80 Shirika la Meli na Uwakala la Zanzibar mbali na kumiliki meli kadhaa za abiria vile vile lilikuwa linamiliki meli mbili za mafuta kwa maana ya MT-Uhuru na MT-Ukombozi.

a) Je, meli hizi mbili za mafuta bado zipo.

b) Je, Serikali kwa sasa haioni umuhimu wa kununua meli za mafuta nyengine za kisasa ili ziendane na sayansi na teknolojia iliyopo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano** - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Na. 48 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

a) Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba katika miaka 70 hadi 90 Shirika la Meli na Uwakala lilikuwa linamiliki meli mbili za mafuta, nazo MT- Uhuru na MT- Ukombozi. Kwa hivi sasa Shirika la Meli na Uwakala linamiliki meli moja tu, nayo ni meli ya MT-Ukombozi, kwa vile MT- Uhuru imeshauzwa.

b) Serikali inaona umuhimu wa kununua meli mpya ya mafuta na Serikali inajua kwamba meli ya MT-Ukombozi iliyonayo hivi sasa ina umri mkubwa na tayari imeshapitwa na wakati, kwa sababu hiyo, Serikali tayari imeanza mchakato wa ununuzi wa meli mpya ya kisasa ambayo itakidhi na kuendana na matakwa ya sheria za bahari zilizopo zinazosimamiwa na IMO. Serikali hivi sasa kupitia kamati yake ya ununuzi wa meli mpya imo katika mchakato wa kupitia *quotation* za ununuzi wa meli hiyo, kutoka *shipyard* zifuatazo.

*Shipyard* ya Damen, *Shipyard* ya Uholanzi, Dalhoo ya South Korea na Dynasty Yacht ya China.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba niulize swali moja la nyongeza katika kuwaweka sawa wananchi. Kwa kuwa kuna kauli kwamba MT-Uhuru ilizama na leo hii anatueleza kwamba iliuzwa. Je, ukweli uko wapi katika kauli mbili hizi na kama iliuzwa basi iliuzwa kwa kiasi gani?

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Naibu Spika, meli ya MT Uhuru ilinunuliwa *second hand* mwaka 1978 nchini Uholanzi na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, na ilikabidhiwa rasmi Shirika la Meli na Uwakala. Meli hii ilidumu kwa takriban miaka 25, ambapo katika mwaka 2003 Shirika la Meli lililazimika kuiuza kwa dola za Kimarekani 18,000 kwa Kampuni ya Saimar. Iliuzwa kwa kufanywa chuma chakavu.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii kuweza kumuuliza Mhe. Naibu Waziri maswali mawili ya nyongeza. Mhe. Naibu Waziri ulikubali kwamba ni kweli meli hiyo imeuzwa

na umetaja fedha ambazo kama ulivyosema wewe. Je, Mhe. Naibu Waziri pesa hizo hivi sasa ziko katika mfuko gani.

Lakini pili Mhe. Naibu Spika, kwa kutokana na hali halisi ya kisheria za nchi yetu. Aidha, meli ikitaka kuuzwa huwa inatangazwa au la pili Mhe. Naibu Spika, kuna chombo ambacho kinasimamia ili usimamizi huo uwe halali. Je, Mhe. Naibu Spika, utaratibu huo wizara yako imefanya?

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Naibu Spika, swali la kwanza ni kwamba utaratibu wa mali za serikali zinapouzwa fedha zinakwenda Mfuko Mkuu wa Hazina.

a) Sote tunapokumbuka kwamba kwa kipindi kirefu mali za Shirika la Meli zilikuwa zikimilikiwa na wizara moja kwa moja, mpaka pale ambapo serikali imefanya mabadiliko katika sheria husika, sheria ya Shirika la Meli na Uwakala.

b) Suala la mchakato, ni imani yangu kwamba mchakato mzima utakuwa umefuatwa katika uuzaji na kama tunavyojua kwamba meli hii imeuzwa katika tathnia ya chuma chakavu, kutokana na uchakavu na hayo mazingira yaliyotokea. Lakini usahihi wake naomba tu Mhe. Mwakilishi nimjibu kwa maandishi.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Naibu Spika, nakushukuru na naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Naibu Waziri amekiri kwamba sasa hivi shirika lake au serikali kwa kupitia wizara yake iko kwenye hatua ya ku-*tension* ili kuweza kununua meli mpya. Hii ni dhahiri kwamba shirika na wizara yake ina uwezo wa kifedha. Lakini shirika hili limekabiliwa na kesi ya wafanyakazi kwa muda mrefu, wamekwenda mahakamani na wameshindwa mara nne kwenye Mahakama ya Rufaa, lakini wameshindwa kuwalipa wafanyakazi wale fedha zao kwa kisingizio kwamba hawana fedha.

a) Sasa ushahidi ni kwamba kumbe shirika lina fedha ndio maana wameamua kununua meli mpya, ni kwa nini wasilipe deni kwanza la wafanyakazi wetu wa Zanzibar ili baadaye wakafikiria kununua meli mpya.

b) Ikiwa sasa hivi wanaingia kwenye ku- *tension* ya kutafuta meli mpya na meli ya MT Uhuru na MV Mapinduzi zote zimeuzwa. Watuambie sasa fedha iliyouziwa meli ya MV Mapinduzi ni ngapi na ziko katika mfuko gani?

**Mhe. Naibu Spika:** Swali mama lilikuwa ni meli za mafuta, kwa hivyo ajibu hayo madeni tu wanayodai wafanyakazi. Mhe. Naibu Waziri majibu, la Mapinduzi tutalifanyia utaratibu.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Naibu Spika, swali la kwanza Mhe. Naibu Spika, Mhe. Hija Hassan amelielekeza katika suala la kesi na uwezo wa shirika katika ununuzi wa meli mpya.

Majibu ni kwamba inayonunua meli ni serikali sio shirika. Lakini kwa kumsaidia tu ushauri kwa wananchi hawa ambao ni wafanyakazi wetu wa Shirika la Meli, mimi nimuombe kama wao wana haki inayostahiki nchi yetu inaongozwa kwa mujibu wa sheria, waendelee katika kusimamia haki zao kwa kupitia mahakama na mahakama amri itakayotoa, bila shaka vyombo vyote vya serikali vitakuwa tayari na vitalazimika kutii amri ya mahakama hiyo. Kwa hivyo, nikuombe tu uendelee kuwashauri watu hawa waendelee kupata utaratibu wa kisheria ili waweze kupata haki yao kadiri inavyostahiki.

Swali la pili nimeshajibu, kwamba kwa mujibu wa utaratibu mali zote za serikali zinapouzwa, kinachoingia kinaingia kwenye mfuko mkuu wa Hazina wa serikali.

**Nam. 23**

**Ukosefu wa Huduma ya Maji na Umeme katika Vijiji vya Mtambwe**

**Mhe. Salim Abdalla Hamad** - Aliuliza:-

Pamoja na juhudi kubwa ya utekelezaji na uchangiaji wa fedha taslim katika kuhangaikia kupatiwa huduma muhimu ya maji na umeme katika vijiji kadhaa vilivyomo katika Jimbo la Mtambwe. Inahuzunisha kuona wanavijiji na vijiji vya Kivukoni, Makoongeni na Kinazini (Mtambwe Kusini) hawajafanikiwa kupatiwa huduma hizo, isipokuwa Makoongeni wanapata huduma ya umeme tu na Kivukoni huduma ya maji tu.

Je, wizara inatoa maelezo gani ya kuridhisha yanayohusiana na upatikanaji wa huduma hizo muhimu, ili wanavijiji hao waweze kuepukana na kunywa maji yasiyo salama na pia waweze kujikwamua kiuchumi kutokana na upatikanaji wa huduma hii ya umeme.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati** - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 23 kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, sera ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ni kuhakikisha kuwa wananchi wake wanapata huduma zote za kijamii, ikiwemo huduma ya umeme. Wizara yangu kupitia Shirika la Umeme inaendelea na kutekeleza sera hiyo kwa kuwasambazia wananchi wa Mijini na Vijijini huduma hiyo Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka huu tayari wizara yangu kwa kupitia Shirika la Umeme, imeshasambaza umeme katika vijiji viwili katika Jimbo la Mtambwe, ambavyo ni Kijiji cha Mkanjuni kiliopo Mtambwe Kusini na Kijiji cha Chanjaani kiliopo Mtambwe Kaskazini. Aidha, vijiji vyengine vilivyotajwa basi tutaingiza kwenye bajeti ijayo.

Mhe. Naibu Spika, pia napenda kumshukuru Mhe. Mwakilishi kwa kueleza hali halisi ya maji kwa upande wa Jimbo la Mtambwe. Upande wa Mtambwe Kusini, wizara yangu hivi karibuni itamaliza kazi ya kuvipatia huduma ya maji vijiji vilivyobakia na vijiji wenyewe ni Kidundo, Chekea na Chanjaani na kwa sasa huduma ya maji imefika katika kijiji cha Kidundo. Wizara yangu kwa kupitia Mamlaka ya Maji inaendelea na utafutaji wa mabomba kwa Kijiji cha Chanjaani na Chekea.

**Mhe. Salim Abdalla Hamad:** Mhe. Naibu Spika, nimpe sifa kubwa Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake, lakini kwa sababu mimi nimeuliza vijiji viliopo katika Shehia ya Mtambwe Kusini na Vijiji vya Kidundo, Chekea na Chanjaani viko Mtambwe Kaskazini. Mimi swali langu ni kuwa kwa sababu juzi tu tumesherehekea sherehe ya Mapinduzi ya mwaka 1964 na kutimiza umri wa miaka 51, pamoja na sifa nyingi za maendeleo zimeelezwa, lakini kwa sababu wana vijiji wa Kijiji cha Kinazini, Makongeni, Utaani pamoja na Mitambuni hawana huduma ya maji, wanakijiji wa kijiji cha Kivumoni hawana huduma ya umeme na wanakijiji wa kijiji cha Mavujika hakuna maji wala umeme na vyote viko Mtambwe Kusini.

Ni lini Mhe. Waziri ataona kuwa na hawa watu wa Mtambwe Kusini wana haki sawa sawa na Wazanzibari wenzao kupata hii huduma?

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Naibu Spika, kama nilivyoeleza hapo awali, lengo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuhakikisha kuwapatia wananchi wake huduma za maji safi na salama pamoja na umeme. Ni kweli kuna baadhi ya vijiji ambavyo hivyo alivyovitaja Mhe. Mwakilishi kwamba havijapatiwa huduma hiyo, lakini tatizo linalosababisha kwamba vijiji hivyo viko mbali sana na mradi, lakini wizara yangu kwa kupitia Mamlaka ya Maji, tayari imejiandaa kutafuta mradi na kuzipatia huduma vijiji hivyo na vile vijiji ambavyo bado havijafikiwa na huduma ya umeme. Kama nilivyoeleza hapo awali kwamba tunaviingiza katika bajeti ijayo na tutahakikisha kwamba vijiji hivyo vitafanikiwa kupatiwa huduma mbili hizo.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Naibu Spika, kwanza nitowe pongezi kwa dakika mbili tu, niwashukuru sana Mhe. Waziri, Mhe. Naibu Waziri pamoja na ZAWA wenyewe kitengo cha maji. Kwa kuwa muda mfupi sasa hivi wakati wowote tunaweza Zanzibar tukaneemeka na masuala ya maji. Sasa naingia kwenye swali lenyewe.

Mhe. Naibu Spika, hivi karibuni ilipita ile katakata maji kule Pemba mpaka Unguja na hasa katika Jimbo langu la Kitope sehemu ya Kichungwani. Je, Mheshimiwa huoni kama iko haja kabla hujaanza kukata ukawaelimisha wananchi nini madhumuni ya kukata yale maji.

Pili, Mheshimiwa kwa kuwa wananchi wengi hivi sasa hawajakuwa na taaluma jinsi gani ya kuanzia katika uchangiaji ule mchangio wa mwanzo na kuchangia kuwa endelevu. Je, Mheshimiwa huoni kuwa iko haja kwa kila Shehia ukazipa semina, ili zikaweza kunufaika na maji safi?

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Naibu Spika, wizara yangu kwa kupitia Mamlaka ya Maji inatoa taaluma kwa wananchi na taaluma hiyo tunaitoa katika vyombo vya habari, ikiwemo televisheni pamoja na redio na tunafanya hivyo ili wananchi watuelewe na wapate wepesi wa kuipata hii taarifa.

Kwa hivyo, pia suala la semina ni vizuri na tutajitahidi wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji tutapeana ushauri ili tulitekeleze na hili suala. Lakini kwa kweli tunatoa taaluma kwa wananchi waweze kuchangia, kwa sababu sio kulipia lakini ni changia huduma hii ili mamlaka iweze kujiendesha vizuri.

**UTARATIBU**

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Naibu Spika, Mhe. Naibu Waziri hakulijibu, naomba sana nimsaidie na narudia tena. Mhe. Naibu Spika, nimekusudia mamlaka ifanye utaratibu kwa kupitia Shehia hadi Shehia katika wilaya zetu, kwa kuwapa semina wale watumiaji wa maji ili wakaelewa hasa madhumuni ya ulipaji ni wa mwanzo na endelevu.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, nimemuelewa Mhe. Mwakilishi, naomba nimjibu kwamba tutalizingatia suala hili na tutalifanyia kazi kama vile ambavyo ametoa ushauri.

**Mhe. Wanu Hafidh Ameir:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa maendeleo ni *process* na serikali bado iko katika *process* ya kusambaza haya maji na umeme katika Jimbo la Mtambwe.

Je, mpaka sasa ni vijiji vingapi katika Jimbo la Mtambwe vimeshapatiwa maji na umeme, ukiachia hivi ambavyo Mwakilishi analalamika kwamba havina maji na vyengine havina umeme?

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Naibu Spika, ni vijiji vingi tu ambavyo tayari vimeshapatiwa huduma hiyo, kuna baadhi ya vijiji havijapatiwa. Lakini ili nimjibu vizuri basi nitamtajia vijiji hivyo kimoja baada ya chengine kwa kupitia majibu ya maandishi.

**Nam. 35**

**Dhana ya Kuanzisha Mwenge wa Uhuru**

**Mhe. Saleh Nassor Juma** - Aliuliza:-

Dhana ya kuanzisha Mwenge wa Uhuru pamoja na mbio zake ilisibu sana katika hatua za mwanzo za kupatikana Uhuru wa Tanganyika. Na kwa kuwa katika kipindi tulichonacho hivi sasa dhana hii ya Mwenge wa Uhuru na mbio zake tayari imezuwa hoja na udadisi katika makundi mbali mbali ya kisiasa, dini na hata ya kiuchumi na ustawi wa

jamii. Na kwa kuwa Tanzania ni nchi ya demokrasia na utawala bora na tayari imeshaweka saini katika mikataba mbali mbali ya haki za binaadamu, kwa msingi huo.

(a) Ni lini Serikali zote mbili za Tanzania (SMT na SMZ) itayasikiliza maoni pamoja na mawazo tofauti yahusianayo na uwepo wa Mwenge na mbio zake hapa nchini.

(b) Je, Serikali haioni kuwa kutumia fedha za Serikali pamoja na kusitisha shughuli za utendaji wa Serikali siku za mbio za Mwenge huku watu walio wengi wakiwa hawapendelei zoezi hilo. Huko si kwenda kinyume na dhana ya demokrasia na utawala bora.

**Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto** - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 35 lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali zote mbili za Tanzania (SMT na SMZ) kupitia Wizara zinazoshughulika na vijana, zimeweka utaratibu wa kusikiliza maoni pamoja na mawazo tofauti yanayohusiana na uwepo wa Mwenge wa Uhuru na mbio zake hapa nchini, kila mwaka, baada ya kilele cha mbio hizo, kwa kuwashirikisha Wawakilishi wa Mikoa na Wilaya zote za Tanzania, kupitia mkutano wa Tathmini wa Taifa.

(b) Serikali haijawahi kupokea wazo wala maoni ya watu walio wengi kutopendelea mbio za Mwenge wa Uhuru, wala serikali haijasitisha shughuli za utendaji wa serikali siku za mbio za Mwenge.

Fedha za serikali kupitia Mwenge wa Uhuru zinatumika kuchochea maendeleo kwa kuhamasisha Wilaya, kushirikiana na wananchi kuanzisha na kukamilisha kuwaondolea wanachi kero. Hivyo, mbio za Mwenge haziendi kinyume na dhana ya demokrasia na utawala bora.

Pamoja na kuhimiza miradi ya maendeleo. Pia Mwenge wa Uhuru unatumika kuwaelimisha wananchi mambo mbali mbali ya nchi ikiwemo mapambano dhidi ya Ukimwi, Rushwa, Dawa za Kulevya, Ukatili na Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto, na hasa Katiba na Sheria Kuu ya Nchi.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri pale Mama Mkwe wangu, Bi Zaynabu, naomba nimuulize swali la nyongeza dogo sana kama ifuatavyo.

Kwa kuwa Mhe. Waziri amesema kwamba zinapomaliza mbio za Mwenge, serikali huwa inachukua maoni katika sehemu kadhaa na haijawahi kupata maoni hata moja linalokataa mbio za mwenge. Naomba nimuulize swali hili lifuatalo.

Je, ni mikutano mingapi ya hadhara waliitishwa wananchi kuulizwa, kukubali au kukataa uwepo wa mbio za mwenge, au ni *suggestion box* ngapi, au ni lini itaitishwa *referendum* wananchi kuulizwa swali, mnataka mbio za mwenge au hamtaki. Ni lini mtaitisha kura ya maoni ili muwaulize wananchi juu ya uhalali wa uwepo wa mbio za mwenge, ili kupanua demokrasia na utawala bora katika nchi hii.

**Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto:** Mhe. Naibu Spika, kwamba ni lini tutaweka mikutano ya hadhara na tutafanya kura ya maoni ya anayetaka na asiyetaka.

Mhe. Naibu Spika, suala hili sio la kulazimishwa watu. Kwa hivyo, wanaotaka sisi wakifika kwenye mkutano wa hadhara ndio tunawaeleza nini tulichokikusudia, lakini kwa kusema kwamba tuitishe kura ya maoni, bado Mheshimiwa haijafika wakati huo, kwa sababu naona watu hawajaukataa mwenge.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri, naomba kuongeza nyongeza ndogo kwa Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, kama alivyosema Mhe. Waziri kwamba suala la kutembeza mwenge ni suala la hiyari na kwa kiasi kikubwa utaratibu huu unafanyika kwa ajili ya kuhamasisha maendeleo ya wananchi katika maeneo yao. Kama mnavyojua kila pale ambapo mwenge unapita basi msingi wake mkubwa ni kuhimiza maendeleo ya wananchi katika maeneo hayo, ama kufungua miradi ya maendeleo katika maeneo hayo. Kwa hivyo jambo lolote ambalo linaleta maendeleo katika nchi ni suala la kupewa kipaumbele.

Kwa hivyo, kwa wale ambao bado hawajaelewa umuhimu wa mwenge, ni vizuri tuendelee kutoa elimu hasa hasa nimshajihishe sana Mhe. Saleh Nassor Juma aweze kuimarisha kutoa elimu katika Jimbo la Wawi, waone umuhimu wa mwenge, kwa sababu ipo miradi mingi imefanyika kwenye jimbo lake kupitia mwenge huo. Ni uamuzi wa nchi, tumefanya makusudi Jamhuri ya Muungano kwa nia njema kabisa ya kuendeleza mafanikio katika sehemu mbali mbali za wananchi.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana.

**Mhe. Shadya Mohammed Suleiman:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuweza kunipatia nafasi hii ya kuweza kumuuliza Mheshimiwa Waziri Suala moja la nyongeza.

Mhe. Waziri ningependa kufahamu mwenge mwaka huu uzinduzi weke na kilele chake kitafanyika wapi?

**Mhe. Waziri wa Uwezeshaji Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto:** Mwenge mara hii utazinduliwa rasmi katika Mkoa wa Ruvuma na kilele chake kitafanyika rasmi Mkoa wa Dodoma.

**Mhe. Salim Abdalla Hamad:** Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshiwa Waziri kuhusu suala la mwenge, naomba kuuliza suala dogo la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Kwa sababu suala mama limesema kuwa dhana ya kuanzisha mwenge wa uhuru pamoja na mbio zake lilisibu sana katika hatua za mwanzo za kupatikana uhuru wa Tanganyika, na wakati huo ilikuwa hakuna Tanzania kwa vile mwenge ulihusiana sana na Tanganyika.

a) Je, ilikuwaje mpaka ukaingia Muungano katika shughuli zake.

b) Kama alivyoeleza Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais, kuwa mwenge azma yake ni kuhamasisha maendeleo pamoja na kuweka majiwe ya msingi katika shughuli nyingi za maendeleo. Ni sababu gani zinazofanya Serikali kuwakata wafanyakazi pesa zao katika mshahara ili mwenge huu uweze kutembea.

**Mhe. Waziri wa Uwezeshaji Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto:** Kwanza nianze na hili suala la mwisho ambalo anasema kwamba sisi tunawalazimisha watu kutoa michango, watu wa Serikali tunawalazimisha kutoa michango. Hatuwalazimishi, Mheshimiwa naomba nikuhakikishie kwamba hatuwalazimishi watu wanalipa kwa hiyari zao, wanatoa michango kwa hiyari zao, wakijua kwamba pesa zao zile wanazozitoa hazitapotea lakini zitakwenda katika maendeleo ya majimbo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa nataka nikwambie kwamba kuna mashindani katika Wilaya zetu, yule anayefanya vizuri zaidi huwa anapewa zawadi, kwa hivyo pamoja na michango yake, pamoja na zawadi atakazopata kunakuwa hakuna matatizo yoyote.

Suala la kwanza naomba arudie.

**Mhe. Naibu Spika:** Suala la kwanza anasema kwamba historia ilikuwa ni kupigania uhuru wa Tanganyika imeingiaje mpaka huku Zanzibar?

**Mhe. Waziri wa Uwezeshaji Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto:** Kwaza ninalotaka kumwambia ni suala zima la Muungano sisi Zanzibar tumeungana na Tanzania Bara tangu mwaka 1964 hadi leo, kwa hivyo ndio maana...

**UTARATIBU**

**Mhe. Salim Abdalla Hamad:** Mwenge wa Uhuru ilikuwa ni kutafuta uhuru wa Tanganyika na wakati huo hakukuwa na Tanzania, Tanzania imekuja mwaka 1964 baada ya Mapinduzi ya Zanzibar ikawa nchi zote mbili zina Serikali zao zilizo huru na chochote cha Muungano huwa kipo katika Katiba na kina utaratibu wake wa kuingizwa.

Suala ni kuwa uliingia ingiaje mwenge huu wa uhuru wa Tanganyika mpaka ikawa na sisi tunaushangilia sawa sawa na Tanganyika hapa Zanzibar kama kwamba ni mwenge wa Muungano.

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba niongezee jibu la nyongeza kwa Mheshimiwa Salim kama ifuatavyo.

Ni kweli chanzo cha mwenge wa uhuru ulitokana katika kutafuta uhuru wa Tanganyika, lakini baada ya Muungano wetu na kuona umuhimu wa kuhamasisha maendeleo kwa pande zote mbili za Muungano wetu ndio Serikali zetu zikafanya maamuzi ya makusudi kwamba mwenge ule uwe ni chombo cha Kiserikali kinachohimiza maendeleo ya wananchi wetu, na kama nilivyosema awali kwamba kwenye jambo la maendeleo ndio msingi imara wa mafanikio ya watu wetu.

Kwa sababu hiyo basi ndio maana mwenge ule unatembea mpaka Zanzibar kwa nia na madhumuni ya kuimarisha maendeleo yetu, kwa nia na madhumini ya kumarisha umoja wetu, kwa nia na madhumuni ya kuimarisha muungano wetu.

**Nam. 28**

**Nafasi za Uongozi za Serikali Kuwa Wazi na Kukaimiwa kwa Muda Mrefu**

**Mhe. Saleh Nassor Juma Kny: (Mhe. Jaku Hashim Ayoub)– Aliuliza :-**

Kumekuwa na mazowea ya muda mrefu kwa Serikali yetu kuachia nafasi nyeti za uongozi zinazokuwa wazi au wanaozishikilia kutokuwa na uwezo wa kufanyakazi kwa sababu moja au nyengine na badala yake nafasi hizo kukaimiwa kwa muda mrefu bila ya kufanyiwa mabadiliko.

Je, Kwanini Serikali yetu inachelewa kufanya mabadiliko ya haraka kwa nafasi za uongozi ambazo viongozi wake wamekuwa hawana uwezo wa kuziongoza kwa muda mrefu.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma – Alijibu :-**

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake nambari 28 kama ifuatavyo:-

Suala la uteuzi wa viongozi katika nafasi mbali mbali za Uongozi linatekelezwa kwa mujibu wa Katiba ya Nchi na Sheria. Vifungu nambari 42(2); 47; 50(3) na (4) na 53 (a) na (b) vya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 (Toleo la 2010) vinafafanua na kutoa mamlaka kamili kwa Mamlaka ya Uteuzi, kuteua au kutengua uteuzi pale itakapohitajika. Katika hali hiyo, ni vyema Mamlaka ya Uteuzi ikipatiwa nafasi ya kutosha kutekeleza kazi yake kwa umakini na uadilifu, bila ya kukiuka maadili ya Kiutumishi na Kidemokrasia na hatimae kuvunja Haki za Binaadamu.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Ahsante sana Mheshimiwa pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba kuuliza suali moja la nyongeza.

Kwa kuwa mamlaka ya uteuzi ni sehemu ya viongozi wetu na kwa kuwa hawa wengine nafasi hizi huwa wanakaa nazo mpaka wakati mwengine hawajiwezi kiafya, na wanaendelea kupewa mikataba tu huku wakikaimiwa pamoja na kwamba tumeshawasomesha vijana wengi ambao wana taaluma ya kutosha kuchukua nafasi hizi.

Je, mamlaka za uteuzi kuendelea kuwaachia wazee tu kuwang'ang'aniza kwa mikataba katika nafasi hizi, huku vijana wengi tumeshawasomesha kwa fedha za walipa kodi wa nchi hii ambapo wengine tunalipa kodi katika mazingira magumu sana ya kimaisha yetu.

Je, huoni kwamba Mheshimiwa kuendelea kuwang'ang'aniza wazee hawa huku Mamlaka ya uteuzi ikiwa imekaa kimya, huoni ni wastani wa *public fund* jambo ambalo ni kinyume na maadili ya viongozi wa umma, ambao mswada wake tunaupitisha leo hii tukijaaliwa tusije tukaitwa hapa.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma:** Nataka nirudie pale pale suala la uteuzi ni la mamlaka ambayo Katiba imempa uwezo anayeteua, na hatuwezi kwenda kinyume na hivyo. Mwenyezi Mungu amemjaalia kiongozi wetu ana busara na hekima, anapima wapi panafaa na wapi hapafai, na hakuna nia ya kwamba pana suala la kupoteza pesa za walipa kodi na nini hapa. Ni suala zima la busara na hekima, kwa hivyo hili ni suala la kikatiba na hatuwezi kulivunja, mamlaka haya ya uteuzi yako kwa mtu maalum ambaye kisheria amepewa yeye.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi kunipa asubuhi ya leo kuweza kumuuliza Mhe. Waziri suala la nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa ametuelimisha suala la kisheria na ndio muongozo wa nchi inavyotakiwa, lakini pamoja na hayo kwa kuwa ametwambia kuna mtu ambaye ndio mwenye mamlaka ya kuweza kuteua.

Je, Mhe. Waziri huoni kwa kuwa ni muda mrefu nafasi zile zinakuwa wazi na utendaji unakuwa unazorota, Je, huwezi ukatafuta mbinu za kumwendea ukamshauri Mheshimiwa muhusika akaweza kuteua haraka?

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma:** Kama nilivyosema mimi ni Waziri katika Ofisi ya Rais sawa na masuala ya utumishi yako chini ya Mamlaka ya Wizara yetu, lakini masuala ya uteuzi hayako kwa Waziri wa Utumishi, yako chini ya Mamlaka ya Rais kikatiba. Kwa hivyo yeye anaelewa kile anachokifanya na nina hakika anatuelewa sote kila mmoja na utekelezaji wake wa kazi, kwa hivyo tumuachie kama Katiba imempa madaraka yeye tusimuingilie.

## HOJA ZA SERIKALI

### Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Sheria ya Kupunguza na Kukabiliana na Maafa ya Zanzibar.

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais:** Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba niwasilishe rasmi Mswada wa Sheria ya Kujikinga na Majanga na kukabiliana na maafa ya mwaka 2015.

Kwanza nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaaliya afya njema na uwezo wa kukutana hapa leo ili tuweze kuendelea na shughuli zetu kama tulivyozipanga, tumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa yote anayotufanyia sisi waja wake.

Aidha, nichukue fursa hii kukushukuru wewe Mhe. Naibu Spika, na watendaji wote wa Baraza la Wawakilishi kwa namna mnavyosimamia vyema majukumu ya Baraza letu. Pia, niwashukuru sana sana Wajumbe wa Kamati na viongozi wakuu wa kitaifa kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kusimamia kazi zetu maelekezo na ushauri wanaotupa yanakuwa dira ya utendaji wa shughuli zetu.

Vile vile, nitoe shukurani maalum kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya katika kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, kazi za kukabiliana na maafa hapa Zanzibar zinasimamiwa kwa kutumia sheria ya kukabiliana na maafa namba mbili ya mwaka 2003 pamoja na sera ya kukabiliana na maafa ya mwaka 2011, katika kutekeleza Sheria namba mbili ya mwaka 2003 imebainika kwamba sheria hii ina mapungufu ambayo yanakwamisha utekelezaji wa shughuli za kujikinga na kukabiliana na maafa hapa Zanzibar. Mapungufu hayo ni pamoja na kutokuwepo kwa uwiano baina ya sera na Sheria kukabiliana na maafa, kukosekana kwa muundo wa usimamizi wa masuala ya maafa katika ngazi za Wilaya na Shehiya na kukosekana kwa mfumo madhubuti wa utoaji taarifa za maafa.

Mapungufu mengine ni kutokujihusisha ushiriki wa sekta binafsi na wadau wengine muhimu wa maafa na kujikita zaidi katika masuala ya uokozi na kuacha masuala muhimu ya kujiandaa, kujikinga na kurejesha hali baada ya maafa. Mhe. Naibu Spika, kutokana na mapungufu hayo Serikali imeona ipo haja ya kutunga Sheria mpya ya kukabiliana na maafa ili kukidhi mahitaji ya sasa na mahitaji ya baadae.

Mhe. Naibu Spika, madhumuni ya taarifa hii ni kuwasilisha Mswada wa Sheria mpya ya kukabiliana na maafa katika Baraza lako tukufu ili Waheshimiwa Wajumbe wapate fursa ya kuupitia, kuujadili na hatimae kuukubali mswada wa Sheria mpya ya kukabiliana na maafa ili tujenge mazingira mazuri ya kukabiliana nayo katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, Mswada wa Sheria ya Kukabiliana na Maafa umegawika katika sehemu nane na una jumla ya vifungu 48, mchanganua wa vifungu hivyo ni kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, sehemu ya kwanza ya Mswada huu una jumla ya vifungu viwili na kifungu cha kwanza kinahusu Masharti ya utangulizi yanayojumuisha jina fupi la sheria na kuanza kutumika kwake.

Kifungu cha pili kinahusu tafsiri ya misamiati inayotumika katika Mswada huu. Mhe. Naibu Spika, sehemu ya pili ya Mswada huu ina jumla ya vifungu vinane kuanzia kifungu cha tatu hadi cha kumi, vifungu hivyo vinaelezea kuhusu kuundwa kwa Kamisheni ya kukabiliana na maafa, Wajumbe wa Kamisheni, Kazi za Kamisheni, Uwezo wa Kamisheni, uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji, kuanzishwa kwa Secretariet ya Kamisheni, Vitengo vya Kamisheni na kazi za Secretariet ya Kamisheni.

Mhe. Naibu Spika, sehemu ya tatu ya Mswada huu ina jumla ya vifungu kumi na nne(14) kuanzia kifungu cha 21 hadi cha 24, vifungu hivi vinazungumzia kuhusu uanzishwaji wa Kamati ya kukabiliana na maafa katika ngazi ya taifa, Wilaya na Shehia na Wajumbe wa kila kamati na majukumu ya kamati hizo pamoja na kuelezea utaratibu wa uendeshaji wa vikao vya Kamati.

Mhe. Naibu Spika, sehemu ya nne ya Mswada huu ina jumla ya vifungu vinne kuanzia kifungu cha 25 hadi 28 vinavyoelezea kuhusu utayarishaji wa mpango wa kukabiliana na maafa katika ngazi ya taifa Wilaya na sekta na utaratibu wa kutoa miongozo kuhusu utayarishaji wa mipango hiyo.

Mhe. Naibu Spika, sehemu ya tano ya Mswada huu ina jumla ya vifungu saba kuanzia kifungu 29 hadi 35, vifungu hivyo vinatoa maelezo kuhusu aina za maafa na utaratibu wa kutangaza hali ya maafa katika ngazi ya taifa Wilaya na Shehiya. Aidha, sehemu hii pia ina vifungu vinavyotoa maelezo kuhusu utaratibu wa kutoa maagizo katika masuala ya kukabiliana na maafa, upatikanaji wa nyenzo za kukabiliana na maafa wakati wa maafa na uwezo wa kamisheni na taasisi nyengine wakati wa dharua za maafa.

Mhe. Naibu Spika, sehemu ya vifungu ina jumla ya vifungu sita kuanzia kifungu cha 36 hadi 41 vinavyoelezea masuala ya bajeti na upatikanaji wa fedha, na matumizi ya kamisheni, ukaguzi wa mahesabu na suala la uanzishwaji wa mfuko wa kukabiliana na maafa pamoja na madhumuni yake.

Mhe. Naibu Spika, sehemu ya saba ina jumla ya vifungu vitatu kuanzia kifungu cha 42 hadi 44 vinavyoelezea makosa na adhabu.

Sehemu ya nane inahusu masharti mengineyo na ina jumla ya vifungu vinne kuanzia kifungu cha 45 hadi 48 vinavyoelezea kuhusu kinga ya Afisa wa Kamisheni, utoaji wa taarifa za maafa, uwezo wa Waziri kutunga kanuni kufuta na kubakiza sheria ya kukabiliana na maafa namba mbili ya mwaka 2005.

**HITIMISHO**

Mhe. Naibu Spika, ni imani yangu kwamba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu wamepata wasaa wa kupitia Mswada wa Sheria inayopendekezwa na hivyo kutoa michango yao na hatimae kukubali mapendekezo ya kuwa sheria mpya ya kukabiliana na maafa.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Naibu Spika, sasa naomba kutoa hoja.

**Mhe. Salmin Awadh Salmin:**...

(*Hapa hakutumia kipaza sauti)*

Kwa hivyo, haifai kujadiliwa. Kwa sababu kwa mujibu wa Kanuni zetu hoja ambayo inawasilishwa hapa kabla ya kujadiliwa inatakiwa kwanza iungwe mkono. Sasa Mhe. Waziri alipotoa hoja hakuna Mjumbe hata mmoja aliyesimama kuunga mkono. Kwa hiyo hoja hii kwa mujibu wa Kanuni hairuhusiwi kujadiliwa.

Mhe. Naibu Spika, ahsante.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Naibu Spika, baada ya kumsikia Mheshimiwa Mwakilishi Salmin Awadh Salmin. Naomba nirudie tena kusema naomba kutoa hoja ili upande wa serikali...

**Mhe. Naibu Spika:** Asante Mheshimiwa hoja imeungwa mkono, tunaendelea. Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi ya Viongozi Wakuu. Maoni ya Kamati.

**Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Baraza la Wawakilishi Kuhusiana na Mswada wa Kuanzisha Sheria ya Kupunguza na Kukabiliana na Maafa Zanzibar Na Mambo Mengine Yanayohusiana Nayo**

**Mhe. Shadya Mohammed Suleiman (Kny/Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa):** Mhe. Naibu Spika, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kwa mara nyengine tena kufika na kuweza kukutana mbele ya Baraza lako Tukufu tukiwa wazima na wenye afya njema, kwa lengo la kujadili mambo mbali mbali yanayohusu maendeleo na ustawi wa nchi yetu na watu wake, ikiwemo kupitisha miswada mbali mbali ukiwemo mswada huu ulio mbele yetu, Mswada wa Kuanzisha Sheria ya Kupunguza na Kukabiliana na Maafa Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana nayo.

Aidha, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu ili niweze kuwasilisha kwa niaba ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Baraza la Wawakilishi maoni kuhusu Mswada niliokwishauainisha hapo juu.

Mhe. Naibu Spika, pia naomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya Kamati, kuishukuru kwa dhati serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kwa kuweza kuona umuhimu wa kuleta mswada mbele ya Baraza ili uweze kujadiliwa na kupitishwa na kuweza kufikiwa lengo lililokusudiwa la kuwa na sheria madhubuti itakayoweza kusaidia kupunguza, kuzuia na pia kukabiliana na Maafa pale yanapotokezea.

Mhe. Naibu Spika, baada ya utangulizi huo Kamati inapongeza hatua zilizochukuliwa na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ya kuwasilisha mswada huu muhimu ambao utasaidia sana kupunguza changamoto na athari zinazoikabili jamii juu ya maafa pale yanapotokezea.

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba nichukue nafasi hii, kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati kwa michango yao muhimu waliyoitoa wakati tulipokuwa tukiujadili na kuupitia mswada huu ambapo mawazo na mapendekezo yao yamewezesha leo hii kufika hapa na kuweza kuwasilishwa mbele ya Baraza lako Tukufu na hatimaye kupitishwa kwa ajili ya kufikiwa lengo lililokusudiwa na serikali kwa maslahi ya nchi yetu. Naomba sasa kwa ruhsa yako niwataje Wajumbe wa Kamati yetu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kama ifuatavyo:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Hamza Hassan Juma | - | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Saleh Nassor Juma | - | M/ Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Ali Mzee Ali | - | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | - | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Subeit Khamis Faki | - | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Ashura Sharif Ali | - | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Shadya Mohamed Suleiman | - | Mjumbe |
| 8. | Ndg Rahma Kombo Mgeni | - | Katibu |
| 9. | Ndg Makame Salim Ali | - | Katibu. |

Mhe. Naibu Spika, baada ya utangulizi huo sasa napenda kutoa maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa juu ya Mswada huu uliopo mbele yetu kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, maoni hayo ya Kamati yamejikita zaidi katika kuuboresha mswada wenyewe lakini pia kusawazisha baadhi ya makosa ya kiuandishi, kilugha na uchapaji kama ifuatavyo:

Kifungu cha 4(3)(c) kisomeke Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi". Sababu ya marekebisho haya ni kufuatana na mpangilio wa cheo hichi kama ilivyotajwa kwenye Katiba.

Aidha, Kamati imefanya marekebisho kwa kuongezwa aya mpya ya (j) inayosomeka "Mkurugenzi wa Bandari". Sababu ya marekebisho haya ni kutokana na umuhimu wa nafasi yake na uhalisia wa majanga na maafa yanayotukumba zaidi huwa yanatokea upande wa Baharini ambapo yeye kwa nafasi yake ni vizuri akajumuishwa.

Kifungu cha 21(g) kirekebishwe kwa kufutwa neno "Kamisheni" na badala yake liwekwe neno "Wilaya". Kamati yangu imeona kuwa kamati ya maafa ya wilaya haiwezi kupokea moja kwa moja maagizo kutoka Kamisheni isipokuwa itapokea kutoka Wilaya kwa mujibu wa ngazi za kiutawala.

Kifungu cha 47 kirekebishwe kwa kufutwa neno "anaweza" lililojitokeza katika mstari wa kwanza na wa pili na badala yake liwekwe neno "atatunga".

Sababu za marekebisho haya ni kwamba Kamati yangu imeona neno anaweza mara nyingi limekuwa likiwafanya mawaziri kukwepa kutunga kanuni kwani hakulazimishwa na Sheria mama kutunga Kanuni ndiyo maana kamati yangu ikaweka neno waziri atatunga ili kuhakikisha anatunga Kanuni na kurahisisha utekelezaji wa Sheria hiyo.

Mhe. Naibu Spika mbali na hayo kamati yetu ilifanya marekebisho kama inavyojionesha kwenye jadweli la marekebisho.

Mhe. Naibu Spika, kamati yangu inaipongeza sana Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa kuleta sheria hii ambayo inaifuta ile Sheria No. 2 ya mwaka 2003 iliyokuwepo mwanzo, ambayo ilikuwa na mapungufu mengi jambo ambalo lilikuwa linakwamisha na kupunguza juhudi na mipango ya kukabiliana na maafa hapa Zanzibar. Lakini kwa kupitishwa kwa sheria hii mpya itarahisisha utaratibu wa kukabiliana na maafa.

Mhe Naibu Spika, aidha sheria hii itaenda sambamba na Sera ya Kukabiliana na Maafa ya hapa Zanzibar, pamoja na makuliano ya mikataba ya kikanda na ile ya kimataifa ambayo Tanzania imeridhia, kwa madhumuni maalum ya kuzuia na kupunguza athari zinazotokana na maafa pale yanapotokezea.

Mhe Naibu Spika, hapa ndipo inapoonekanwa umuhimu wa Wajumbe wako kushiriki katika mikutano mbalimbali inayofanyika Duniani na kupitishwa kwa maazimio ambayo nchi wanachama baadaye hulazimika kutunga sheria katika nchi zao. Sasa hapa naomba kuwasilisha kilio cha wajumbe wako kuhakikisha wajumbe wa Kamati zako za kudumu za Baraza wanapata "*Exposure*" na kujifunza uzoefu wa nchi nyengine namna na mbinu wanazozitumia katika kukabiliana na majanga mbali mbali katika nchi zao na kuweza kuzileta huku kwetu ili kupunguza hizo athari za maafa. Kwani wakati kama huu wa kutunga sheria ndio utaona umuhimu wa uzoefu na taaluma katika kuishauri serikali.

Mhe Naibu Spika, sehemu ya pili ya mswaada huu inazungumzia kuundwa ka Kamisheni nguvu zake, uteuzi wa mkurugenzi pamoja na sekretarieti. Sehemu hii itaongeza ufanisi katika uhuru wa kubuni mbinu na maarifa ya kuweza kutafuta nyenzo na pesa za kukabiliana na maafa, ambapo kwa hivi sasa mkurugenzi anafanya kazi kama ni idara tu ya serikali ambapo sheria zinaambatana katika kubuni mbinu mpya za kutafuta pesa na nyenzo za kukabiliana na maafa. Kwa hiyo ni matarajio ya Kamati yangu kuwa kuanzishwa kwa Kamisheni kutaongeza ufanisi katika kukabiliana na maafa.

Mhe Naibu Spika, sehemu ya tatu ya mswaada huu kama inavyoeleza sheria hii, kuwa kutakuwepo kamati za maafa za wilaya ambazo kutakuwepo wajumbe wakiwemo Wawakilishi na Wabunge husika katika wilaya zao, ambao watabuni mbinu za kukabiliana na maafa pia kuweza kuhamasisha wananchi na taasisi mbali mbali kuuchangia mfuko wa maafa ambao utawasaidia wale watakaoathirika na majanga na maafa katika maeneo yao. Hii itasaidia kuondoa malalamiko ya wale wanaopata majanga kuweza kupata huduma kwa haraka iwezekanavyo, ili kupunguza makali ya athari za maafa au majanga yaliyowakumba.

Mhe Naibu Spika, sehemu ya nne na ya tano ya mswada huu inaelezea kuhusu kutangaza. Utayarishaji wa mipango ya kukabiliana na maafa na utaratibu wa upatikanaji wa nyenzo kutoka ngazi ya juu hadi Shehia ambapo itasaidia kuweka mgawanyo wa madaraka na kiutendaji ili kuharakisha utekelezaji wake katika kuzuia, kutoa tahadhari na kukabiliana na maafa katika ngazi zote zilizotajwa katika sheria hii.

Mhe Spika, jambo hili ni muhimu kwani tumeona changamoto nyingi hasa pale yanapotokezea maafa tatizo linakuwa haonekani kiongozi wa kutoa amri, ambapo mipango yote inabidi itoke hapo na miongozo yote pia itoke hapo pamoja na usimamizi wake, hasa kwa majanga yanayotokea Baharini ikiwemo kuzama kwa meli ambapo huchukua muda mrefu kuwahi kutoa huduma kwa wahanga na kupelekea maafa makubwa. Kwa hiyo kwa kupitishwa kwa sheria hii itasaidia kuondoa urasimu ili kuwahi kutoa huduma kwa wakati.

Mhe Naibu Spika, sehemu ya sita inaelezea upatikanaji wa fedha, ikiwemo zile zinazoidhinishwa katika bajeti ya Serikali kwa ajili ya uendeshaji, lakini pia kuanzishwa kwa Mfuko wa Maafa ambapo utasaidia utekelezaji wa kukabiliana na maafa. Lakini pia mfuko huo utaweza kuchangiwa na nchi, taasisi, mashirika, makampuni na watu mbali mbali ili kuwepo pesa wakati wote kwani majanga yanapotokea huwa hayatoi taarifa na hutokea ghafla, kwa hiyo jamii inakuwa haijajiandaa kukabiliana na hali hiyo, kwa hiyo mbinu mbali mbali zitakazotumika zitasaidia kuutunisha mfuko huo.

Mhe Naibu Spika, sehemu ya saba inazungumzia makosa na adhabu kwa mtu yeyote atakayekusudia au kukwamisha kwa makusudi shughuli za kukabiliana na maafa, kwa mujibu wa sheria.

Mhe Naibu Spika, kamati yangu imeridhika na jitihada za serikali za kuandaa mipango ya kukabiliana maafa kwa kuleta Mswaada huu ili kupunguza makali ya maafa pale yatakapotokea, na nawaomba Wajumbe wote, kuuchangia, kuuboresha, na hatimaye kuupitisha ili uwe Sheria ili kuweza kutoa huduma bora wakati wa kukabiliana na maafa.

Mhe Naibu Spika, naomba pia kuchukua nafasi hii kuwashukuru wajumbe wangu wa Kamati kwa kuweza kunipa mashirikiano muda wote hadi kuweza kuwasilisha ripoti hii ya kamati yako.

Mhe. Naibu Spika, aidha napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii na Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa umakini mkubwa na wa hali ya juu, kwa niaba ya Kamati naunga mkono hoja.

Mhe Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**Mhe Naibu Spika:** Asante Mhe. Mwenyekiti, hoja imeungwa mkono. Waheshimiwa Wajumbe mpaka hivi sasa nina wachangiaji wawili tu, kwa hivyo naomba yule mwenye nia ya kuchangia alete jina mapema ili tuweze kujipanga uzuri katika utoaji wa michango yenu. Kwa hivyo namuanza Mhe. Makame Mshimba Mbarouk na pili Mhe. Ali Salim Haji. Kwa hivyo mwenye nia ya kuchangia alete ili tuweze kuweka vizuri katika kuchangia.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Naibu Spika, nashukuru sana leo hii kuweza kuutia baraka Mswada huu wa kujikinga au wa kujilinda na maafa. Nimshukuru Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote akiwemo Katibu wake, wakurugenzi na kadhalika.

Mhe. Naibu Spika, Zanzibar ni Kisiwa, lakini watu wengi hawajajua nini maana ya maafa au nini maana ya kujilinda na maafa yanapojitokeza. Kawaida yetu huwa tunachelewa lakini tunapochelewa basi tunakuwa tunaleta Miswada ambayo ni mizuri sana. Hii siku zote mimi huwa nasema tuletewe Miswada mapema kwa wale wajumbe ili waweze kuchangia jambo lililokuwa lenye mazuri zaidi. Lakini hata hivyo wana *experience* wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kwa uzoefu wao huwa wanapenda sana na wana taaluma ya kuweza kuchangia vizuri.

Mhe. Naibu Spika, mimi nikianza na ukurasa wangu huu wa 299 kuna mambo hapa yameainishwa yakijieleza na hasa katika kipindi hichi cha kujiandaa na maafa. Mheshimiwa ni kweli sawa sawa na binaadamu wote sasa hivi ni walemavu watarajiwa. Usijione mzima ukajiona na ukasema mimi ni mzima lakini kumbe ujiweke katika hali halisi ya ulemavu wa utarajiwa.

Mhe. Naibu Spika, haya maafa ni suala ambalo halina wakati maalum. Sasa mimi niwashukuru sana Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa kutoa indhari au kufahamisha jinsi gani kinga inatakiwa likitokezea jambo la maafa. Wameandaa utaratibu mzuri sana ambao sasa hivi tutakuwa tuna Kamisheni ambayo itakuwemo humu. Kamicheni itakuwa na muundo wake na utendaji wake wa kazi na ni vizuri wameonesha jinsi gani viongozi watakaohusika katika Kamisheni. Lakini isitoshe vile vile mpaka Sheha na yeye anakuwemo katika mtendaji wa Kamati hizo za maafa.

Mhe. Naibu Spika, takriban Masheha wa Zanzibar niseme hawajajua nini maana ya maafa, huo ni ukweli usiopingika. Kwa namna moja au mbili hawajapata taaluma. Hilo nakubaliana nalo, na hawaoneshi sehemu gani ambayo labda mnawahusisha, sijui kwenye nini. Au kama kuna sheria gani ambayo kama ilikuwepo huko nyuma Mhe. Waziri utanisaidia, kama kulikuwa hakuna na sasa hivi ndio tunaifanya sheria ya kuwaweka basi ni vizuri sana, nasema *well, good* kabisa.

Mhe. Naibu Spika, sasa hivi maafa yanatokea katika shehia lakini ripoti wapi wazipeleke. Mheshimiwa masheha wengine hawajui. Sasa kwa kuwa sheria hii ipo imenifurahisha sana Mhe. Naibu Spika. Majimbo yetu au shehia zetu ndipo kunakotokea matatizo, lakini hata na mimi Mhe. Mwakilishi inapotokea maafa nashindwa wapi hilo tatizo nikaliripoti. Hili niseme ukweli sio vibaya wala si dhambi, kusema ukweli, unaambiwa useme ukweli na ndivyo inavyotakiwa. Kiongozi yoyote ni lazima awe mkweli katika kufanya jambo. Jambo hulijui sema silijui tu, usijitie unalijua kumbe hulijui hata *definition* yake utakuwa unajisemea ovyo tu, hilo linakuwa sio jambo zuri Mhe. Naibu Spika.

Lakini baada ya kuletwa Mswada huu nimejifahamu hata na mimi nitakuwa mjumbe kwenye Kamati hizo kwa kupitia ngazi za Wilaya. Nimeelewa Mhe. Naibu Spika, hainipi shida. Lakini sasa natafuta njia ya kujua kuwa nitajilinda vipi inapotokezea maafa au sababu zipi zinazosababishwa na mwananchi kuleta maafa.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwenye jimbo langu niseme sehemu nyingi sana kuna wananchi wanapigiwa minazi nyumba zao, nyumba zao wanaunguliwa masikini ya Mungu. Lakini utakuta watengenezaji ni Wawakilishi na Mbunge, lakini kumbe tuna Mkurugenzi anayehusika na masuala kama yale, tunamuacha. Sijui kwa sababu tunamuacha kwa kuwa tunamuona hana pesa, bajeti yake ni ndogo ya kuweza kusaidia yale maafa, inawezekana hiyo.

Mhe. Naibu Spika, huo ndio ukweli ulivyo, kwa sababu tunapokuwa sasa hivi tunaandaa na hili ndio tatizo linalotupa tabu kabisa. Tunaandaa mambo mazuri lakini hatuangalii bajeti yetu ikoje. Huyu Mkurugenzi tunampa kitengo kikubwa sana cha nchi nzima niseme, sio kitu cha masihara. Lakini bajeti yake inasikitisha na inatia huzuni, ataweza wapi kuya- *control* maafa.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu nchi za wenzetu wanavifaa vya teknolojia ya kuelewa wakati gani upepo unakuja ambao utaleta athari katika nchi. Yeye masikini ya Mungu hata hiyo ofisi sijui kama anayo, na hata kama anayo itakuwa si ya *modern*. Kwa sababu inatakiwa Mkurugenzi Mwenyewe aweze kuona na kuwa na vitu vile vya kuweza kuona mambo ya majanga. Sasa sijui, labda atakuwa na *television* ya kawaida anaangalia katika ulimwengu.

Sasa ile ni moja Mhe. Naibu Spika, ningeomba sana kuwa tuwe *serious* katika hii miswada tunayoleta. Tumeona majanga mengi yametutokezea, lakini yote majanga yale tatizo lenyewe vifaa hatuna viliokuwa *strong* na vinakwenda na wakati vya kuweza kuokoa majanga kama yale.

Mhe. Naibu Spika, nikiuliza kwenye ghala yake Mkurugenzi hana. Naiomba sana Serikali Kuu kupitia Mhe. Waziri wa Fedha mswaada huu auone kwa huruma kabisa, kwa sababu ndio mlengwa mkubwa ni yeye wa kuwatafutia *funds,*yaani kwa kuwatafutia bajeti yao *within a time* iingie kwa wakati ili kuweza kuokoa. Kwa sababu kama nilivyosema hili suala la maafa halina *time* maalum. Kwa mfano juzi kulikuwepo kwa Mhe. Subeit, nyumba chungunzima zimeizuliwa mabati, tena wameonesha jitihada nzuri sana, kwa hilo ninawashukuru sana. Mheshimiwa nipongeze sana wamekwenda kule na baada ya kufika wametekeleza wajibu, nyumba zimepigwa mabati na watu wamepewa vifaa, ile ndio inavyotakiwa, ndio maana yake ukiwa na fedha unatakiwa upeleke pale masuala kama yale.

Nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa utekelezaji ule tena sana na hongera sana, panapo sifa mimi ninakupa vitu vyako, usiwe na wasiwasi pamoja na Mkurugenzi.

Mhe. Naibu Spika, ile ndio hali halisi inavyotakiwa, hata nchi za wenzetu na nimesikia hapa Mheshimiwa wangu Mwenyekiti alitoa taarifa, suala la kwenda kupata maelimisho, jinsi gani watu kuweza kuokoa, mimi nakubaliana nalo, *of course* si lazima Baraza la Wawakilishi au Kamati, lakini kwenye Kamati hizi naomba sana Mheshimiwa zielekeze huko, kwa sababu hawa wajumbe wanatakiwa na wao wajue dhana hii kubwa ya kuwa yeye ni mjumbe katika masuala ya maafa.

Mhe. Naibu Spika, naomba sana wajumbe watakaoingia katika Bodi na wajumbe watakaokuwa kwenye Kamati nazo naomba sana Mhe. Waziri zipatiwe *funds*. Tena hii imo katika Wizara kubwa, kwa sababu mimi linanisikitisha jambo moja kuwa Wizara ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar nikisikia kuambiwa ina bajeti finyu mimi ninakuwa ninaumia sana kwa sababu ndio mtendaji mkuu wa Serikali nzima ya Zanzibar na tunatangaza uchumi unakuwa kila siku hadi siku, tusiwe wabahili wa kutoa hela jamani. Nataka kusema tusiwe wabahili katika hilo, tuiwekeze fedha kabisa pale panapo umuhimu kwa jamii kwa sababu yeye ana *rotation* kubwa ya wananchi, yeye mfuko wake anao akitoa mfukoni mwisho utatoboka,yaani atakuwa anatoa kila siku tu mfukoni mwake haiwezekani.

Mhe. Naibu Spika, anatoa lakini haiwezekani sasa, nalo hili tulione lina msingi. Siku moja tulifanya harambee ya meli hapa tukakata bajeti sehemu nyingi, yaani tukakata kidogo kidogo, kwa nini tushindwe na hili. Ina maana

sheria tukiipitisha lazima tufanye harambee tuwatafutie njia ya kupata *funds*, lazima wizara husika tugawe kidogo kidogo ili tuoneshe mfuko wa kutononeka *and then* watakuja watu wa nje nao watachangia.

Kwa sababu Mkurugenzi na yeye halali usingizi na atatafuta *donors* wa kuweza kumsaidia pale, lakini keshajua ndani ana mabilioni ya fedha. Mhe. Naibu Spika, sasa nalo hilo niseme nichangie jumla kwa jumla kwa sababu mimi mwenyewe ni mjumbe wa hii Kamati nitakwenda jumla jumla jinsi gani nilivyojisikia raha kabisa kuweza kufahamu kujua sasa hivi tuna maafa ya aina mbili; kuna maafa makubwa makubwa ambayo ndio tunayosema ya kishehia, sasa tizama uzuri wa mswada huu imeeleza sheria hizo zitakuweko huo, ndio hiyo tunaanzia katika shehia, kwa mfano mtu akipigwa na mnazi au kupigwa na nini.

Sasa mimi nashukuru sana hivi kipindi cha kati tu kwenye majimbo minazi mingi sana imewaangukia. Halafu naomba sana kuwe na *control* sheha aweze kuleta barua *official* ili moja katika kunusuru masuala, kuna nyumba sasa hivi ziko karibu na minazi kama unavyojua Zanzibar kwetu misitu yetu mikubwa ni minazi. Na hili Mkurugenzi naomba sana wanapoletewa barua za kuwasaidia angalau, ndio kukinga kwenyewe huko; kukata minazi, kukata miembe ambayo iliyo karibu na nyumba kwa sababu kila siku ukacha tunazaa, ina maana *population* inazidi kuwa kubwa, ardhi yenyewe ni ndogo.

Hiyo hiyo ardhi tunataka tulime na tunatakiwa ardhi tuweze kufanya mambo mengine, sasa kwa kuwa tunaanza kutafuta njia za kinga ili maafa makubwa yasitokezee, sasa ni moja katika kujiandaa moja ni hilo. Kwa sababu ninaomba sana Mkurugenzi wa Maafa ashirikiane na Mkurugenzi wa Misitu ili wakubaliane na kuweza kuwahurumia wale wananchi ambao minazi yao imekaa karibu ya mapaa. Jamani hilo suala tulifanye *immediately* kabisa, Mkurugenzi shuka chini na nenda katika shehia kaangalie ili kuweza kuwasaidia wananchi kuwaokoa katika janga hili ili lisitokezee.

Mhe. Naibu Spika, tatizo letu ni moja linatukuta ambalo hilo siku zote huwa ninapiga kelele. Tatizo tunalolizungumzia hapa nitafurahi sana Mheshimiwa wangu Mkurugenzi wa Maafa, hasa achukue *example* katika Jimbo la Kitope na aende kule Fujoni akaangalie sehemu ya minazi inakaribiana kabisa na paa, lakini anashindwa kuukata ule mnazi kwa sababu hajapata kibali, anashindwa pengine yule mwenye eka aliyemuuzia ile sehemu ndogo ya kujenga anamkatalia, sasa ana maana gani. Naomba sana Mheshimiwa hili suala nenda kawaokoe pale Fujoni, la kama si hivyo tutatoa mafedha na tutauwa watu, wacha kutoa fedha, fedha si kitu fedha zinachumwa, lakini roho inachumwa na nani, ikitoka imetoka tu. Kwa hivyo, mimi naomba sana.

Lakini la pili, jinsi gani sasa wananchi wetu kwa kupitia radio, kwa kupitia semina, kwa kupitia kuunda Kamati ndogo ndogo katika shehia ili jinsi gani jamani ee, tukitaka kuokoa moto au lisijitokeza jambo la moto tunatakiwa tuwe katika *model* gani au tukimbilia *defence* ya aina gani ili tujilinde. Sasa nalo hilo ningeomba sana Mheshimiwa hii tutakupitishia tu Mheshimiwa wala msiwe na wasiwasi wowote. Lakini kuna mambo ambayo ni lazima tujiandae tuwe na *draft* ya kuweza kufanya hizi kazi, sio tunapitisha sheria *and then* inaingia kwenye *briefcase* mchezo umeisha, hii Mheshimiwa inakuwa haileti maana. Na mimi ninavyokujua Mhe. Waziri na kijana wako Mkurugenzi mko shupavu sana na hasa Katibu, huyu Katibu wako ni Dokta kweli kwa sababu huwezi kupewa mtu udokta wa kubuniwa buniwa kama mimi.

Mimi unaweza ukanita Dokta, lakini udokta wangu mimi ndio hivyo tu, lakini kuna mtu ukimwita Dokta ni Dokta kweli, si kitu cha mchezo, ni mtu ambaye anakuwa na tija katika wizara na fani yake anaitumia kwenye Wizara. Nimshukuru sana anapoondoka anaacha jina na hiyo ndio inavyotakiwa, ndio sifa ya kiongozi yoyote. Saa nyengine mimi humsifu sana Dr. Shein kuwa anapotuchagulia watu anachagua watu *bright* kweli, sasa ile mtu tena ni udhaifu wake mwenyewe kutokufanya jambo. Nampa sana pongezi wala sina haja nae kutaka kitu chochote, yeye hana uwezo wa kunisaidia chochote, lakini ninampa sifa yake kutokana na udokta wake aliokuwa nao, hiyo ukweli tuseme. Kusimamia jambo likawa ni *ratio* ya kuonesha udhibiti na uwezo wako katika akili na ni upungufu wa kutokuwa udokta kusimamia jambo likawa halijawa.

Mhe. Naibu Spika, sasa hili ni suala la majanga na kama amesimamia ni *active* kweli huyu, mapungufu madogo madogo lazima yamshinde hana *helicopter* na *speed boat, of course,* hiyo hatuwezi kumlaumu, lakini yuko katika ku-*plan*, *just plan, plan* unajua ukipange kitu kikaenda kwa wakati Mhe. Naibu Spika, basi ndio tunavyotaka iwe.

Sasa tizama huu muundo, kwa mfano ukurasa huu wa 302 kazi za Kamisheni yenyewe inasema; kuwezesha

upatikaniji wa fedha kwa raslimali nyengine kwa wakati wa dharura za maafa. Nani mwengine anaweza kuona *knowledge* kama hiyo. Kwa sababu Serikali inaweza ikawa *sometime* ikawa haina, ndio kama nilivyosema bajeti yake haikupita kwa *time*, haikuingia kwa *time,* lakini imetokea janga hili la kuweza kuokoa, anajua wapi *funds* hizi mimi nitakwenda kuzipata za haraka haraka kusaidia wananchi. Na kama huwi mzuri na huongei vizuri, huwezi kupata mambo kama haya, hebu tizameni tumepata fedha ngapi, kila mtu kaleta fedha zake, tumechangia yalipotokea maafa yale madogo madogo.

Mhe. Naibu Spika, niseme kwanza tuwe na maelimisho katika benki, naomba sana wizara ziwe karibu na mabenki kuwaelimisha kwa sababu mabenki na wao wanakuwa na mfuko wa kusaidia jamii. Napenda sana benki zote zilivyokuwa zimeji-*register* hapa Zanzibar na wao *PBZ, NMB* na benki nyengine, basi niwashukuru sana kwa sababu na wao waweze kuelewa hii dhana ya maafa jinsi gani na wao watakuwa *control* kukitokea janga kwa kupitia kuekeza katika Serikali, mimi hili niseme kuwa wawe karibu na kuonesha sera zao kuwafahamisha jinsi gani ambavyo wanaweza *anytime* kupiga mlango waweze kusaidia kutokufungwa. Kwa sababu kule benki na wao wanakuwa na vifungu vya kuweza kuwasaidia watu wenye matatizo, ninawashukuru sana wanafanya hilo jambo. Utakuta *NMB* na *Barclays* leo kasaidia wapi, kasaidia wananchi wenye hali ngumu na halikadhalika na watu wengine. Mheshimiwa hili suala ninashukuru sana wenye mabenki walio-*register* Zanzibar wamo katika hali halisi ya kusaidia.

Lakini na wao japo humu sikuwaona kwenye sheria hii, sitaki niilazimishe Mheshimiwa Waziri na Mwanasheria, kama ikiwezekana na wao tuwaingize humu, hii ni *key,* yaani ufunguo wao wa kuweza kupata mambo humu ya kuweza kusaidia kupata *funds* kiasi likitokea jambo la ghafla, lakini humu kwenye sheria sijawaona. Jana nilijaribu kupekua sana nilisahau miwani, *of course,* unajua utuuzima nao unaenda, sasa miwani sikuchukua kwa maana hiyo nilikuwa natizama *roughly* tu. Lakini leo nimechukua miwani nimeona hawa watu hatukuwaingiza humu, naomba sana Mheshimiwa *special* hii nione tu tuwajengee na wao heshima tuangalie tutawaingiza katika maeneo gani katika hizi kada tulizoziweka humu.

Sasa tukisema tuwaweke basi tutaangalia ana sheria itatwambiaje, Mwanasheria ajaribu, sheria haina *definition*, sheria ina upana mrefu na ukaangalia hali halisi ya kuwa hii haitotoa hasara katika sheria mama basi naomba waingizwe na wao humu na wao hawa watakuwa na mchango mkubwa tukiwataja kwa sababu tumewataja humu; tumemtaja Mkuu wa Mkoa, Kamanda, Kamishna na kuna watu wengine ambao waziri ataona wanafaa. Sasa mimi naomba tuwaingize hawa kwenye mabenki na ndio mtego wenyewe, ndio mtama huo. Kwa sababu ukiwatia mle unaita katika Kamati yako jamani ee, kumetokea hili, basi wao kwa kuwa wale wenzetu wana vifungu vile katika sheria zao za kibenki basi hutopata shida katika kuanzisha kuokoa katika maafa yale.

Mhe. Naibu Spika, ningeomba sana kama kuna uwezekano tungekuwa na *special radio* ya kuweza kuangalia hali ya hewa, hali ya mtiririko kila baada ya *time* na kuweza kuwaeleza wananchi, nalo hilo lingetusaidia sana. Kwa sababu wenzetu jambo la mwaka kesho wanaliona leo, wanaanza kulitolea taarifa, nalo hili naomba sana Mheshimiwa ili kwa kuupa huu mswada nyama tungeweza kutafuta vitu kama hivyo ili vikaweza kutusaidia. Kwa mfano kama sasa hivi wenzetu wale watu wa hali ya hewa, wanakwambia kama leo wavuvi msende kuvua upepo uko hivi na hivi na hivi na sisi tukawa tuna-*depend* na wao tusichanganye mambo, nataka hapa nieleweke Mheshimiwa ikiwezekana na sheria kama inatupa tukiwa na vitu kama hivyo vya teknolojia la kuangalia janga gani litatukabili hapo mbele.

Kwa sababu mambo yana-*change*. Hivi juzi tulikuwa na upepo mkubwa sana mpaka vyombo vikazuiwa kwenda, nashukuru na wenye vyombo waliona hilo hawakufanya tamaa, wenye vyombo vyote wali-*stop* kwenda Pemba kwanza kutokana na hali halisi ya upepo mkali sana. Sasa pale wewe unatakiwa uwe na *attention*, pale mtu wa maafa aanze kujiandaa na awe *ready* na vile vyombo ambavyo kila mara wanatangaza, awe mkali katika vitu ambavyo vinataka kufanywa kwa kuvuka mipaka. Kwa sababu mtu mwenye tamaa atasema hapana, mimi nita-*try* nitaenda, kumbe anakwenda kutuulia wananchi. Sasa mimi hapo niombe sana Mheshimiwa kuwa hiki kitu kiweze kukubalika kwa wakati mzuri sana.

Mhe. Naibu Spika, ukiendeleza kunipa na mimi nitaweza kusaidia zaidi.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema kuwa muundo ambao ni *page* ya 306, hapa ndio kuna ule muundo wenyewe Kamati ya Kukabiliana na Maafa ya Wilaya itakuwa chini ya uenyekiti na Mkuu wa Wilaya, mimi sina tatizo nalo na ndio maana nikasema kuwa tuangalie wale watu wetu watakwenda katika *course* ya wilaya au ile ya kitaifa,

lakini watu kama wale ma-*big men* wale twende kwenye *course* ya kitaifa huwezi kumuweka katika wilaya, tuachieni sisi wabunge na wawakilishi tuwemo katika wilaya.

Lakini hapa Mheshimiwa sijamuona Diwani wangu na Diwani na yeye ana nafasi katika Wadi zake, lakini Mhe. Waziri tuangalie, silazimishi nataka nikwambie, lakini kuna vitu ambavyo tunavyoviona kwenye *table* tukija hapa ndio tunaviona zaidi. Sasa ukiiona hilo linaingiana basi ningeomba na wewe Mheshimiwa tutoe heshima hiyo na tuweke katika kada gani utaangalia wewe mwenyewe za chini kabisa huku, utajua vipi vya kuweza kuwaweka na kuweza kufanya shughuli kama hizo.

Mhe. Naibu Spika, kuna jambo ambalo muhimu sana nataka nilizungumze, ningeomba sana na hili suala Mhe. Makamu wa Pili naomba nikugeukie wewe. Unajua Zanzibar sasa hivi kusema la ukweli boti tunazo *Alhamdulillahi;* boti za *emergency* japo si za Serikali, lakini niseme za Serikali, tuna *speed boat* hapo KMKM wanazo, lakini hatuna *emergency helicopter* na tunakwenda katika mfumo huu sasa hivi kwa kujiandaa na kujikinga na hayo maafa yenyewe. Mheshimiwa tumia ujasiri wako Mheshimiwa Makamu wa Pili, hakuna haya katika kuomba kitu chenye manufaa, hakuna kuvunja sheria katika kuomba kitu chenye manufaa. Sheria imetuweka wazi, haya imetuweka tuondoe pembeni, nchi hii lazima Zanzibar tuwe na *helicopter* ya kuona lile jambo janga la ghafla likitokea Mheshimiwa tuangalieni, hata ukenda kukodi *helicopter* mpaka ikifika hapa tumeshawamaliza watu wamekufa na *more than* tumetumia fedha nyingi.

Mheshimiwa, naomba sana na kama Rais ananisikia wa Zanzibar ninamuomba sana hili alione kififkra zangu na litakuja kufanikisha na nikifa mtanitilia ubani, *helicopter* hii aliichangia Mhe. Mshimba, kwa maneno si kwa fedha maana fedha sina si mchezo, maana yake niseme ukweli ulivyo, yaani kwa fedha si masihara, sijui mishahara yangu mingapi niweze kuichanga ili niweze kupata *helicopter*.

Lakini hili jambo la msingi tumeshalisema sana wakati huo tangu mwenyewe Dr. Mwinyi tulilizungumza jamani kuna vitu ambavyo lazima nchi tuwe navyo vitu hivyo. Kuna *life jackets* zile kubwa mfumo wa kama boti ni vitu ambavyo ni muhimu, lakini jamani tulifanya harambee narudia tena lile suala ambalo kwa mujibu wa sheria Mhe. Naibu Spika, naomba radhi kwa hili na hii tufanyeni harambee, *helicopter* ni muhimu sana katika uokozi kwa wananchi wetu. Kwa sababu vinakwenda vyombo vile mbali sana masafa, unaambiwa tu lile janga lililopita *helicopter* ndio iliowaona wale watu, hatushawishiki hapo kwamba *helicopter* ndio iliyofanya chanzo cha kuwaona wale watu waliozama.

Sasa na hii mimi naomba sana kama zipo kwa wenzetu kule jirani zimekaa tu kwenye mabanda tukachukuweni tuilete hapa moja itusaidie katika mambo ya uokozi hali halisi ilivyotokezea.

Kwa sababu Mheshimiwa tunakata miti ovyo. Moja ya sababu za kusababisha upepo uweze kuingia kwa nguvu kwenye kisiwa. Mheshimiwa tunakata miti ovyo tunachimba fukwe ovyo, sheria inakuja hapa ya mazingira, lakini nayo ni moja katika chachu ya kusababisha matatizo ya maafa ya bahari kuipa nguvu kupanda juu hiyo ni moja. Kwa hivyo, naomba nalo katika makatazo moja ni hilo, tuki-*block* masuala hayo tukasema wananchi kata mti panda mti, sheria zikawepo za kusimamiwa basi maafa mengine yanaweza yakakingika.

Mhe.Naibu Spika, lakini mengine huwezi kukinga kwa sababu hakuna mjiti wa kujizuia kule. Sasa mimi naomba sana kwa kuwa kama nilivyokwambia mimi ni Mjumbe wa hii Kamati, kwa hivyo, naomba sana mimi niwe naenda kijumla jumla.

Mhe. Naibu Spika, niingie katika ukurasa huu wa 311, sasa uone kuwa yale mambo niliyokuwa nikiyasema sibuni, kuna kifungu cha 30 endapo Kamati zitakubaliana na maafa, hapa kidogo kuna kitu imeingia "maafaza" naomba kidogo turekebisha ni "maafa" za sheria au sijui zimechanganywa na sheria ya wilaya. Mheshimiwa zimejichanganya hizi sentensi zake, inasema; Maafa imezidi uwezo wao Mkuu wa Wilaya na kushauriana na Mkuu wa Mkoa wa Mkoa husika na kuthibitishwa na Kamisheni na atatangaza hali ya maafa kwa Shehia ya Wilaya husika.

Mheshimiwa, ndio yale nikasema kwamba anataka kutangaza huyu Kamishna wangu, Kamisheni inataka kutangaza, lakini ukienda kule kwenye vyombo vya habari pengine umeme unaambiwa hamna na anataka kutoa tahadhari ya ghafla, lakini pengine yeye angekuwa na chombo ambacho kitaweza kutangaza na kikaenea Zanzibar nzima na kiko

*full time,* kina mambo yake kimeji-*control* kila kitu hata kama umeme ukijizima wala hana longolongo la mambo chungunzima atakuwa na uwezo wa ku-*connect* na kwenda Zanzibar ikapata habari.

Mhe. Naibu Spika, ndio maana nikasema pale lazima na hii tuipe nguvu, kuwepo na chombo ambacho kitaweza *public* ya haraka sana. Hili ni lazima na huko wenzetu halikadhalika na ndio wanavyojiandaa hivyo. Kwa hivyo, maelezo ya Kamati bado narejea kwamba utukubalishe Kamati ziende nje zikajifunze.

Mhe. Naibu Spika, mimi nimesoma jana padogo sana, lakini je, angelinipeleka nje ningefahamu vipi? Si ningefahamu zaidi. Kwa sababu kule nje *theory* na *practical* yenyewe. Mimi jana nimesoma *theory* tu, sasa jiulize je mtu kama huyu ningempeleka akaona ile *pratical* yenyewe hasa jinsi gani watu namna wanafanya, kwa sababu juzi kuna watu, kwa mfano hata mimi ni mchezaji mpira nataka niingie katika *league* lazima nifanye mazoezi. Mazoezi yenyewe yawe *original* hasa au nakwenda kufanya mechi nyingine za nje ili kujitayarisha na kuingia *league* ya Zanzibar. Sasa na hili lazima tukaone mafunzo na hili wawakilishi sio mbaya kwa sababu mwakilishi yeye ni timu ya mwanajeshi, *any time* anaweza na yeye akasaidia kuweza kuokoa lile jambo kwa sababu taaluma anayo.

Mhe. Naibu Spika, kwa mfano leo mtu anaungua na moto nitakwenda kumuokoa vipi, nitatumia *techniques* gani, nitamshuti tu, nikimshuti kumbe nammaliza. Lakini kumbe ningetafuta guo lenye maji nikamkumbatia woo, si itakuwa tayari nimemuokoa. Sasa na hili jamani musione tabu kutoa fedha wasomesheni hawa ili wawe walimu wazuri na waweze kufanikisha na hili suala linakuwa gumu sana na ndio maana unakuta hata tutazame wenzetu wa Bunge, Bunge wengi wamepita katika mafunzo ya ustawi kama ya JKT na kadhalika, sisi hapa hatupitishwi…

**Mhe. Naibu Spika:** Mheshimiwa malizia.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Naibu Spika, ahsante namalizia dakika zangu tano, ukiona hivyo nina bashrafu ya mwisho.

Mhe. Naibu Spika, sasa haya ni mambo ambayo tunatakiwa lazima serikali iwe *active* kweli kutoa mafunzo kwa waheshimiwa, ni rahisi sisi kwa sababu ukiipeleka ile *message* kwa wananchi, wanaelewa, leo mimi ukinisomesha vizuri, nitamwambia tatizo hili lakuweka vijiti hapa nje kuota moto ni hatari, mimi itakuwa nimeshamwambia, lakini nitashindwa kumwambia kwa sababu naona wananchi wangu wanajiokoa katika ubaridi, kumbe ndio wanajimaliza.

Mhe. Naibu Spika, sasa mimi nafikiria tukipewa elimisho hilo na tukipelekwa katika nchi za wenzetu tukaangalia, basi Kamisheni hii ita-*play* vizuri sana asilimia mia moja ita-*play* na majanga madogo madogo tutaweza kuyaondoa.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana, nimshukuru Mhe. Makamu wa Pili na amenisikia na nina imani kwenye bajeti ataniambia uwezo wa kupatikana *helicopter* upo, naamini hilo atanipa lugha hiyo kwa Wazanzibari kuwa matumaini kuweza kupata *helicopter*. Nimshukuru sana Mhe. Waziri wangu mara nyingi sana huwa namwambia kuwa ananitafutia, amenitafutia visakina atashindwa kunipatia na yeye kuunga mkono hii *helicopter,* yaani visakina vizuri vya *benz* vimekuja hapa na niliomba hivi hivi kama masihara, nyinyi mnafikiri ninawafanyia masihara, lakini nasema kitu *reality,* kweli, haiwi Makamu wa Pili leo akachukue kisakina kinasukumwa, ni aibu nchi hii.

Kwa hiyo, mimi naunga mkono asilimia mia kwa mia. Ahsante sana.(*Makofi*)

**Mhe. Ali Salum Haji:** Mhe. Naibu Spika, na mimi nikushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia Mswada huu wa Kukabiliana na Maafa.

Mhe. Naibu Spika, kabla sijaanza chochote basi na mimi nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kuleta mswada huu. Kwa kweli dhamira ya serikali imeonesha namna gani imekusudia kuwasaidia wananchi wake pale ambapo panapojitokeza maafa na majanga katika nchi yetu. Ni kweli nchi yetu ni kisiwa na visiwa mara nyingi huwa kunakabiliwa na maafa ya aina mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, mswada huu una malengo mazuri na una nia njema, lakini nataka niseme tu kwamba kabla sijaanza kuingia ndani nimtanabahishe Mhe. Waziri namna ya kuweza kujipanga ili kutafuta namna ya kuweza kukabiliana na sheria hii itakapokuwa tayari, *otherwise,* tunaweza tukatunga sheria, lakini tukashindwa na

utekelezaji, kwa sababu malengo ni mazuri, lakini inawezekana uwezo ikawa hatuna wakuweza kukamilisha yale majukumu ambayo wametukabidhi.

Mhe. Naibu Spika, mjumbe aliyepita alijaribu kuzungumzia zaidi suala la *helicopter*. Ni kweli maafa makubwa ya nchi yetu yanayotukabili mara nyingi huwa ni kuzama kwa vyombo, sasa mimi sitaki kulizungumza hilo zaidi, siende zaidi ya *helicopter* tu hata kujipanga kuwa na boti za kisasa katika kukabiliana na maafa ni suala jema. Kwa sababu mara nyingi maafa yanapotokezea katika nchi yetu huwa wanategemea sana vyombo vya watu binafsi, Mwenyezi Mungu anatujaalia mara nyingi vyombo vinakuwa viko karibu na majanga yanayojitokeza, lakini Mwenyezi Mungu atuepushie mbali pale kutakapokuja kutokea tatizo na boti za wafanyabiashara zikawa ziko Dar es Salaam na maafa yametokezea karibu ya Zanzibar inahitaji kuharakisha kwenda kuwaokoa watu wakashindwa kufanya kazi kwa muda muafaka na hatimae wananchi wakaweza kupoteza maisha.

Sasa nasema kwamba sheria ni nzuri, lakini haja ya namna ya kujipanga katika kuja kuitekeleza ndio suala la msingi, vyenginevyo tutabakia kwamba tuna mambo mazuri, lakini utekelezaji utakuwa hakuna.

Mhe. Naibu Spika, kingine ambacho kinanipa mashaka katika utungaji wa kupitishwa mswada huu kuwa sheria, baada ya kuwa sheria kutokuja kutekelezeka ipasavyo ni namna mazingira ya nchi yetu sasa hivi katika masuala ya mipango ya miji yalivyoathirika. Tunaangalia zaidi maafa ya bahari tu, lakini kuna maafa ya moto mimi yananipa mashaka kwamba nchi yetu hii wakati wa ujenzi wake ulipoanza ulikuwa na mazingira mazuri sana, lakini njia zote za Manispaa ya Zanzibar zimekuwa hazipitiki kwa magari ya Zimamoto kuweza kukabiliana na hayo maafa wenyewe.

Sasa hili nalo pia ni athari ya kuweza kujipanga kuwa na mipango ya miji iliyokuwa mizuri, kwa sababu tunaweza kuwa tuna *fire* kijiji kinateketea, lakini *fire* halifiki kwenda kuzima huo moto wenyewe. Sasa nalo hili ningependa kutoa tahadhari kwa wizara wakaanza kuangalia namna ya kuanza kuutengeneza mji wetu katika mpango uliokuwa mzuri ili kuweza kufika katika maeneo ili majanga yatakapokuja kujitokeza kuweza kuyakabili na kuweza kuyatatua.

Mhe. Naibu Spika, jengine ambalo ninahisi kwamba itakuwa ni changamoto katika taasisi hii nalo pia napenda kutoa tahadhari kuliangalia kwa kina. Mji wetu wakati unapangwa katika awamu za kwanza na za pili waliweka maeneo maalum ya dharura ya kuweza kupata maji ili kutokwenda masafa ya mbali wakati tunazima ule moto ili lile janga lisiweze kuendelea na kuzima moto kwa haraka. Lakini maeneo yale sasa hivi imebakia kuwa historia, mengine miundombinu yake imeshaharibiwa, lakini nalo tatizo la maji pia linapelekea kuwa ni athari kubwa ya kuweza kukabiliana na majanga ya moto katika maeneo mbali mbali.

Niwashukuru sana na niwapongeze wenzetu wa Zimamoto wamejaribu kuwa na *reserve tank car* ya maji wanapokwenda katika majanga ya kuzima moto, kwamba nalo hili lilifanyika baada ya kuona hiyo athari ya kwamba maji katika maeneo mengi yamekuwa ni tatizo. Kwa hivyo, wanakuwa wanachukua *reserve,* yaani *fire* inapomaliza maji yake hiyo *reserve* inawekwa halafu inakuwa inakimbilia haraka kwenda sehemu husika.

Sasa mimi nasema kwamba kuna baadhi ya maeneo wakati sisi tunaendelea kupitisha hii sheria tukaanza kuiangalia kwa kina ili kwenda sambamba sheria, utendaji na utekelezaji wa rasilimali au baadhi ya vitu ambavyo vimo katika maeneo yetu, vyenginevyo ni kwamba kuna hatari ya kupitisha sheria nzuri, lakini utekelezaji wake ukawa unaathari ndani yake. Nasema hili kwa sababu tuna ushahidi wa kutosha na tuna mifano mingi ambayo tumeanzisha, tumeanzisha mambo mengi sana, lakini yanashindwa kutekelezeka kwa sababu ya hali yetu tuliyokuwa nayo, na sio kwamba serikali inakuwa haitaki, lakini nao uwezo wenyewe wa serikali kuweza kutatua hayo matatizo ndio inatupelekea kuwa katika hali hiyo.

Mhe. Naibu Spika, kuna mambo mazuri sana, mimi naweza kukutolea mfano mpaka kuna Bodi ya Mikopo, tumeanzisha Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, bodi inafanya kazi vizuri, ina ratibu uzuri, lakini uwezo wa serikali katika suala lake la kiuchumi linapelekea bodi kutokuweza ku-*manage* vizuri katika shughuli zake. Inafika wakati wanafunzi wanahitaji pesa, wanafunzi pesa hawatumiwi, serikali ina nia njema, lakini uwezo ndio huo. Sasa nasema kwamba tunakuwa tunajaribu kutanua wigo mkubwa wa kuweza kuanzisha taasisi mbali mbali katika kuwasaidia wananchi wetu kwa sababu serikali ina dhamira njema, lakini hali ya uwezo wa nchi bado hairuhusu.

Sasa nasema kwamba kuna haja ya kujipanga vizuri na mimi naamini hapa *professor* hapa alimsifu sana dokta juu Katibu Mkuu, anasema kwamba si kila jambo linahitaji fedha za ndani. Lakini kama tutakuwa na mipango mizuri tukakaa na wahisani katika mazingira mazuri, basi tunaweza tukatafuta njia nyengine mbadala ya kuweza kuisaidia nchi yetu kwa kupata ufadhili kupitia nchi mbali mbali ilimradi lile ambalo tumelianzisha liweze kutekelezeka kama serikali ilivyokusudia.

Mhe. Naibu Spika, baada ya dibaji hiyo ndogo, sasa naomba kwa heshima yako niingie kwenye mswada wenyewe moja kwa moja nichangie yale mawili matatu ambayo kwenye mswada mimi nimeyaona na ninaomba niende katika ukurasa wa 301 kuhusu kuanzishwa kwa Kamisheni.

Mhe. Naibu Spika, katika kifungu cha 4 kimeelezea Kamisheni itakuwa chini ya Uwenyekiti wa Makamu wa Pili wa Rais, sina tatizo na hilo.

La pili, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais atakuwa Makamu Mwenyekiti, sina tatizo na hilo.

Mhe. Naibu Spika, lakini niko katika kifungu cha 4(3) kinahusu Wajumbe wa Kamisheni wale waliolezewa hapa chini.

Mhe. Naibu Spika, tumeambiwa kwamba mawaziri wote wa serikali watakuwa ni wajumbe, sikatai, lakini mimi nahisi kwamba tungejaribu kuliangalia kwa kina kuweza kupunguza wajumbe ili kuweza kubana matumizi ya serikali, kwa sababu wajumbe hawa sifikirii kama watakuwa wanakaa vikao vyao, wakishakaa vikao wanaondoka, ni kwamba wanahitaji maposho. Sina tatizo kwamba labda ninawaonea choyo, lakini ni katika namna ya kuona kwamba tunabana matumizi ya serikali katika ile hali halisi, kwa sababu kuna maeneo mimi nakubaliana nayo kwamba baadhi ya mawaziri wakawa ni wajumbe, lakini sitegemei kwamba kuna baadhi ya mawaziri tukawalazimisha kuwa wajumbe.

Kwa sababu ukiangalia wizara zao hazionekani kama zitakuwa zina mantiki ya kiathari ya kimaafa maafa. Tuangalie wizara mbili; nimeangalia Wizara ya Utumishi wa Umma hii wizara sitegemei kwamba katika suala la kimaafa litakuwa linahitajika labda waziri wake aingie kuwa ni mjumbe katika eneo hili au Wizara ya Uwezeshaji. Sasa nasema kwamba hebu tungeangalia kwamba kuna haja au kuna ulazima kweli wa kwamba mawaziri wote au Baraza zima la Mawaziri kwamba wawe ni wajumbe wa hii Kamisheni.

Mhe. Naibu Spika, mimi nahisi kwamba kuna haja ya kuangalia kwa kina kuona tunabana vipi ili kuweza kupunguza matumizi ya hii kamisheni vyenginevyo itakuwa kile ambacho tunakitafuta kuweza kuwasaidia wananchi chote kinatumika katika kuwapa maposho Wajumbe wa Kamisheni katika masuala mazima ya vikao vyao.

Mhe. Naibu Spika, katika hiyo hiyo kamisheni nimejaribu kuangalia katika ukurasa wa 302 hapa kwenye kifungu (f) ametajwa Kamishna wa Polisi, halafu kuna (h), Mkuu wa Kikosi cha Kuzuia Magendo na (i) Kamishna wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi. Sasa mimi nakuwa najiuliza kama tuliweza kuamua mawaziri wote tukawaingiza katika Kamisheni, kwa nini tumeshindwa kuviingiza vikosi vyote navyo kuingia katika Kamisheni. Sasa kwenye vikosi ambao tunawategemea wao ndio nguvu kazi tosha, tumeanza kuwabagua baadhi ya vikosi tumeviacha, lakini kule kwengine kwenye Baraza la Mawaziri tu mbona wao tuwamalize wote waingie kwenye mazungumzo.

Mhe. Naibu Spika, mimi hapa ninakuwa ninapata mashaka, kwa hiyo, Mhe. Waziri aje anieleze sababu ya kuviacha kikosi cha KVZ na mafunzo wasishiriki katika Kamisheni kuhusu suala zima la kuja kukabiliana na maafa Mhe. Waziri, atakuja kutoa ufafanuzi atanisaidia hili. Vyenginevyo, kama huku kuna vikosi havina haja au havina umuhimu wa kuingia katika Kamisheni basi na mimi sioni umuhimu baadhi ya mawaziri kuingia katika Kamisheni hii ya maafa.

Mhe. Naibu Spika, kingine katika ukurasa wa 303 katika kifungu cha 6 (f) naomba ninukuu kidogo;

> "Kamisheni itakuwa na uwezo wa kumshtaki mtu yeyote ambaye amekataa kutoa au kupokea huduma wakati wa dharura wa maafa".

Mhe. Naibu Spika, hiki kifungu mimi kidogo kinanipa mashaka, kinanipa mashaka tunaweza tukaja tukamshitaki mtu tukamtia hatiani tukamfunga pasipo na sababu za msingi. Kwa nini niseme hivi Mhe. Naibu Spika? Kwa sababu

inawezekana unahitaji unaweza kumtaka mtu kusaidia kutoa huduma wakati wa maafa, lakini kumbe na yeye mwenyewe alikuwa ana tatizo la kukimbilia kuna jambo limemsibu anahitaji kulifanyia haraka kwa kulipatia ufumbuzi. Sasa lakini huku sheria inamlazimisha kwamba atakapokataa kutoa huduma basi mtu huyo anapaswa ashtakiwe. Sasa mimi ningeomba tuliangalie Mwanasheria yupo, liangalie namna ya kuki-*frame* hiki kifungu, vyenginevyo tutakuja kuwatia watu hatiani tuwashtaki kumbe unamtaka yeye atatue tatizo lako wewe wakati yeye mwenyewe ana tatizo lake naye analikimbilia kwenda kulitatua.

Sasa nafikiri tutafute namna ya kukiweka sawa hiki kifungu, vyenginevyo tusije tukawatia watu hatiani pasipokuwa na msingi. Tunajua utamaduni wa nchi yetu huu hauna matatizo yoyote na wengi tunaona na watu wengi wanafanya kwamba mtu inawezekana si lazima hata maajali yanatokezea mtu anagongwa na gari, gari linapita mtu anasimamishwa anasimama anamchukua mgonjwa anamfikisha hospitali au anamfikisha polisi kwenye kuchukua *PF3,* baadae anampeleka hospitali kwenda kupata huduma, lakini sio wote wanaosimama, inawezekana mtu umemsimamisha lakini na yeye ana dharura zake.

Kwa hiyo, isije ikafika pahala gari fulani tumeisimamisha halikusimama unaamua kumshitaki unachukua namba kisha unakuja kumshtaki dereva kwa sababu labda kulikuwa kuna jambo analiharakia.

Kwa hivyo, mimi nafikiri tutizame namna na hususan kuangalia mazingira yenyewe haya yalivyo, kwa sababu nasema kwa hivi sasa hivi sheria hii tukishaipitisha, tutategemea sana vyombo hivi binafsi vikatusaidie kutatua matatizo ya baharini. Sasa kama tutaviomba vile vyombo vitusaidie, lakini vile vyombo vyenyewe kama vitakuwa vina tatizo au kuna mambo mengine ambao watu wanaweza kukataa. Sasa mimi nafikiri kwamba tuangalie namna ya kuweza kufanya mawasiliano mazuri katika hiki kifungu.

Mhe. Naibu Spika, vyenginevyo tunaweza kuja kuwatia hatiani na mtu na chake pamoja na kwamba na sheria unamlazimisha mtu sheria kwa mali yake hii ni hatari, kwamba mali yako umlazimishe sheria mtu lazima ajitolee kuisaidia, kweli ni imani na kweli ndio Uislamu, lakini si vitu ambavyo vya msingi kutoka kwa mtu huyo.

Mhe. Naibu Spika, kingine ambacho nataka nikizungumzie ni kwamba narejea tena kama nilivyozungumza mwanzo kuondoshwa kwa vikosi vya KVZ na Mafunzo navyo katika ukurasa wa 305. Mimi bado nalia na taasisi hizi mbili na nielezwe sababu ya msingi ya kuondolewa watu hawa na kwa kweli sasa hivi tunaweza kuona utamaduni mzuri sana wa vikosi vya SMZ kuweza kushirikiana kufanya kazi zao kwa pamoja. Sasa hivi tunaona kazi zinakwenda vizuri, unamkuta KVZ, KMKM na Polisi wote wamo ndani, lakini katika baadhi ya taasisi tunawaweka pamoja, lakini katika baadhi ya mambo tunaanza kuwabagua hawa waende hawa wasiende.

Mhe. Naibu Spika, nao katika kuanzishwa Kamati wametajwa hapa, katajwa Afisa Mkuu wa Utawala wa Jeshi la Polisi kifungu cha 11(2) kutoka (d), (f) na (h), wametajwa maafisa;Afisa Mkuu wa Utawala wa Jeshi la Polisi Zanzibar, Afisa Mkuu wa Utawala wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi, Afisa Mkuu wa Utawala Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo, lakini hakuna Afisa wa KVZ wala Afisa wa Mafunzo. Hapa napo nataka nielezwe kwa nini maafisa hawa hawakuweza kushirikishwa katika taasisi hii ili na wao wakaweza kutoa michango yao katika kulisaidia Taifa lao pale ambapo maafa yamejitokeza.

Mhe. Naibu Spika, nalo hili linajirejea tena, lakini hapa nimeanza kupata kigugumizi. Kifungu cha 14 ukurasa wa 306, Kamati ya Kukabiliana na Maafa ya Wilaya itakuwa na wajumbe wafuatao. Sasa hapa katika kifungu cha 14(2)(h) Kamanda wa Zoni wa Kikozi cha Valantia Zanzibar amewekwa.

Mheshimiwa naanza kupata mashaka kwamba juu tumemkataa, lakini chini tunamuweka. Mimi Mhe. Waziri atapokuja ajaribu kunipa maelezo ya kutosha hivi huku chini ana nguvu gani ya kuweza kulisaidia Taifa lake hata asiwe na nguvu za kusaidia Taifa lake katika *level* ya kitaifa kule juu.

Mhe. Naibu Spika, mimi mchango wangu ulikuwa ni huo tu kwa haraka haraka. Lakini nirejee kusema tena kwamba, nampongeza Mhe. Waziri na kwa kweli hii sheria ni nzuri, tunakuwa tunapata majanga mengi sana na kwa kweli labda kabla ya kuanzishwa sheria hii tulikuwa tunauona ugumu wa wananchi wetu pale wanapopata matatizo, tulikuwa tukikimbilia katika taasisi za Mkuu wa Wilaya, Masheha wanaratibu shughuli zile panapotokezea majanga mbali mbali.

Kwa mfano upepo, Mkuu wa Wilaya anakua anajinasibu niorodheshee wananchi waliopata matatizo, sisi kwa kushirikiana na masheha tunaorodhesha wale wananchi kila ukishapeleka kwa Mkuu wa Wilaya alikuwa anakwambia bwana mimi nisharipoti kwa Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Mkoa naye anakwambia mimi nisharipoti Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, lakini ukienda juu unaambiwa suala hili haliko kisheriza zaidi na sasa hivi hakuna mfuko na uwezo.

Sasa kuletwa kwa sheria hii nahisi yale matatizo ya manung'uniko ya wananchi wetu yanaweza yakaondoka na pale ambapo yanaweza kujitokeza majanga basi wananchi wetu wanaweza kusaidiwa kwa namna moja au nyengine. Kwa sababu unaweza ukamsaidia mtu kumuokoa, lakini unaweza kumsaidia mtu katika majanga, unapokuja upepo na mabati yakaruka wananchi wetu ni wanyonge na wengi inafikia pahala inakuwa hawana makaazi yaliyokuwa mazuri. Nina imani kwamba tukiwa na sheria na mfuko basi tunaweza tukasaidia wananchi wale ili kuondosha zile athari walizozipata.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo kwa niaba yangu na kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Kwahani naunga mkono mswada huu. Ahsante.

**Mhe. Fatma Mbarouk Said:** Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia fursa hii kuchangia machache katika Mswada huu wa sheria ambao unasomeka kwamba; "Kuanzishwa Sheria ya Kupunguza na Kukabiliana na Maafa Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana nayo".

Mhe. Naibu Spika, huu mswada ni muhimu na niwaambie wenzangu kama kawaida ninapoanza kuchangia huwa naanza na kuwaomba Waheshimiwa kwamba mswada huu basi tuuchangie na baadae kuupitisha.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwanza niipongeze Kamati na naunga mkono maoni ya Kamati. Vile vile, kabla ya kuanza kuuchangia niwatakie wenzangu wote heri ya Mwaka Mpya na wale ambao wamepata maafa mbali mbali Mwenyezi Mungu awape subira.

Mhe. Naibu Spika, nikianza na Sehemu ya Kwanza ambayo ina masharti ya utangulizi, kuna namna ya kupunguza maafa maana yake. Lakini niseme kwamba kama visiwa na hasa visiwa vyetu hivi vya Zanzibar vina athari nyingi ambazo sasa hivi zinajitokeza na ni kuvamiwa na bahari. Niiulize tu serikali kwamba imejipanga vipi katika kukabiliana na hayo hasa athari hizi zinazotokana na kuzidi kwa hewa ukaa.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea nije ukurasa wa 305, Sehemu ya Tatu, Kuanzishwa Kamati ya Kitaalamu. Hapa imeandikwa kwamba Kamati hii ya Kukabiliana na Maafa, kuna Kamati ya Kitaalamu. Mimi ningependa hii *marginal note* ambayo iko huku imeandikwa Kamati ya Kitaalamu, kwanza niulize utaalamu uko mpana hata kufagia ni utaalamu, tukisema kwamba hii ni Kamati ya Kitaalamu basi ni utaalamu wa namna gani. Kwani mfano mtoto kabakwa huu ni mfano tu natoa, basi kuwe na wataalamu ambao watahitaji utaalamu wa kibaiolojia na kisaikolojia ni namna gani yule mtoto ameathirika.

Vile vile, nikienda na ukurasa mwengine hapa wa 308, kuhusu kuanzishwa kwa Kamati ya Kitaalamu ya Kukabiliana na Maafa ndio hiyo hiyo imejirudia rudia, kwamba kuna Kamati ya Kitaalamu ya Kukabiliana na Maafa. Kamati ya Kitaalamu ya Kukabiliana na Maafa ya Wilaya ni mambo hayo hayo ambayo nimeshayachangia kwamba hii ni Kamati gani na itazingatia utaalamu gani.

Kifungu cha 17 vile vile kimesema Muundo wa Kamati ya Kitaalamu ya Kukabiliana na Maafa ya Wilaya. Kamati hiyo ni hayo hayo ambayo nimeyauliza ni utaalamu wa kiasi gani.

Ukienda ukurasa wa 309 ambao unasema Muundo wa Kamati ya Kukabiliana na Maafa ya Shehia. Kamati hii kwenye kifungu cha (2) inasema kwamba; "Kamati ya Kukabiliana na Maafa ya Shehia itakuwa na Wajumbe wafuatao:

(a) Wajumbe wa Baraza la Ushauri la Shehia,
(b) Wawakilishi wawili wa Jumuiya ya kiraia ndani ya Shehia,
(c) Mwakilishi wa Watu wenye Ulemavu, na
(d) Wabunge, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Madiwani wa Majimbo na Wadi husika.

Kifungu cha (3), Katibu wa Shehia atakuwa ni Katibu wa Kamati ya Kukabiliana na Maafa ya Shehia".

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli hapa vile vile ningeomba kwamba jinsia izingatiwe. Kwa sababu hapa pameelezea kwamba kutakuwa na walemavu, lakini jinsia haikutajwa. Kwa hivyo, ningeomba pia jinsia ikazingatiwa.

Vile vile, kuna kifungu cha 21 kinasema; "Kamati ya Kukabiliana na Maafa ya Shehia itakuwa na kazi zifuatazo". Kule kote kumetiwa kwamba kutakuwa na Kamati ya Kitaalamu, lakini kwenye Shehia haikutiwa utaalamu na mimi hili ndio jambo ambalo nalipinga, kama sheria hii ilikuwa ya kitaalamu sasa kwanza izingatie hilo. Kwa hivyo, hapa naunga mkono sana kwamba iweko Kamati ya kukabiliana na maafa ya shehia kama inavyosomeka na kule kwengine kwamba ya kitaalamu ningeomba kama tumekubaliana itakuwa ya kitaalamu basi na huku iwe ya kitaalamu vile vile.

Mhe. Naibu Spika, nikienda Sehemu ya Nne, Mipango ya Kupunguza na Kukabiliana na Maafa. Kiswahili wakati mwengine kinakuwa na tungo tata, hizi tungo tata zinaweza kutufahamisha au wengine tukafahamu ndivyo sivyo. Nitoe mfano, siku moja nilikwenda kwenye semina na Mwenyekiti wa semina pale alitwambia namna ya Kishwahili kinavyokuwa kina utata ndani yake, lakini ningeomba kwanza niombe radhi kwa sababu nitachosema hapa pengine nitaonekana labda nimetaka kutukana. Basi sisemi maana Mhe. Hamza Hassan Juma, hapa ananikatisha tamaa ananambia nitatukana.

Kwa hivyo, sikusudii kutukana isipokuwa nilitaka kufahamisha namna gani Kiswahili kinavyoleta utata wakati mwengine.

Lakini hata hivyo, kwa sababu ni nafasi yangu ili kukijua namna gani Kiswahili kinaweza kikaleta utata, kulikuwa na hoteli sehemu imekabiliana na kinyozi. Sasa kwa sababu upepo siku zote ukisafirisha unakwenda *straight* unasafirisha zile nywele zikawa zinaingia kule kwa yule muuza hoteli, siku moja akaandika bango kusema kwamba; "sasa kuanzia leo tunanyoa chini". Sasa watu wote walijenga hofu pale. Kwa hivyo, ni lazima kuwe na Kiswahili ambacho kitatufahamisha labda kunyolea na kunyoa kile Kiswahili kwa kweli kiliwagonganisha watu.

Kwa hivyo, na hapa niseme kwamba tukisema kupunguza na kukabiliana na maafa ina maana sasa tunapunguza kule kukabiliana, maafa ni makubwa lakini tunapunguza kukabiliana na maafa. Kwa mfano hapa nasema kwamba maafa yameshatokea, lakini unapunguza kukabiliana nayo ndivyo ninavyofahamu mimi, ukisema mpango wa kupunguza na kukabiliana na maafa ina maana unapunguza yale maafa yametokea lakini bado unapunguza kukabiliana nayo.

Mhe. Naibu Spika, najua hapa kuna mambo mawili ambayo huku chini kuna kupunguza kukabiliana na kwa sababu vifungu viko mbali mbali basi lazima tungesema mpango wa kukabiliana na maafa au mpango wa kupunguza maafa kwenye hii *heading* ambayo imewekwa hapa.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea nije kwenye ukurasa wa 312 ambao kwenye *marginal note* unasema huku; "Upatikanaji wa Rasilimali wakati wa Maafa", ambapo kifungu cha 34 kinasema; "Endapo ikionekana na Kamisheni na Kamati ya Kukabiliana na Maafa ya Wilaya kwamba:

(a) Rasilimali inayomilikiwa na mtu yeyote ikihitajika kwa ajili ya kazi za kukabiliana na maafa.

Wakati huo huo kuna sehemu ambayo inasema kwamba hii Kamati itakuwa inakodi sehemu. Lakini mimi ningesema kwamba kusiwe na sababu ya kukodi kwamba jambo likitokea basi rasilimali yoyote, kwa sababu haya maafa yanapotokea yanaathiri watu wote. Kwa hivyo, kama wewe ni Mzanzibari na una eneo labda linaweza likasaidia basi kusiwe na sababu ya kukodi eneo lile, isipokuwa ujitolee kwa mujibu wa uwezo wako na ile sehemu ambayo itachukuliwa na hizi Kamati za Maafa.

Sehemu ya Sita, Masharti ya Fedha. Kifungu cha 36(1) kinasema kwamba; "Kutakuwa na Akaunti Maalum ambayo itaingiza fedha zote za Kamisheni kama zilizoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi".

Kifungu cha (2) kinasema; "Kamisheni inaweza katika kutekeleza kazi zake na kwa mujibu wa masharti ya fedha hizo zilizopatikanwa, kutumia fedha hizo kwa malipo, posho, mishahara, gharama za kazi na malipo yoyote muafaka yanayojitokeza ikijumuisha matumizi muhimu".

Vyanzo vya Fedha, kifungu cha 37(1); kinasema kwamba; "Matumizi ya fedha yatafanywa na Mkurugenzi Mtendaji kwa idhini ya Kamisheni".

Mimi nikisema vyanzo vya fedha ni vile vyanzo ambavyo vitaingiza fedha, lakini ukiingiza matumizi kwamba yatafanywa na Mkurugenzi, yeye huyu ni *Accounting Officer,* labda ambaye yeye atasimamia. Lakini ilikuwa haipendezi hapa kuwa na yeye katiwa kwenye vyanzo vya fedha. Hii nakubaliana na kifungu cha 2(a) kiasi cha fedha kama itakavyoainishwa na Baraza la Wawakilishi kwa njia ya ruzuku. Nakubaliana nayo kwamba fedha hizi ambazo sisi tutazipitisha hapa ambapo Mkurugenzi Mtendaji atakuwa ni *Accounting Officer*.

Halafu kifungu cha 2(c) inasema kwamba; "Fedha nyengine zinazoweza kupatikana ama kutokana na utekelezaji wa majukumu yake au vyenginevyo".

Mhe. Naibu Spika, hii mimi naiunga mkono.

Mhe. Naibu Spika, ukurasa wa 314 kifungu cha 40 kinasema; "Mfuko wa Kukabiliana na Maafa". Tumesema hapa kwa mujibu wa sheria ya fedha ya umma kutakuwa na Mfuko wa Kukabiliana na Maafa Zanzibar ambao utajumuisha fedha zote zilizoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi katika makadirio ya bajeti ya mwaka.

(b) Misaada iliyoidhinishwa na serikali, na

(c) Michango ya wananchi.

Mhe. Naibu Spika, hii michango ya wananchi kwa kweli sifikirii kama wananchi watakuwa na uwezo huu au angalau labda watakuwa na uwezo, lakini hapa kidogo akija Mhe. Waziri anifafanulie kuhusu mchango huu.

Fedha nyengine zozote zinazotokana na adhabu zilizoainishwa chini ya sheria hii, fedha nyengine zozote ambazo zimewekwa au zimepatikana ama kutokana na utekelezaji wa kazi au vyenginevyo.

Malengo ya Mfuko, kifungu 41, Mfuko utatumika kwa malengo yafuatayo:

(a) Kutoa huduma za maafa;

Mhe. Naibu Spika, lakini kuna kifungu (c) kinasema kwamba; "Misaada ya kibinadamu wakati wa dharura au maafa ya ngazi ya Kitaifa, Wilaya na Shehia".

Nikisema kwamba misaada ya kibinadamu, maafa siku zote yanawakuta wanadamu, kwa hivyo, ukitia moja kwa moja ni kuongeza tu ule upana na urefu wa sentensi ambayo hata ukitoa hiyo misaada ya kibinadamu basi pia haitobadilisha maaana. Kifungu kiwe wakati wa dharura au maafa ya ngazi ya kitaifa, Wilaya na Shehia, haina haja hata kutia ya kibinaadamu, kwa sababu tunajua kwamba misaada inayotoka yote ni kwa ajili ya wanaadamu haitobadilisha maana.

Na hapa ndiyo ile niliyosema kule kukodi ardhi, vifaa, ununuzi wa vifaa na nyenzo nyengine na kuanzisha majengo ya dharura wakati wa maafa. Hii kukodi ardhi, ardhi yote ni mali ya umma na unapoitaka serikali kutumia ardhi basi inaweza lakini isiwe na bajeti kubwa ambayo itakuwa inatugharimu sana kwenye hizi Kamati zetu.

Kwa hivyo, hii kusema kwamba kukodi ardhi mimi siiwafiki kwa niaba ya wananchi wangu kwamba sipendelei kwamba iweko kukodi ardhi wakati tumeshasema kwamba kwa mujibu wa sheria ya ardhi, ardhi yote ni mali ya umma.

Makosa na adhabu katika Sehemu ya Saba;

(a) Makosa kifungu cha 42(1); Mtu ambaye amekataa kutekeleza majukumu yake bila ya sababu za msingi,

(b) Amefanya kitendo chochote kisichoruhusiwa, au

(c) Amekataa kusalimisha mali zake au kutoa huduma wakati wa maafa.

Ndiyo hii nafikiri nilipotoa mchango wangu huku kwamba ardhi ni mali ya umma. Kwa hivyo, nasema kwamba ametenda kosa akitiwa hatiani atalipa faini isiyopungua shilingi za kitanzania milioni moja na isiyozidi shilingi za kitanzania milioni mbili au kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita na kisichozidi mwaka mmoja au adhabu zote.

Mhe. Naibu Spika, inategemea na ile athari ambayo imetokea au yale maafa, ikiwa mtu yule ambaye amefanya kosa lile na sasa kutathmini kwamba adhabu hii ya miezi sita na kulipa Tanzania shilingi milioni moja. Sasa kama athari ilikuwa ni kubwa ya maafa ambayo yeye kafanya kapewa ni adhamu. Kwanza itathiminiwe ile athari ambayo yeye ameisababisha kwamba pengine ni mamilioni ya pesa ambayo yeye labda yalikuwa asaidiwe, lakini ukasema milioni moja unampa ni adhabu.

Mhe. Naibu Spika, mimi naona itakuwa haitatusaidia, ni sawa sawa na kifungu cha pili vile vile ya sehemu hiyo ya saba ambayo inasema; "Mtu ambaye atamzuia mtu aliyeidhinishwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria hii atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atalipa faini isiyopungua shilingi za kitanzania. Lakini tano ambayo vile vile mimi nasema si kipimo cha adhabu hiyo, yaani adhabu kwanza ipimwe kwa lile jambo ambalo limetokea pale na ile athari iliyotokea pale ni kiasi gani.

Makosa yanayohusu kukataa kutoa taarifa mtu ambaye amekataa kutoa taarifa yoyote inayohitajika na Kamisheni inayohusiana na maafa ametenda kosa na akitiwa hatiani atalipa faini isiyopungua shilingi za Kitanzania laki mbili au kifungo kisichopungua mwezi mmoja na kisichozidi miezi mitatu au adhabu zote mbili.

Mhe. Naibu Spika, na hiyo vile vile nasema bado hatujatathmini ile athari au labda Mhe. Waziri atakapokuja atanifahamisha vizuri namna walivyotathmini hizo athari ambazo zimetokea na vile vile athari za uongo pia, tunajua uongo ni dhambi na unaposema uongo basi unatakiwa vile vile uwajibike kutokana na uongo uliosema, unaweza kusababisha hata kuuliwa kwa mtu kwa sababu ya uongo wako. Tuondokane na tabia hizi za uongo uongo.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, tusitizame upande mmoja wa shilingi ila tutizame na upande mwengine. Mtu anayesababisha labda kuokoa maafa basi na yeye vile vile labda atazamiwe na yeye kupewa tunzo tusitizame upane mmoja kama akaokoa basi na yeye vile vile atunzwe kwa yale ambayo ameokoa pale.

Kanuni kama kawada, ni lazima kuwe na Kanuni. Lakini vile vile, sijui ukurasa gani ule nimeupita fani yangu hasa ya Uhasibu ile, niunge mkono sana kwamba fedha zile lazima zikaguliwe na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za serikali na vile vile baada ya kufunga mahesabu, lazima Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za serikali apelekewe mahesabu yale yaliyofungwa kwa kuirahisishia serikali kujua ni namna gani ya uwezo wake kimadeni na kimapato vile vile ili kujua serikali kwamba ina mali zake kwa kiasi gani, itakapopeleka mapema maana yake tumekuwa mara nyingi Taasisi hizi za Serikali zinapeleka Mahesabu yao wakiambiwa tarehe 30 Septemba basi anangojea mpaka tarehe 29 wakati hapa kuna muda mrefu kuanzia Juni tunapofunga hesabu, Julai mpaka tarehe 30 Septemba ile ni *deadline*.

Lakini mara nyingi ukienda maofisi mengi tatizo tunalikuta kwamba anapeleka saa nyengine tarehe 30 yenyewe na akesha huku ana sikitika kwamba mimi nilipeleka tarehe 30, umechelewa ka sababu ile ni *deadline* tu. Wewe hapa kuanzia Julai hadi Ogasti, kwa hivyo, hapa napigia msumari hasa kwamba zile taasisi zinazochelewa kufunga mahesabu yake kwa wakati kwa kweli tukipita kule na Kamati yetu ya *PAC* tunazikuta. Ingawaje Mashika na wao wanafanya kalenda ya Januari - Disemba, lakini ni hizi wizara zetu zinatumia kalenda ile yetu sisi ya serikali kuanzia Julai-Juni siku zote.

Baada ya hayo kwa naiba ya wananchi wangu wa Amani walionichagua kwa kura nyingi naunga mkono iwapo na waziri atakuja kunijibu mawili, matatu ambayo atanisaidia naunga mkono mia kwa mia. (*Makofi*)

**Mhe. Mohammed Haji Khalid:** Ahsnate sana Mhe. Naibu Spika, na mimi mchana huu kupata nafasi kutoa yangu machache kuhusu Mswada huu ulio mbele yetu unahusu mambo yanayokubaliana na maafa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, maafa ni jambo kubwa na kama walivyosema wasemaji waliotangulia kuwa sisi ni kisiwa tumezungukwa na bahari, kwa hivyo, maafa yetu yanaweza yakatokea baharini katika vyombo vya usafiri pengine

yanasababishwa na mambo ya kimaumbile kama upepo na mengineyo pengine upepo mkali nyumba na miti ikaanguka na hatimae kuharibu mali na miundo mbinu mbali mbali. Kwa hiyo, maafa ni jambo linalotokea bila ya kutarajiwa.

Kwa hiyo, serikali kufika pahala ikaona kuna umuhimu wa kuunda chombo ambacho kitajaribu kukabiliana na maafa ni jambo zuri na ni jambo la busara na inafaa kupongezwa kwa jambo hilo zuri.

Mhe. Naibu Spika, mimi mchango wangu hautakuwa mkubwa sana kuhusu suala hili. Lakini ningeomba nianze na muundo wa hii Kamisheni. Kwa muono wangu mimi Kikamisheni ni kubwa mno na Kamisheni hii imezungumzwa kuwa ni wakala wa serikali. Lakini kwa mawazo yangu mimi hii Kamisheni ndiyo serikali kwa sababu ni watu wawili tu wa Serikali Kuu ambao hawamo Kamisheni, ni Rais mwenyewe na Makamu wa Kwanza wa Rais basi, wengine wote ni Kamisheni.

Kwa hivyo, Kamisheni hii ni wakala wa nani na ndiyo serikali yenyewe. Kwa hivyo, kwa ukubwa huo ningeomba hii Kamisheni upunguzwe ukubwa wake kwa sababu mawaziri wote ni wanasiasa. Kwa hivyo, hichi kimefanywa kama ni chombo cha siasa kwa sababu mawaziri wote ni wanasiasa, yaani mawaziri mpungue ili nyinyi hii Kamisheni ilete taarifa kwenu. Lakini nyie ndiyo Kamisheni na nyie ndiyo Serikali mnafanya vipi?

Mhe. Naibu Spika, nimependekeza mimi kwa muono wangu Kamisheni hii Wajumbe wake wapungue tena sana. Pendekezo langu ni kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais angeliwekwa Mwenyekiti, Mhe. Waziri wa Nchi katika Ofisi yake aendelee kuwa Makamu, Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikao na Vikosi Maalum vya SMZ awe ni mjumbe Waziri wa Ardhi, Maji, Makaazi na Nishati awe ni Mjumbe, Waziri anayehusiana na mambo ya Mazingira awe ni Mjumbe, Waziri wa Afya awe ni Mjumbe, Waziri wa Miundo Mbinu Mawasiliano awe ni Mjumbe, Mwanasheria Mkuu awe ni Mjumbe na Vikosi vyote vya SMZ na Jeshi na Polisi kwa Zanzibar wawe ni Wajumbe kwa sababu hawa kwa sifa fulani ni fani zao hizi za kupambana na majanga na maafa. Lakini mawaziri wengine wote watolewe. Hao niliowataja nimewataja kwa sababu zao wanahusiana na mambo ya aina hii.

Kwa hiyo, Mhe. Naibu Spika, hilo pendekezo langu la kupunguza ukubwa wa Kamisheni. Wakuu wa Mikoa na wengine wote kwa kweli ili Kamisheni iweze kufanya kazi yake vizuri ni kuwa na Wajumbe wachache ambao watafanyakazi kwa ufanisi. Lakini Wajumbe hawa waliopendekezwa ni karibu thalathini au zaidi wakikutana ni kama semina, baada ya kuwa ni kikao cha kawaida huwa ni kama wamekuja kufanya semina. Kwa hivyo, pendekezo langu liko hivyo.

Halafu Mhe. Naibu Spika, pametajwa hapa Sekretarieti, lakini katika muundo haipo, imetajwa tu kuwa itakuwepo, lakini haipo, sijaiona, lakini kama iko pahala ningeomba nielekezwe iko wapi, ambayo imetajwa kuwa itaongozwa na Mkurugenzi Mtendaji, lakini naona anaongoza kitu ambacho hakipo au sijakiona.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, mimi nije katika hizi kazi za Kamisheni ziko nyingi, lakini nitachukuwa chache tu; Moja kuwawezesha upatikanaji wa fedha na rasilimali nyengine wakati wa dharura au maafa. Hili ni jambo muhimu kwa sababu maafa siku zote ni jambo ambalo limeathiri maisha ya watu na mali zao. Kwa hivyo, ili kuweza kuwasaidia au kurudisha miundo mbinu iliyoharibika katika maafa hayo lazima fedha zipatikane.

Kwa hivyo, Kamisheni lazima ipange mipango mizuri ya kutafuta fedha kwa kutumika kwa ajili iliyokusudiwa na isije kuwa ni kama kitega uchumi cha Kamisheni kwa ajili ya Kamisheni yenyewe. Lakini zitumike pale ambapo maafa au majanga yametokea ili ziweze kusaidia kuondoa tatizo lililotokea, tusingojee kuwa mpaka patoke maafa ndio tuanze kutafuta mtu mmoja mmoja asaiadie hiki au kile lazima Kamisheni iwe na mfuko wake wa kuweza kujitegemea kuendesha shughuli zake.

Mhe. Naibu Spika, jengine kuwa na jukumu la kusimamia na kuratibu kazi za kukabiliana na maafa. Hii lazima wananchi wapewe taaluma wapewe elimu waelekezwe namna gani yanapotokea maafa waweze kujikinga na hayo maafa. Kwa hivyo, nayo *point* hii ni ya msingi.

Jengine ni kupendekeza kwa serikali juu ya utaratibu wa upatikanaji wa fedha kwa ajili kukabiliana na maafa. Hii ndiyo nime-*comment* wakapendekeze kwa serikali ipi na hii Kamisheni yenyewe ndiyo Serikali. Kwa hivyo, labda waende kwa Rais tu, lakini angelikuwa hayumo na Makamu wake wa kwanza, lakini Kamisheni nzima ndiyo serikali yenyewe.

Mhe. Naibu Spika, jengine kuhakikisha kuwepo kwa uwajibikaji kwa taasisi muhimu katika utekelezaji wa sheria hii. Hili uwajibikaji katika kusimamia sheria ndiyo jambo ambalo linatushinda, sheria nyingi na nyengine ni nzuri, lakini ikishapita hapa ndiyo imeshapita kila pahala haitekelezwi, hasimamiwi, haitafutwi na haizingatiwi. Kwa hivyo, tumepitisha sheria nyingi sana nzuri lakini kufatilia kwake na utekelezaji wake hauonekani.

Kwa hivyo, hili ni jambo la msingi, kama ni kweli tumekusudia kupambana na maafa uwajibikaji lazima uwe wa kweli uwepo, vyenginevyo tutakuwa tunatia maji pakachani, pakacha haikai maji ukiinyanyua yote yatatoka karafuu na muhogo unakaa ndani ya pakacha lakini sio maji, kwa hivyo, ningeomba tusitie maji pakachani.

Mhe. Naibu Spika, jengine ninalotaka kusema ni dogo tu, Kamisheni itakuwa na uwezo, ule uwezo wa Kamisheni umeanza kifungu cha 6(a) hadi (g). Mimi nitazungumza kidogo kifungu cha 6(a) na (g) tu. Kama alivyozungumza Mhe. Ali Salum, ni kumshitaki mtu yoyote ambaye amekataa kutoa au kupokea huduma wakati wa dharura au maafa.

Mimi Mhe. Naibu Spika, hii kidogo ni ngumu kwa sababu Kamisheni ina watu wa nguvu, ukiachana na wa sasa wengi waliomo ambao ninataka wapungue mimi, lakini sitaki wapungue ndiyo watu wa nguvu, anaweza kupita mtu pengine na gari yake akamwita "wewe fulani! lete gari, peleka mgonjwa pahala", yule mtu akasema gari yangu haina mafuta, ikaonekana kuwa kakataa kutoa huduma au nina safari nyengine muhimu itaonekana kuwa kakataa kutoa huduma.

Kwa hivyo, hii kumshitaki mtu lazima ichunguzwe na izingatiwe kwa nini linalotaka hakufanya, siyo ionekana kuwa kakataa tu. Hivyo, lazima atazamwe kwa nini kaambiwa afanye kitu fulani au toa huduma fulani hakufanya, sababu yake ni ipi kabla ya kumchukulia hatua ya kumshitaki.

Mhe. Naibu Spika, kifungu cha (g) kinasema; "Kwa kushirikiana na taasisi zinazohusika kufanya ukaguzi kwa mtu yeyote, jengo, eneo au chombo kwa lengo la kukinga, kupunguza na kukabiliana na maafa na hali za dharura. Hii kadhalika ni nzuri. Mimi ningeomba sheria hii ikishapita kuhusu kukagua mambo haya wakaanze kule Pemba na jengo la Wizara ya Fedha. Jengo lile linahatarisha linaweza likasababisha maafa na hata vifo, kwa sababu ni bovu na lipo pahala ambapo kuna matumizi ya watu. Kwa hivyo, katika kifungu hiki sheria hii ikipita, Kamisheni ianze kukagua eneo lile kuona namna gani itaweza kunusuru hali mbaya iliyokuwepo pale.

Mhe. Naibu Spika, mimi nimalizie kwa hizi Kamati za Maafa za Shehia ambako ndipo chini kwenye watu wengi na wengi wetu tulioko huko ni watu wa kawaida, baadhi ya mambo hatuyajui. Kwa hivyo, Kamisheni iandae mpango maalum wa kitaalamu iende chini kwa shehia zetu mbali mbali kuwapa watu elimu, kuwaelekeza vipi wataweza kujikinga, kujilinda, kujihifadhi na maafa pale ambapo hali hiyo ya maafa ikitokea. Kwa sababu Kamati zitaundwa, lakini zikiachwa kimya bila ya kuelekezwa kwamba likitokea hili, hatua ya kufanya ni hivi na likiwepo jambo fulani, la kufanya ni hivi.

Kwa hivyo, hawa katika ngazi ya Shehia, Sheha na Kamati yake na watu wengine wanaohusika lazima wapewe taaluma ya kutosha ya kuweza kuwafahamisha watu wanaowaongoza namna ya kujikinga na majanga haya. Kwa sababu huko vijijini na mashamba maafa mengi yanatokea. Mara nyengine hata kulima chumvi ikavamia kipando chako ni maafa ijapokuwa ni madogo, jua linapokuwa kali, mazao ya chakula yakakauka bila ya kufika wakati wake uliokusudiwa ni maafa. Hivyo, waelimishwe ni vipi baada ya hali hii kutokea hatua gani wataweza kuchukua.

Mhe. Naibu Spika, mimi katika mswada huu mchango wangu ni huu mfupi, pale ambapo Mhe. Waziri atanielekeza na kuiona ile mambo ambayo mimi sikuiona nitamuunga mkono.

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante sana Mheshimiwa. Sasa nafasi tunampa Mhe. Abdulla Juma Abdulla, atafuatie na Mhe. Abdalla Mohammed Ali na kama muda utabakia tutamalizia Mhe. Mgeni Hassan Juma.

**Mhe. Abdulla Juma Abdulla:** Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi nisiwe mwizi wa fadhila nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kutoa mawazo yangu. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Chonga kuhusiana na jambo muhimu sana la maafa, mbele yetu tuna agenda muhimu sana kwa sababu jamii yetu ya Wazanzibari tumeshuhudia majanga na maafa ya kila aina na yamewaathiri sana wananchi wa Zanzibar. Kwa hivyo, ni vyema

kila mtu akajitahidi kutoa mawazo yake ili hatimaye tukapata sheria itakayotusaidia vya kutosha ya kupunguza maafa na kukabiliana nayo pale yanapotokea.

Mhe. Naibu Spika, kwanza mimi nataka niipongeze Serikali baada ya kuzungumzia muda mrefu bila ya kuwa na sheria namna hii na kwa kuwa athari zake zimekuwa zikionekana mara kwa mara, sasa imefikiria kuleta sheria ambayo ikikaa vizuri itatuongoza katika kupunguza makali ya majanga haya ambayo yanatokea.

Kwa hivyo, kwanza naipongeza Serikali kwa jambo hilo, lakini jambo hili la kukabiliana na maafa ni jambo la kimkakati na ni jambo la kitaalamu. Sasa nilikuwa ninadhani kwa sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambao ndiyo tunatunga hii sheria, Serikali ingefanya busara sana kama ingetupatia nafasi kwanza ya kutupatia taaluma angalau tujua A, B, C ya namna ya kujilinda na maafa au kujikinga na maafa au kukabiliana na maafa yanapotokea na pengine taaluma hiyo ingeweza kupatikana hapa nchini kupitia semina na mafunzo mbali mbali au hata isingekuwa vibaya kama Serikali ingeandaa ziara maalum ya kuwatembelea wenzetu walio na mazingira kama ya kwetu ili tukapata uzoefu wao wanafanya nini wakati wa kukabiliana na maafa.

Mhe. Naibu Spika, lakini leo inasikitisha tunatunga sheria hii tukiwa hatujui chochote cha kufanya kuhusu maafa. Mimi nafikiri hili ni tatizo lazima Serikali ikubali kama hapa kidogo imefanya tatizo.

Mhe. Naibu Spika, halafu jambo jengine ni kwamba maafa yanatokea miongoni mwa wananchi wetu. Maana maafa hayatokei huku juu Serikalini, yanatokea kule kwenye *grassroot,* yaani kwenye wananchi wenyewe vijijini. Sasa ni muhimu sana katika mikakati ya kukabiliana na maafa, Serikali ikatokea kipaumbele maalum cha kuwafundisha watu kule chini kwenye *grassroot*, kukitokea maafa wawe na *formula* angalau ya kuweza kukabiliana nayo kabla ya hii Kamisheni tunayoiunda hapa haijakaa.

Mhe. Naibu Spika, maana yake hii hata ikikaa pengine ni masaa au siku nzima imeshapita jambo ambalo kwa maafa mengine yatakuwa yakiathiri sana. Kwa mfano kama majanga ya moto. Majanga ya moto yakitokea kijijini siku nyengine huko hata hiyo gari ya *fire* ikifika huko, basi imeshakuwa hatari. Lakini kama wale watu wenyewe wamepewa taaluma mbili, tatu wanaweza kujihami kwa njia ya gharura. Sasa nilikuwa naona ni jambo jema sana kama Serikali itaweka *concentration* maalum ya kuwafundisha watu kule chini kwenye Shehia ili na wao kabla ya Serikali kutia nguvu zake, basi wao wenye wao wawe wanajua namna ya kukabiliana na maafa yale ambayo wanaweza kukabiliana nayo.

Mhe. Naibu Spika, nakumbuka wakati wa miaka thamanini tulipokuwa nchi yetu ipo kwenye vita tunapigana na Mzee Iddi Amini, kulikuwa na mafunzo maalum wanajeshi wakipita maskulini wakitwambia, kwamba bwana unachimba shimo, sijui unachimba hivi na unafanya hivi, ili likitokea balaa lile la mabomu ya Mzee Iddi Amini tuweze kujihami kabla jeshi halijaja kule mitaani. Sasa nafikiri na hili ni mfano wa hilo hilo, wananchi wangeelimishwa vya kutosha.

Hivi karibuni ulitokea moto Micheweni, hata Serikali iliposimka na kwenda kule kwa kweli nyumba nyingi zimeshateketea. Lakini kama wananchi wa Micheweni wenyewe wangekuwa wamepewa mafunzo fulani, basi pengine yale maafa yasingefika kiwango kile, wangeweza kukabiliana wao wenyewe. Sasa hili naomba Serikali sana ilifanye kuwa ni jambo muhimu sana katika kukabiliana na maafa.

Mhe. Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, sasa naomba niingie kwenye Mswada moja kwa moja. Ninataka nianze na kifungu cha pili ambacho kinazungumzia habari ya tafsiri ya maneno haya. Hapa naomba niende moja kwa moja kwenye tafsiri ya neno maafa yanayosababishwa na binadamu. Ukikisoma kile kifungu ni kikubwa sina haja ya kukinukuu chote, lakini ndani yake kuna neno mafuriko. Mafuriko hayasababishwi na binadamu. Kwa hivyo, naomba katika tafsiri ya neno maafa yanayosababishwa na binadamu neno mafuriko pale litolewe, kwa sababu mafuriko ile ni amri na kudra ya Mwenyezi Mungu wala si binadamu anayesababisha.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo sasa niende kifungu cha tano kinazungumzia, "Kazi za Kamisheni". Ukisoma kifungu cha 5 (b) kinasema;

> "Kuweza upatikanaji wa fedha na rasilimali nyengine wakati wa dharura au maafa".

Sasa Mhe. Naibu Spika, wakati mwingi tulipokuwa tukichangia humu katika Baraza moja katika suala ambalo Waheshimiwa Wajumbe waliligusa sana lilikuwa ni suala la kuwepo fedha za kutosha kwa ajili ya kukabiliana na

maafa. Lakini kifungu hiki kinaashia kwamba kama nitakuwa nimekifahamu vizuri, kinaashiria kwamba maafa yatokee halafu ndiyo Kamisheni itafute uwezekano wa kupata pesa. Ninafikiri kwa utaratibu huu haututoweza kukabiliana na maafa.

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa ninadhani Kamisheni iandae utaratibu na kwa sababu Kamisheni hii ni Serikali nzima yote ipo humu, ukimuacha Rais pekee, lakini Serikali nzima ipo hapa. Sasa ni vyema wakaandaa utaratibu wa kuwa na *funds* maalum, tena ikawa ipo *stand by* ya kutosha kabisa, ikitokea maafa tuweze kuitumia kwa ajili ya kukabiliana na maafa, lakini tukisema tukaanze kutafuta pesa sasa, kwa kweli watu wetu watapotea, watapoteza mali zao na pesa kwa zilivyo ngumu katika nchi hii hazitopatikana.

Hivyo, naomba labda *otherwise,* kuna mfuko unaanzishwa sijui sijasoma vizuri kwenye huu Mswada, lakini kama hakuna kitu kama hicho basi naomba Serikali izingatie hilo.

Mhe. Naibu Spika, halafu kifungu cha 6 kuhusu "Uwezo wa Kamisheni". Ukisoma pale (f) kinasema;

> "Kamisheni itakuwa na uwezo wa kumshitaki mtu yeyote ambaye amekataa kutoa au kupokea huduma wakati wa dharura au maafa".

Sasa hili nilikuwa na mushkeli nalo kidogo kwamba Kamisheni iweze kumshitaki mtu yeyote ambaye atakataa kutoa huduma wakati ni wajibu wake kutoa huduma.

Lakini isimshitaki mtu aliyekuwa anayekataa kupokea huduma, maana yake kupokea huduma hii ni hiyari ya mtu mwenyewe. Sasa ukimlazimisha mtu anayekataa kupokea huduma naye umshitaki, kwa kweli kimantiki inakuwa haileti sura nzuri, pengine mtu kapata maafa nyumba yake imeungua maslani lakini kwa sababu anazozijua mwenyewe na kwa sababu ya uwezo alionao haihitaji kupokea huduma ya kusaidiwa kujenga, anaweza kujenga mwenyewe. Kwa sababu ukisema ukamshitaki kwa sababu kakataa tu kupokea huduma ile ya msaada, mimi nadhani itakuwa hukumpa uhuru wa kutosha. Kwa hivyo, naomba hili neno kupokea huduma afadhali litolewe katika huu Mswada.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende kwenye kifungu cha 10 ambapo pale kuna Sekretarieti ya Kamisheni hii na pale panatajwa kazi za Sekretarieti na ile (a) inasema;

> "Kuandaa na kufanya utetezi na kujenga uwezo katika ngazi zote ili kujiandaa kukabiliana na kurejesha hali baada ya maafa".

Sasa kuna neno linanipa ukakasi silifahamu maana yake nini au pengine halina haja hapa au limeondikwa kwa makosa. Hili neno "kuandaa", haya yanayofuata hapa "...na kufanya utetezi". Kama ilivyokusudiwa ndiyo hivi kufanya utetezi basi hili neno hapa halina mantiki na nilikuwa naomba haya maneno matatu yafutwe "na kufanya utetezi", haya maneno yafutwe na ibakie, "Kuandaa na kujenga uwezo katika ngazi zote ili kujiandaa na kukabiliana na mafaa", ibakie hivi. Neno "kufanya utetezi", nafikiri halileti maana inayolingana na hapa lilipotumika.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende kifungu cha 10 (f) kuhusu "Kazi za Sekretarieti". Ile (f) inasema;

> "Kushirikiana na taasisi mbali mbali katika kuondoa vikwazo vinavyoweza kuzuia juhudi za kukabiliana na maaafa".

Mhe. Naibu Spika, hii ni *point* muhimu sana kwa sababu kuna vikwazo ambavyo mara nyengine vinasababisha maafa kuwa makubwa kwa sababu, kwa mfano kama ikitokea *case* ya majanga ya moto, kuna baadhi ya mahala magari yale ya Zimamoto yanakuwa hayafiki; ama hayafiki kwa sababu ya..., kwa mfano kama ukipita kule Mji Mkongwe kuna baadhi ya chochoro mule vimetiwa vikuta kati kati ambapo kama si vile vikuta gari ingekuwa na uwezo wa kupita, lakini pametiwa vikuta pale, nafikiri ni kwa sababu ya uhifadhi wa mazingira na nini.

Lakini sasa vikuta vile vinazuia gari la Zimamoto lisipite pale. Sasa ikitokea maafa hata gari likitafuta upenyo wa kupita au pengine ishindikane, basi kuna majumba mengi yatakuwa yashateketea.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia, Idara hii inayoshughulikia na Mipango Miji ya Wizara ya Ardhi nayo mara nyengine inaweza ikajikuta inaingia kwenye lawama kwa sababu ya kuachia ujenzi holela. Ujenzi holela ni tatizo kubwa sana ambalo Mwenyezi Mungu ayapushie mbali, lakini likija likitokea balaa katika baadhi ya mitaa yetu, zinaweza

zikaungua nyumba kwa mamia bila ya uwezekano wa gari la *fire* kupita pale kwenda kuzima moto. Kwa hivyo, wawepo makini sana watu wa Mipango Miji ili wahakikishe pale ambapo wananchi wanaelekea kujenga basi waende wakaweke utaratibu wa kujenga ingesaidia sana hilo.

Mhe. Naibu Spika, ukiangalia kifungu cha 10 (k) napo pale pameandikwa, "Kushirikiana na taasisi zinazohusika kufanya ukaguzi na kusimamia majengo, vifaa na nyenzo kilichogundua mambo yanaweza kusababisha maafa. Hii nayo ni muhimu na kwa bahati mbaya pamoja na kutunga sheria, tumetunga sheria ya kuzingatia majengo, yatathminiwe majengo, sijui wakadiriaji, nakadhalika. tumetunga huku. Miongoni mwa mambo muhimu sana ni kuweka njia za kutokea kwenye jengo fulani wakati majanga ya moto yakitokea kwenye lile jengo, lakini mpaka leo bado tunaendelea kuyafungia macho haya mambo na kuna siku yatatudhuru.

Mimi mara nyingi huwa napenda kutoa mfano sana wa Hospitali ya Mnazi Mmoja ambayo ndio hospitali kuu ya nchi yetu. Kuna wakati wa kuwaangalia wagonjwa ile hospitali inakusanya watu kule juu, lakini ukiiangalia njia ya kutokea ni ngazi mbili tena nyembamba, huwezi kufungua *lift* ikitokea janga, utaelekea kwenye ngazi ile ya Kaskazini au ya Kusini, ni nyembamba mno hazina uwezo wa kutoa watu.

Sasa kuna haja ya serikali kuyaangalia majengo ya jamii kama haya ili yawepo na nafasi nzuri, likija kutokea janga watu waweze kuondoka pale kwenye jengo bila ya kuathirika wengi, lakini vyenginevyo Mwenyezi Mungu atuhifadhi sana, yasije yakatokea majanga kama yale pale, itakuja kuwa balaa kubwa, tutakuja kusoma baada ya kupata hasara kubwa.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine ambalo nataka niligusie kuna hii Idara ya Utabiri wa Hali ya Hewa. Idara hii nayo ni muhimu sana ikapatiwa vifaa vya kisasa zaidi na ikapatiwa wataalamu waliobobea katika fani ya utabiri wa hali ya hewa. Hivi juzi nilikuwa nasikiliza redio, Idara ya Hali ya Hewa walitoa utabiri kwamba ndani ya siku mbili kutoka pale, itanyesha mvua kubwa sana itakayoenea maeneo ya Mikoa ya Pwani, ikiwemo Zanzibar na Pemba. Mimi nilikuwa nimekaa kwa wasi wasi mkubwa, maana yake sijui mvua ikinyesha italeta majanga gani, kwa bahati sikuona hata wingu katika maeneo hayo.

Kwa hivyo, hii inawezekana ikawa ni vifaa wanavyotumia sio vizuri au ni taaluma ndogo, lakini kinyume chake wanaweza wakawa wasitowe na wasione kutoa utabiri wa aina hiyo, lakini kumbe kuna upepo mkubwa sana unakuja na ukawahi kavikuta vyombo vyetu vinavyosafiri baharini na hatimaye yakawa majanga yale ambayo kila siku yanatuumiza roho.

Sasa nilikuwa nafikiri Idara hii ya Utabiri wa Hali ya Hewa, katika mikakati ya kukabiliana na maafa, nayo ni muhimu sana ikapewa vifaa vya kisaa na ikapatiwa wataalamu wenye uwezo mkubwa sana wa kuweza kushughulikia mambo ya utabiri wa hali ya hewa.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine katika kifungu cha 11, kinaanzisha Kamati ya kitaalamu ambayo itakuwa chini ya Mwenyekiti wa Katibu Mkuu wa Wizara inayohusiana na Uratibu wa Kukabiliana na Maafa. Sasa katika watu waliotajwa pale sijawakuta wataalamu wa Idara ya Hali ya Hewa, nao ni muhimu sana kuwepo. Kwa hivyo, nilikuwa naomba kama Kamati hii ya wataalamu haitakuwa kubwa sana ni muhimu wataalamu wa utabiri wa hali ya hewa na mtaalamu wa mazingira pia wakawemo katika Kamati hii ya wataalamu.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine niende kwenye kifungu cha 15, ambacho hiki kinaeleza kazi za Kamati za kukabiliana na maafa za wilaya. Ukisoma *section* b(ii), utakuta miongoni mwa kazi zao ni kufuatilia majanga, vihatarishi vinavyosababisha majanga na matishio ya maafa na hali za jamii zilizokatika hatari ya kukumbwa na maafa katika wilaya.

Mhe. Naibu Spika, hoja yangu hapa labda ni kuzikumbusha hizi Kamati za wilaya, kwamba kuna vihatarishi vinavyosababisha au vinavyohashiria kutokea kwa maafa au majangwa na vihatarishi hivi vinasababishwa na mmong'onyoko wa maadili ya vijana wetu.

Mhe. Naibu Spika, vijana wetu wameharibika, ni watumiaji wakubwa wa madawa ya kulevya na mtu akishakoroga akili, yeye mwenyewe ni janga halafu anaweza kusababisha janga pahala pengine. Kuna mtu napenda kumtolea mfano kwa sababu alitokea katika eneo langu. Alivuta bangi akachafua akili yake, akenda akawakamata ng'ombe wa jirani zake akawakata miguu wote, kwa bahati nzuri yule ambaye ng'ombe wake alikatwa miguu alikuwa ni mtu wa

busara, lakini kama asingekuwa mtu wa busara basi angechukua panga akenda kumkata kichwa yule jamaa, akishakumkata kichwa ingekuwa ni vita vikubwa vya kijamii, hayo nayo ni maafa.

Sasa ili kuepuka haya hizi Kamati za wilaya kwa kushirikiana na vyombo ulinzi ikiwemo polisi na hata vikosi, wajitahidi kudhibiti vijana wetu waache tabia hii ya kutumia madawa ya kulevya, ni hatari sana. Maafa mengine yanatokea kwa sababu hiyo tu, kwa sababu wasilipuuze hili, ni jambo ambalo linaweza kuwa hatari sana.

Mhe. Naibu Spika, jambo la mwisho ambalo nilitaka nilitolee mawazo kidogo. Tukiangalia Kamati za kukabiliana na maafa za wilaya, Waheshimiwa Wabunge na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ni Wajumbe mule, lakini hata ukiangalia kwenye Kamati za Shehia sasa, Wabunge na Wawakilishi pia wamewekwa tena mule kwanye Kamati za Shehia.

Sasa nilikuwa na mawazo kwa sababu ndani ya jimbo ingekuwa kuna Kamati ya kukabiliana na maafa ya jimbo, basi tungewabakisha Wabunge na Wawakilishi pale, lakini ya jimbo hakuna kuna ya shehia na kwa kuwa wameshakuwa wajumbe katika Kamati za Wilaya hawa wabunge na wawakilishi, nilikuwa nadhani zile za shehia wakaachiwa madiwani, hasa ukizingatia kwamba kuna kina kifungu kinachosema kwamba, Kamati inaweza kumualika mtu yeyote kushiriki katika Kamati hiyo.

Kwa hivyo, wabunge na wawakilishi ukiwafanya kama ni wajumbe wa Kamati za Shehia, inakuwa mwakilishi huyo huyo au mbunge huyo huyo anakuwa ni mjumbe wa Kamati zaidi ya sita, maana yake pangine jimbo lina shehia sita na zote mwakilishi ni yeye, tutamuongezea mzigo mzito kweli kweli. Sasa ni bora abakie kuwa mualikwa pale ambapo tatizo litatokea, lakini kwa ujumbe abakie kwenye Kamati ya Wilaya.

Mhe. Naibu Spika, nadhani baada ya kusema hayo na kwa umuhimu wa mswada huu, mimi binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Chonga, tunauunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja.

**Mhe. Abdalla Mohammed Ali:** Mhe. Naibu Spika, na mimi nashukuru Adhuhuri hii kunipatia fursa ya kusema kidogo katika sheria hii iliopo mbele yetu.

Mhe. Naibu Spika, kwanza mimi ni imani yangu kwamba sheria hii itabakia tu kwenye makaratasi na kwa dunia inavyokwenda na kwa dua za Masheikh wetu, basi nina imani kwamba maafa yatatuepuka. Kwa maana hiyo labda niseme tu kwamba tunajua hivi sasa wataalamu tuko wengi na kutokana na kuwa wataalamu tuko wengi, huwa tunakuwa na mbinu nyingi za kufanya miradi. Sijui niseme kwamba na hii ni moja tu ya kuona kwamba sasa tuanzishe sheria kama hii ambayo labda itakuwa ni moja tu kati ya miradi ya kujiongezea mapato kwa baadhi ya watu ambao watakuwemo katika kamisheni hizi.

Mhe. Naibu Spika, tumejifunza mengi na Mwenyezi Mungu alituonyesha kwamba yeye bado yupo na kwa maana hiyo tulipata misukosuko mingi katika kipindi cha miaka minne au mitano iliyopita. Lakini katika yote haya yaliyotokea tumesimama pamoja, hatukuwa na kamisheni, wala hatukuwa na nani, Kamanda wa Polisi wala jeshi, yote haya tuliyasimamia pamoja na yalikwenda kwa pamoja na nashukuru tulifanikisha vizuri sana. Sasa leo kuja kwa kamisheni kama hii iliyosheheni watu kama hawa, sifikirii kama itafanyakazi zake kama kawaida.

Mhe. Naibu Spika, labda nikukumbushe tu kwamba Baraza lako tukufu pia lilipitisha sheria ya utalii kwa wote. Lakini la kushangaza ni kwamba huko vijijini anaweza akatokea huyo mgeni ambaye tunamwita mtalii basi yatakayomkuta unashangaa. Sasa kama kweli tuna nia ya sheria kama hizi kuzitekeleza vilivyo, basi tungekwenda mbele. Lakini bado najenga imani kwamba nia ni hiyo hiyo, sio ya kusema kwamba tunaunda kamisheni ya kufanya masuala yetu yawe mazuri na yaende mbele zaidi.

Mhe. Naibu Spika, labda sasa niingie kidogo tu katika sheria hii. Mimi ningependa tu Mhe. Waziri angenieleza kidogo, kwa sababu katika sheria hii inasema; "Kukabili maafa" maana yake ni utoaji wa huduma za dharura na misaada kwa umma. Anapotumia neno hili la "umma" anakusudia nini, kwa sababu baadhi ya wakati hutokea katika mitaa yetu au vijiji vyetu, wengine hupatwa na maafa madogo madogo. Sasa anaposema umma, anakusudia watu watano, watu sita, watu saba au nini hasa iliyokusudiwa hapa, kwa sababu nina wasi wasi kwamba itatokea wakati kama umma ni kuanzia watu kumi, basi watu kumi wale wanapotokewa na maafa wakasaidiwa.

Lakini mtu mmoja au wawili wakawa wao wanapotokewa na na maafa wasisaidiwe, kwa sababu hawajafikia neno "umma" kwa maana ninayoifahamu mimi. Sasa hii nina wasi wasi inaweza ikajakuleta longo longo katika jamii, kwa sababu huo umma atasaidiwa mtu mmoja mmoja pengine. Sasa hawa ambao ni watu wawili tu ambao kwa wakati ule wametokewa na matatizo, hawa na wao watahesabika vipi? Kwa hivyo, ningependa Mhe. Waziri atakapokuja anieleze kwamba umma hapa ana maana ya watu wangapi na ni vipi hii?

Lakini wakati huo huo kuna wengine. Nakumbuka, nina kumbukumbu kwamba katika jimbo lililo na *mortuary*, kuna wakati watu walikula kasa kule na jamii karibu watu wa familia tatu au nne ziliangamia, hawa nao watahesabika kama waliopata maafa au wao watachukuliwa vipi. Kwa hivyo, Mhe. Waziri anifafanulie kidogo hii umma anakusudia kufanya nini. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nikirejea ile dhana yangu ya mwanzo ya mkururo wa watu. Hii kamisheni imeandaliwa kama vile tunaandaa vita, naona humu makamanda, huku makamanda kama kuna tatizo fulani. Nafikiri sheria ingeanzia chini kutoa taaluma, yaani elimu na sio kusubiri tu kwamba sisi tuna lile tatizo ndio tukalikabili, tutafute kamanda wa KMKM, kamanda wa JWTZ na kamanda wa Valantia.

Mhe. Naibu Spika, kuna majanga mengine ambayo yanataka elimu huku mwanzo ili yasije yakatokea maafa. Sasa mfumo huu wa kuweka kamisheni hii au hii Kamati yenyewe, naona kama vile sijui kuna vita hapo mbele au vipi, kwamba makamanda watupu. Hebu fikiria waziri sisi tunakwenda mbele tu, tunasubiria jambo litufike hatuna maandalizi yoyote ambayo hivi sasa tunahitaji wataalamu ambao watasaidia lile jambo lisije kufika.

Kwa sababu kuna uchomaji wa mashamba ukame ambapo watu wanakata miti, hatuhitaji watu katika Kamati hii ambao watapita kutoa taaluma vijijini na kuelimisha kama alivyosema wajina wangu pale, kwamba ujenzi pengine wa kiholela ambao unasababisha pengine ikipata ajali nyumba moja basi moto uenee kwa haraka. Hatuhitaji watu kama hao, tunaowahitaji ni vikosi tu katika Kamati kama hizo.

Mhe. Naibu Spika, naomba waziri angeangalia hivyo, kwamba hapa hatuandai mapambano, tunaandaa utaratibu wa kuondosha, labda hata na Masheikh wangekuwemo, kwa sababu na wao kwa vile sisi ni Waislamu dua zao zinafika mbali za kuondoa mengine yasitufike, hawahitajiki?

Mhe. Naibu Spika, naendelea kidogo katika kifungu cha 4 kinasema;

> "Katibu Mkuu wa Wizara inayohusika na uratibu wa kukabiliana na maafa atakuwa Katibu wa Kamisheni".

Mhe. Naibu Spika, kwa nini awe Katibu Mkuu, huyu Katibu Mkuu wa wizara ana majukumu yake na kamisheni nyingi tulizoziweka zina makatibu wao, kwa nini kamisheni hii sasa huyu katibu ashughulike na kamisheni hii, asitafutwe mtu mwengine au huyu mtendaji akawa anatosha, katibu akawachiwa majukumu mengine ya kufanya, yeye aendelee na kuwa ni katibu. Nafikiri angeangalia waziri kwamba huyu majukumu yake yatakuwa ni makubwa au iwe ndio tumeiweka tu iwe ndio haifanyikazi yoyote, sifikirii kwamba yeye awe ndio Katibu Mkuu halafu apewe kazi ya kamisheni kama hii aje afanyekazi zake zinavyotakikana. Mhe. Waziri, ingeangaliwa kama kuna uwezekano basi hapa akatafutwa mtu mwengine ambaye atakuwa ni makini zaidi au hata huyo mkurungenzi mwenyewe basi angetosheleza tu bila kumpa majukumu mengine Katibu Mkuu.

Mhe. Naibu Spika, labda niende kidogo katika adhabu. Naona wakati umemaliza dakika mbili zilizobakia niende makosa na adhabu. Hapa tunasema kwamba mtu ambaye atakuwa anatenda kosa akiwa amekataa kusalimisha mali. Kwa sababu mswada huu sijauona wa kiingereza anakusudia nini, kusalimisha to *surrender* au *to summit,* kufanya nini?

Lakini pia, makosa haya tungejaalia kwamba yatatokea, hakuna yule mtu ambaye kafanyakosa la kusababisha majanga au maafa samahani, yule mtu ambaye kafanya maafa kwa makusudi baharini kenda kuigonga meli na imezama. Je, huyu mtu tutamuweka katika kundi gani, kwa makusudi kenda kutia moto msitu hatimae pamesababisha jangwa, huyu mtu hukumu yake iko wapi?

Mhe. Naibu Spika, tujaalie kwamba labda mtu kenda kaazimwa gari yake apeleke maji hakutaka, sasa yeye ndio atakuwa ametiwa katika hatia kama hii. Lakini je, kusalimisha anakusudia nini?

Mhe. Naibu Spika, naona muda wako nimechukua wa kutosha nashukuru kwa hayo. *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsanteni Waheshimiwa Wajumbe, nawashukuru kwa ushirikiano wenu mlionipa tangu asubuhi hadi mchana huu. Naomba niwaarifu kwamba katika orodha yangu ya wachangiaji nimebakiwa na wachangiaji watano. Tukija jioni mapema ataanza Mhe. Mgeni Hassan Juma, Mhe. Ismail Jussa Ladhu, Mhe. Salma Mohammed Ali, Mhe. Suleiman Hemed Khamis na Mhe. Hija Hassan Hija. Naahirisha kikao hadi saa 11:00 za leo jioni.

*(Saa 7:00 mchana Kikao kiliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Salma Mohammed Ali:** Mhe. Naibu Spika, kwanza hatuna budi tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika hapa tukiwa wazima na kufanya wajibu wetu. Pili nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kutoa maoni yangu machache katika Mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, katika ukurasa wa mia tatu baada ya *paragraph* inayoeleza maana ya maneno maafa yanayosababishwa na binaadamu, naomba ifuatiwe na *paragraph* ya maneno inayosema, maafa yanayosababishwa na Serikali. Ninasema hivi kwa sababu maafa mengi yanayotokea huja kwa sababu ya uzembe mkubwa unaosababishwa na Serikali yenyewe, kwa kutilia nguvu hoja hii naomba uniruhusu nitoe mifano.

Mhe. Naibu Spika, kuna kama maafa ya moto hivi tujiulize katika majengo ya Serikali kwenye maduka na viwanda je vifaa vya kuzimia moto vipo, na vinakaguliwa. Nina hakika Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengi havipo hivyo vifaa na hivyo vilivyopo basi havifanyi kazi, je pakitokea moto na ukashindwa kuzimwa sio Serikali yenyewe iliyosababisha maafa haya.

Lakini vile vile Mhe. Naibu Spika, mfano mwengine katika wilaya zetu magari ya kuzimia moto yako mangapi, na je ni mazima au mabovu na muda wote huwa yanakuwa na mafuta, na katika matangi huwa yana maji. Mara nyingi hutokezea kuungua kwa majengo na hufika kumalizika kwa majengo yale ndipo badala yake hutokea gari la Zimamoto bila ya hata aibu, kwa hivyo pia maafa haya Serikali inachangia kutokea kwa maafa haya.

Mhe. Naibu Spika, pia katika taratibu za ujenzi na usambazaji wa maji huwa panaweka maeneo na vifaa maalum vya kuchukulia maji magari ya Zimamoto wakati panapotokea maafa, maeneo hayo huwekwa koki na mifereji ya wima. Lakini Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu huu umepuuzwa koki na mifereji ya wima zimevunjwa na hata katika hiyo miundo mbinu inayowekwa sasa basi haziwekwi, je iwapo Mheshimiwa Naibu Spika, patatokea moto na gari la Zimamoto likashindwa kupata maji maafa haya tuseme kayasababisha nani kama si Serikali yenyewe.

Lakini vile vile Mhe. Naibu Spika, katika utaratibu wa ujenzi mamlaka husika zinapuuza usimamiaji wa ujenzi unaoruhusu gari za Zimamoto kupita, kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, huachiwa wananchi wakajenga kiholela na baada yake moto unapotokea humaliza kijiji kizima bila ya gari la Zimamoto kuweza kufanikiwa kupita, kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, maafa haya pia huwa yanasababishwa na Serikali.

Lakini tuje kwenye maafa ya mafuriko, maafa ya mafuriko mara nyingi huwa yanasababishwa na mvua kubwa maji ya mvua huvamia nyuma zilizojengwa mabondeni. Mhe. Naibu Spika, maafa haya yakitokea wakulaumiwa ni nani, wakati Serikali ipo na inawaachiwa wananchi wajenge holela huku wakisubiri maafa yatokee kisha waweke vikao vya omba omba. Mhe. Naibu Spika, nadhani katika hii mifano niliyotoa Serikali isijitoe kujiwekea maana kama na wao wamo katika wasababishaji wa maafa.

Lakini vile vile Mhe. Naibu Spika, ukiusoma huu Mswada utaona kamati nyingi zimeundwa Kamati ya Taifa, Wilaya, Shehiya. Lakini ukisoma kazi za kamati hizi nyingi ni kushughulikia maafa yakishatokea, naomba sote tuzingatie methali ambazo wametueleza wazee wetu waliopita kama kinga ni bora kuliko tiba, kwa hivyo kwa kuandaa kamati hizi na ikawekewa kazi za kushughulikia maafa yakishatokea nadhani si sahihi.

Mhe. Naibu Spika, mimi naona Mswada huu ungelikuwa na maana zaidi kama kamati zilizoundwa zingelijikita katika hatua za kuzuia maafa katika maeneo mbali mbali niliyoyataja na hata ambayo sikuyataja, kwa sababu Mhe. Naibu Spika, hata katika maafa yaliyotokeya baharini kwa kuzama kwa vyombo vile, ripoti zote mbili zilionyesha kama maafa yale yalisababishwa na uzembe wa watendaji wa Serikali. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, naomba hapa Serikali iwe makini na nashauri sana *paragraph* ya maana ya maneno yenye kusema maafa yanayosababishwa na Serikali ifuatie baada ya maana ya maneno ya maafa yanayosababishwa na binaadamu.

Lakini vile vile ukizingatia Mhe. Naibu Spika, kuna kama jengo la Mtemani jengo namba nne, jengo lile ni bovu na limewekewa mwega kama mgomba sasa jengo lile likianguka wakiumia wale waliomo na hata wapitao maafa haya Mhe. Naibu Spika, tuseme kasababisha nani?. Kwa hiyo naomba Mswada huu uzingatie mambo hayo.

Nakushukur sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi na nitaunga mkono Mswada huu baada ya kupata ufafanuzi juu ya masuala yaliyomo. Ahsante sana.

**Mhe. Ismail Jussa Ladhu:** Mhe. Naibu Spika, awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru Muumba Mwenyezi Mungu Subuhanahu wataala kwa kutujaalia kuwa hai na wazima, na tukaweza kukutana tena hapa katika mkutano huu wa Baraza la Wawakillishi. Nikushukuru na wewe Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi na mimi baada ya kuwasilisha maombi yangu kuchangia mjadala wa Mswada wa Sheria ya kuanzisha Sheria ya Kupunguza na Kukabiliana na Maafa Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Naibu Spika, nimetumia makusudi neno kuchangia mjadala wa Mswada kwa sababu unatofautisha, baina ya mjadala wa Mswada na mjadala kuhusiana na Mswada. Ili nieleweke niseme kwamba binafsi nimesikitishwa sana na kitendo cha Serikali kutojipanga vyema na matokeo yake kulipelekeza Baraza hili ovyo kabisa, kwa nini nasema hivyo Mheshimiwa Naibu Spika, katika Miswada minne ambayo itajadiliwa katika Mkutano huu wa Baraza la Wawakilishi unaoendelea, miswada mitatu ya Sheria imewasilishwa kwa hati ya dharura kwa maana hati iliyotiwa saini na Mheshimiwa Rais.

Mhe. Naibu Spika, kitendo hichi si kitendo ambacho kinapaswa kuachiwa hivi hivi bila ya kutolewa kauli na Baraza lako, kwa nini nasema hivyo Mheshimiwa Naibu Spika, chombo hichi cha Baraza la Wawakilishi ni chombo kikubwa sana na kimetambuliwa katika Katiba ya Zanzibar katika ibara ya 5 (a) inayozungumzia mgawanyo wa madaraka. Katika ibara hiyo Mhe. Naibu Spika, naomna niinukuu inasema 5(a) Zanzibar itafuata mfumo wa mgawanyo wa madaraka kati ya Mamlaka tatu, Mamlaka ya Utendaji, Mamlaka ya Kutunga Sheria na Kusimamia utekelezaji wa Shughuli za umma na Mamlaka ya Kutekeleza utoaji haki.

5(a)2 inasema Mamlaka ya Utendaji ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mamlaka ya Kutunga Sheria na kusimamia utekelezaji wa Shughuli za Umma ni Baraza la Wawakilishi na Mamlaka ya kutekeleza Utoaji Haki ni Mahkama.

5(a)3 Inasema hakuna Mamlaka itakayoingilia Mamlaka nyengine isipokuwa kama na kwa kadri ilivyoelezwa katika Katiba hii.

Mhe. Naibu Spika, nilipo mimi zaidi ni katika 5(a) kijifungu kidogo cha pili au ibara ndogo ya pili inayoelezea mamlaka hizi tatu, na baadae Katiba yetu ya Zanzibar mwaka 1984 ikafafanua mamlaka ya Baraza la Wawakilishi na uwezo wake, katikia Ibara ya 78 ya kuhusiana na nguvu za kutunga Sheria, na baadae ibara ya 87 na 88 ikaweka utaratibu wa kujadili Miswada lugha ya Miswada na namna ya Baraza la Wawakilishi litakavyotekeleza kazi zake. Na mmoja wapo katika ibara ya 88(a) inasema Baraza la Wawakilishi pamoja kuongoza shughuli zake kutokana na vifungu vya Katiba hii litafanya kazi kwa mambo yafuatayo ya utekelezaji, (a) Kutunga Sheria pale ambapo utekelezaji wa jambo unahitaji kuwepo kwa Sheria hiyo.

Sasa Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni Katiba yetu na haya ndio Mamlaka ambayo imekipa chombo hiki, lakini kama hivyo haitoshi Katiba hii hii imetamka kwamba Baraza hili litakuwa na mamlaka ya kutunga kanuni za kuongoza shughuli zake, na tumetunga Kanuni Mhe. Naibu Spika. Kanuni zetu zimeelekeza utaratibu wa Serikali kuwasilisha Miswada katika chombo hichi na utaratibu wa Baraza hili kushughulikia Miswada hiyo.

Mhe. Naibu Spika, kanuni ya 79 katika Kanuni za Baraza la Wawakilishi imeweka utaratibu huo na kwa sababu ya kunusuru muda sitoisoma yote, lakini kwa madhumuni ya kueleweka naomba nisome sehemu yake.

"79(1) Inasema Mhe. Naibu Spika, kila Mswada wa Serikali utatangazwa katika gazeti la Serikali katika toleo angalau moja, lakini iwapo matoleo yatazidi moja kuwe na kitambo kisichopungua siku saba katika hilo la kwanza na la pili.

Kanuni ya 79(2) inasema tangazo la kwanza la Mswada wa Serikali litatokea kukiwepo angalau siku 21 kabla ya Mswada huo kusomwa kwenye Baraza kwa mara ya kwanza na litakuwa linaonyesha Mswada mzima, pamoja na maelezo yaliyotiwa style na Waziri yanayotaja madhumuni na sababu za Mswada huo".

Lakini Miswada ya dharura imetajwa wapi Mhe. Naibu Spika, imetajwa katika kanuni ya 80 inasema. "Endapo shahada iliyotiwa saini na Rais itawasilishwa mbele ya Baraza na Waziri akitamka kwamba Mswada wa Serikali ni wa dharura na wa haraka sana hata kuwa haiwezekani kutimiza masharti ya Kanuni ya 79 basi masharti hayo yatawekwa kando kwa jili ya mswada huo". Hivyo Kanuni ya 79 itasita kutumika bila ya hoja yoyote.

Mhe. Naibu Spika, nimeona nianze na maneno haya kwa sababu nimesema mwanzo naona Serikali haikitendei haki chombo hichi na inakipelekesha ovyo *(Makafo)*

Mhe. Naibu Spika, tumeweka taratibu katika Kanuni hizi kwamba Mswada unasomwa mara tatu sasa, unasomwa mara ya kwanza baada ya kuwa umechapishwa katika Gazeti rasmi la Serikali na ukitoa angalau siku 21 kuanzia tarehe ya kuchapishwa ili usomwe kwa mara ya kwanza, madhumuni ni kuwa Wajumbe kupata nafasi ya kujisomea, lakini madhumuni vile vile ni wawakilishi na tumeitwa wawakilishi kwa sababu tunawakilisha tupate nafasi ya kwenda kuchukua maoni ya watu. Lakini vile vile kamati zimepewa muda wa kuita maoni ya wahusika mbali mbali kupata maoni yakiwemo maoni ya kitaalam, kwa nini maoni ya kitaalam Mhe. Naibu Spika, kwa sababu Muwakilishi hata akiwa na fani yake na taaluma yake hawezi kuwa mtaalam wa kila fani na kila jambo, mimi nimesomea Sheria lakini siwezi kuwa mtaalam wa ujenzi, siwezi kuwa mtaalam wa afya, siwezi kuwa mtaalam wa elimu, siwezi kuwa mtaalam wa mambo mengine kadhaa wa kadhaa fani zisizo za hisabu.

Sasa unapoleta Mswada bila ya shaka utakuwa unahusu fani fulani au taluma fulani, kuna baadhi ya mambo Mswada hauhusu utungaji wa Sheria tu unataka pia kutambua lile lililoundiwa sheria, kwa hivyo ndio maana tunawekewa utaratibu wa kusoma kwa mara ya mwanzo, likikamilika hilo Mhe. Naibu Spika, na baadhi ya Kamati kujiridhisha ndio tunapokuja na hatua ya pili Mswada sasa kuja kusomwa kwa mara pili ili kufungua mjadala na hatimae kwa mara ya tatu wakati wa kupitishwa kabisa mwisho wake.

Sasa Mhe. Naibu Spika, utaratibu huu daima uheshimiwe natambua kuwa kuna Miswada ya dharura na ndio maana Kanuni zetu zimetambua hilo na zikaweka misingi yake, lakini nimekisoma makusudi Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu hiki cha Kanuni ya 80 kwamba maneno yaliyotumika ni kwamba akitamka kwamba Mswada wa Serikali wa dharura na wa haraka sana, sasa kinachonisikitisha Mhe. Naibu Spika, na Serikali ni kwamba inageuza sasa utaratibu wa Miswada ya dharura ndio utaratibu wa kufanya kazi Serikali na chombo hiki.

Mhe. Naibu Spika, katika Baraza lililopita palikuja Miswada hapa palikuja Mswada wa Sheria ya kufuta Sheria ya Tawala za Mikoa namba moja kwa mwaka 1998, na kuanzisha upya Sheria ya Tawala za Mikoa ya mwaka 2014 na mambo mengine yanayohusiana na hayo umeletwa kwa hati ya dharura huo, ukijuliuliza uharaka wake maana yake Kanuni zimetamka wa dharura na wa haraka sana, dharura yake na haraka sana ipi hakuna maelezo ya kuridhisha chombo hichi Mhe. Naibu Spika.

Ukaletwa Mswada mwengine katika Mkutano uliopita Mswada wa Sheria wa kufuta Sheria ya Baraza la Manispaa nambari tatu ya mwaka 1995, na Sheria ya Halmashauri za Wilaya na Mabaraza ya Mji Namba nne ya mwaka 1995 na kuanzisha upya Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa Zanzibar ya mwaka 20014 kwa madhumuni ya kuhaulisha Serikali za Mitaa uwezo wake kazi na wajibu, muundo, mpangilio, fedha na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Na huu pia hatukuambiwa kwa nini wa dharura kwa nini wa haraka sana, lakini Mhe. Naibu Spika, kumbe Serikali ilipobaini kwamba imeachiwa imeona sasa huu ndio mtindo, katika mkutano huu Miswada minne imeletwa mitatu imeletwa kwa hati za dharura tunampotosha Mheshimiwa Rais washauri wake Mhe. Naibu Spika *(Makofi)*

Mimi nimwambie Mheshimiwa Rais watendaji wake na washauri wake wanampotosha ikiwa wao hawawajibiki ipasavyo, wakamfanya yeye anatia saini hati za kuleta Mswada wa dharura Barazani hapa Miswada ambayo si ya dharura wala si ya haraka sana, ni kwa sababu tu serikali chini ya Ofisi ya Makamo Pili wa Rais imewapa watu wa

kuratibu mambo haya, imeshindwa kutekeleza wajibu wake, imeshindwa kufanya kazi zake, kwamba hakuna Miswada mpaka Baraza linakaribia ndio watu wanatoka kitimtim wanakuja kumtilisha saini Rais, anakuja hapa tunaletewa Miswada...hii sio kuwatendea haki wananchi, sio kukitendea haki chombo hiki Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, ndio maana nikasema nachangia mjadala wa Mswada, kwa sababu tutizame tangu asubuhi mijadala inavyokwenda hapa. Mhe. Naibu Spika. huwezi, suala la kukabiliana na maafa kwa mfano, Mswada tunaoujadili sasa hivi ni suala zito ambalo nchi hii imeshakumbana na mikosi miwili mikubwa katika kipindi hichi mbali ya mengine tuseme ya maumbile *natural disaster*. Pametokea ajali ya *MV. Spice Islander* hapa watu kwa maelfu wamekufa. Pametokea ajali ya *MV. Skagit* ya muda mfupi, watu kwa mia wamekufa.

Mhe. Naibu Spika, nilidhani kwamba hii ingekuwa ndio kiamsho chetu sisi kwamba tunatakiwa kujipanga vizuri zaidi. Sasa unapoleta Mswada ambao unaratibu suala kama hili, unasimamia suala kama hili, unatekeleza suala kama hili ukawaletea Wajumbe kwa hati ya dharura kwamba Mswada unapewa juzi leo ujadiliwe, tunatendea haki nchi hii na wananchi wa nchi hii.

Mhe. Naibu Spika, tutaishia kuondosha njia na kuripua kazi humu ndani na ni hasara na hatari kubwa sana kwa nchi, kwamba unafanya jambo kubwa kama kutunga sheria kwa staili ya kuripua na kuondosha njiani.

Leo Mhe. Naibu Spika, ikawa tunaupitia juu juu tu hapa mtu anachangia na tumeona staili ya uchangiaji tangu asubuhi Mhe. Naibu Spika. Halafu tukapata sheria mbovu, kesho kutwa ikawa haikukidhi mahitaji ya kuondoleana maafa, Mwenyezi Mungu aepushie mbali, atakuwa nani hakutekeleza wajibu wake, chombo hiki cha kutunga sheria au serikali iliyoletwa Mswada kwa hati ya dharura kwa jambo zito kama hili.

Mhe. Naibu Spika, huku sio kuwatendea haki wananchi wa Zanzibar, huku sio kukitendea haki chombo hichi. Matokeo yake ukiangalia Mswada huu kwanza sheria zetu hapa katika nchi hii zinaletwa Barazani, lugha inayotumika ni Kiswahili kwa hivyo Mswada wa msingi unaotumika ni wa Kiswahili. Lakini sote tunajua kwamba sheria zetu zinabakia katika vitabu vya sheria kwa lugha ya kiingereza. Ndio maana mara nyingi wajumbe wako wanapokuwa makini wanafanya kazi kubwa ya kulinganisha maandishi yaliyokuwemo katika Kiswahili na tafsiri ya Kiingereza yanawiyana, tumesaidiana mara nyingi humu ndani.

Mhe. Naibu Spika, leo mimi nimepewa nakala ya Kiingereza wakati naingia pale jioni hii. Napata wapi muda wa kulinganisha kwamba niseme lugha iliyuokuwemo humu na humu zinawiyana ni sawa sawa.

Mhe. Naibu Spika, lakini kama hiyo haitoshi ukenda kwenye madhumuni na sababu za Mswada wa sheria hii naomba tuiangalie, ndio mambo ya kuripua yanavyoishia Mhe. Naibu Spika. Ukurasa wa 317 mwisho kule inasema:

> "Sehemu ya Nane: inahusu masharti mengineyo yanayoelezea kuhusu kinga ya Afisa wa Kamisheni, utoaji wa taarifa za maafa, uwezo wa Waziri Kutunga Kanunu kufuatana na kubakiza Sheria ya Kukabiliana na Maafa Namba 2 ya Mwaka 2003".

Mhe. Naibu Spika, nimeitizama hii Sehemu ya Nane iliyotajwa katika madhumuni haya, ambayo ipo katika ukurasa wa 315 ya gazeti rasmi la serikali. Kuna vifungu vitatu hapa, kuna kifungu cha 45, 46,47, nimetizama kote hapa, wapi katika sehemu hii kuna vifungu vinavyohusu Kubakiza Sheria ya Kukabiliana na Maafa Nambari 2 ya mwaka 2003 sijaviona.

Mhe. Naibu Spika, narejea tena, madhumuni yanatwambia Sehemu ya Nane inahusu masharti mengineyo yanayoelezea kuhusu Kinga ya Afisa wa Kamisheni, utoaji wa taarifa za maafa, uwezo wa waziri kutunga kanuni, kufuatana na kubakiza Sheria ya Kukabiliana na Maafa Nam. 2 ya Mwaka 2003.

Sasa naangalia wapi hayo masharti ya kubakiza kanuni au kubakiza sheria ya mwaka 2003, katika Sehemu ya Nane ambayo ina kifungu cha 45, 46, 47, sioni. Kifungu kinachohusu Kanuni Mhe. Naibu Spika, ni kifungu cha 47, naomba mtu akisome kuanzia mwanzo mpaka mwisho, atusaidie labda mie kiswahili changu leo cha Makunduchi kimenipiga chenga kwamba hapa panazungumzwa kubakiza, sijaona miye, sio Sheria sio Kanuni.

Mhe. Naibu Spika, haya ndio mambo ya kuripua na nikasema watendaji wa serikali wana muangusha Mhe. Rais wanapomsainisha hati za kuleta Miswada kwa dharura, ikiwa Miswada imejaa matatizo kama haya na huku wajumbe hawawezi kuwa makini kuisaidia serikali, kwa sababu Mswada wamepewa juzi leo wajadili na tuupitishe hapa, huu sio utaratibu mzuri hata kidogo.

Mhe. Naibu Spika, niseme jengine. Kuonesha kwamba hatujui hata tunachokifanya. Nilipoisoma kanuni ya 79 nilisema kwamba imesemwa masharti ya kawaida ni Mswada uchapishwe angalau siku 21 kabla ya kuwasilishwa na kusomwa kwa mara ya kwanza. Sasa wao wametwambia Miswada hii ni ya dharura. Miswada ya dharura Kanuni ya 80 inasema hupaswi kufuata masharti ya Kanuni ya 79, lakini tizama kilichofanyika Mhe. Naibu Spika.

Hii Miswada tuliyogaiwa juzi kwenye Kikao chako cha *briefing* hili gazeti rasmi la serikali, hili limefanywa kwamba, natumia makusudi neno hili limefanywa kwamba limetoka tarehe 30 Disemba 2014 ndiyo tarehe yake hapa. Ukihesabu mpaka tarehe 21 Januari kwenye tangazo ni siku 21. Kwa hivyo hapa imefanywa tuamini kwamba siku 21 zimetimia. Sasa ulipaswa ujiulize kwamba serikali hii ilikuwa inajua Mswada huu ni wa kawaida unafuata siku 21 kwa hivyo gazeti limeandikwa tarehe zitimie siku 21 au ni wa dharura kwa hivyo umekuja kwa hati ya dharura imetiwa saini na Mhe. Rais, kipi ni kipi?

Haya ndio mambo ya kuripua Mhe. Naibu Spika, serikali makini haifanyi mambo yake kwa staili ya kuripua. Lakini baya zaidi kama nilivyosema serikali inafanya mambo yake kwa kuripua kuondosha njiani, matokeo yake inakipelekea na chombo hiki kikubwa cha wananchi nacho kifanye kazi kwa kuripua na kuondosha njiani. Hii si haki Mhe. Naibu Spika na kama nilivyosema suala lenyewe tunalolijadili ni suala la kuanzisha Sheria ya Kuanzisha Kamisheni ya Maafa ambayo nchi hii tumeshakabiliana nayo makubwa katika miaka mitano hii mara mbili. Ilipaswa iwe fundisho kwamba tupate muda wa kutosha, tupate muda Kamati zipate wataalamu wakae nazo, wazisaidie utaalamu, ili kama kuna mapungufu turekebishe tuwe na sheria nzuri, halafu tuje tupambane katika utekelezaji baadae.

Mhe. Naibu Spika, jengine katika hayo niliyoyasema hii kwenye madhumuni na sababu inasema kwamba kuna vifungu vya kubakiza Sheria ya Kukabiliana na Maafa Nam. 2 ya Mwaka 2003. Ukiwasikiliza wajumbe wengi waliochangia hapa tangu asubuhi wanazungumza kama vile hii ni sheria mpya hatujapata kuwa nayo. Lakini utawalaumu vipi waheshimiwa wajumbe ikiwa Mswada wenyewe wamepewa juzi kwa vile matayarisho ni ya siku mbili. Mimi baada ya kwenda kuiyona nimekwenda kuitafuta hii sheria ya mwaka 2013 nnayo hapa Mhe. Mhe. Naibu Spika, hii hapa na inayo saini ya Mhe. Amani Abeid Karume, katia saini kama Rais wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, katika hali ya kawaida ningepata muda unaotakiwa ilikuwa ni kazi yangu kama ni mwakilishi na kazi ya waheshimiwa Wawakilishi wengine, kulinganisha kwamba kuna tatizo gani katika sheria hii inayopelekea serikali itake kuifuta ilete sheria mpya. Kwa sababu katika sheria kunatakiwa kuwe na *mischief* katika sheria ili kuiondosha ulete sheria mpya inayoondosha *mischief* ile. Sasa leo mie katika madhumuni na sababu kote huku waziri hakutwambia popote katika maelezo haya hapa kurasa mbili hizi hapa au moja na nusu. Nini mapungufu ya sheria hii ambayo imepelekea serikali kuifuta na kuleta sheria hii. Kwa hiyo Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema tuna matatizo makubwa sana.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu sisi wametunyima fursa ya kufanya kazi yetu nawaomba wao waliofanya kazi watwambie sasa, sheria hii ya mwaka 2003 ina mapungufu gani ya msingi yaliyopelekea yaonekane kwamba haifai hata mlete itungwe sheria mpya, naomba maelezo.

Lakini la pili naomba vile vile watwambie walipotunga sheria hii mpya wameangalia uzoefu wa nchi gani. Mhe. Naibu Spika, nimalizie kwa mfano mwengine katika hoja hii na namalizia sasa hivi Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, katika madhumuni na sababu tena tunaambiwa katika paragrafu ya pili tunaambiwa kwamba aidha sheria mpya itawiyana na sera ya kukabiliana na maafa ya mwaka 2011 pamoja na makubaliano na mikataba ya kikanda na kimataifa inayohusiana na masuala ya kukabiliana na maafa iliyoridhiwa na nchi yetu. Tunarudi pale pale, kama Wawakilishi tulipaswa tujiridhishe kwamba yepi yamezingatiwa. Lakini huo muda wa kuyatafuta haya na kuyapata uko wapi kama Mswada unapewa moja siku ya tatu unawasilishwa ndani ya Baraza.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema hali hii haitoi fursa wala nafasi ya Wawakilishi kufanya kazi yao ipasavyo. Mimi kwa kawaida yangu sitoweza kufanya kazi ya kuripua. Lakini nataka nioneshe mifano michache tu Mhe.

Naibu Spika ya ndani ya Mswada. Halafu naomba Waziri akija katika haya anisaidie. Sheria ikiwa mbaya, ikiwa Wawakilishi hawakuwa makini katika kuitunga hapa, mzigo huu utabeba serikali uliamua kuja na staili hiyo ambayo wamekuja nayo.

Mhe. Naibu Spika, katika kifungu cha nne cha Mswada kinazungumzia muunda wa Kamisheni na inasema hivi:

"4.(1)Kamishen itakuwa chini ya uenyekiti wa Makamu wa Pili wa Rais.
(2) Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais atakuwa Makamu Mwenyekiti.
(3) Wajumbe wa Kamishen watakuwa:
(a)Mawaziri wote wa serikali,
(b) Mwanasheria Mkuu wa Serikali,
(c) Katibu Mkuu Kiongozi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi,
(d)Wakuu wa Mikoa wa Zanzibar,
(e) Kamanda wa Brigedia ya Zanzibar, Jeshi la Wananchi la Tanzania,
(f) Kamishna wa Polisi Zanzibar,
(g) Naibu Mkurugenzi Mkuu wa Usalama wa Taifa, Zanzibar,
(h) Mkuu wa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo KMKM, na
(i) Kamishna wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi.

Mhe. Naibu Spika, hii serikali nzima ukimuondoa Rais na Makamu wa Kwanza na Rais. Sasa naomba tusaidiwe kwamba hii Kamishen ni serikali ndogo nyengine. Kwa sababu kwa ukubwa huu na Wajumbe hawa najiuliza mimi kweli hili litafanya kupelekea ufanisi.

Mhe. Naibu Spika, niseme kwa uzoefu wa nchi za wenzetu wakati wa maafa makubwa zaidi ni vita. Kwa hivyo zimezoeleka katika nchi za Jumuia ya Madola kuwa na kitu wanakiita *war cabinet.* Lakini hata hiyo *war cabinet* inaongozwa na mkuu wa serikali ambao katika mfumo wa Jumiya ya Madola ni Waziri Mkuu lakini haijumuishi Mawaziri wote, inakuwa ni baadhi ya mawaziri muhimu. Hii mawaziri wote, wakuu wa vikosi vyote, wakuu wa mikoa wote. Sasa najiuliza hii tunaunda serikali nyengine ndogo kwa kutumia sheria hii, naomba nisaidiwe.

Mhe. Naibu Spika, jengine naomba nisaidiwe katika ukurasa wa 303 kifungu cha (7). Katika sheria hii ambayo inafutwa ilikuwa inasema kwamba Katibu Mkuu wa Ofisi ya Waziri Kiongozi na kwa lugha iliyotumika humu ndani hawakuitaja hivyo, wamesema 4(1) ya sheria hii inayofutwa na sina hakika kama inafutwa *by the way* Mhe. Naibu Spika, maana hii sheria kasema haikuifuta sheria hii. Huu Mswada huu hauna kifungu cha kuifuta hii, lakini inasema:

*"4.(1) The Principal Secretary of the Ministry responsible for matter regarding the co-ordination of relief during disaster shall be the Executive Secretary of the Commission and shall be responsible to the Minister for the discharge of its functions under this Act."*

Kwa maana ya kwamba Katibu Mkuu wa Wizara inayoshughulikia maafa ndio anakuwa Katibu Mtendaji wa Kamisheni kwa hali ya sasa tumesema kwamba Katibu Mkuu katika Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais. Lakini hapa ni tofauti, hapa kunaanzishwa Mkurugenzi mtendaji. Ningetegemea na ningedhania Mhe. Naibu Spika, kwamba kwa sababu hiyo kwamba pangetizamwa utaalamu, lakini katika sifa zilizotajwa ni kwamba 7(2) inasema:

7(2) "Mtu atafaa kuwa Mkurugenzi Mtendaji ikiwa ni:
(a) Mzanzibari,
(b) Mwenye angalau Shahada ya Kwanza ya fani inayohusiana na uongozi,
(c) Afisa Muandamizi wa Umma."

Mhe. Naibu Spika, dunia imebadilika kwa kasi sana, siku hizi kina fani ina *degree* yake na inasomeshwa hata hii *disasters management* watu wanachukua degree wana shahada zao. Sasa kwa nini kama tunataka kufanya kiwe *professional* hichi chombo tumekitoa katika mfumo wa zamani kwamba Katibu Mtendaji ndio tunakuja katika mfumo kwamba kuwa na Mkurugenzi Mkuu. Kwa isiwepo kwamba mtu mwenye shahada katika fani inayohusiana na kukabiliana na maafa. Tunasema fani uongozi na tumeona maafa yaliyopita yalivyoshughulikiwa katika nchi hii, shagh'ala bagh'ala ilikuwa pale bandarini. Tuliwakuta viongozi wa serikali mawaziri wanatukanana wenyewe kwa

wenyewe pale Bandarini tunashuhudia kwa macho yetu Mhe. Naibu Spika. Sasa unapoweka Mkurugenzi mtendaji kwamba fani yake ni ya uongozi tu anatosha, mimi huwa najiuliza Mheshimiwa kwamba hili linatosha sasa mengine Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema kwamba ningeomba maelezo ya jumla kuhusiana na tafauti ya Miswada hii kimsingi matatizo ya Mswada huu yalikuwa wapi sheria hii hadi imebidi kuja hii.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie kwa kusema suala moja kwamba Mswada huu kwa jumla katika Kamati za Mikoa na Wilaya na Shehia imewatambua viongozi wake kwua Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Masheha na wameingiwa katika kamati mbali mbali, si tatizo katika mfumo wa utawala wa nchi. Tatizo linakuja inapokuwa hawa viongozi wenyewe tunaowataja wanaowacha kufanya shughuli zao za kiserikali wakajifanya ni sehemu ya siasa.

Mhe. Naibu Spika, hizi tunavyozungumza tumezowea kuwaona mpaka wiki hii inayoendelea Wakuu wa Mikoa wamevaa mishati ya chama fulani wanajiingiza katika shughuli za kisiasa za chama kile. Lakini tuna taarifa vile vile za Wakuu wa Mikoa kufika kutoa vitisho na kuna baadhi ya maeneo wameanza kuagiza mpaka kuwambia masheha kwamba Kamati zile za Maendeleo za Shehia wajumbe wanaotoka chama fulani watolewe.

Sasa leo suala la kukabiliana na maafa ni suala kubwa Mhe. Naibu Spika, tunapowakabidhi hawa kama nilivyosema mfumo wa utawala sina tatizo nao lakini tatizo linakuja *behavior* utendaji wao, kweli hapa utapata ushirikiano wa wananchi wote kuweza kukabiliana na maafa na yakija maafa hakuna vyama hapa, kuna suala la kwamba kuna tatizo katika nchi lishughulikiwe. Nilikuwa naomba maelezo kutokana na hoja hizo.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na maelezo hayo nasema nasita, sisemi kama naunga mkono Mswada wala naukataa. Kwa sababu ili niweze kuunga mkono au kuukataa natakiwa nijiridhishe juu ya maudhui yake, malengo yake kwamba ni Mswada Mzuri. Lakini kwa utaratibu wa serikali hii wa kuturipulia kazi nashinda kutamka hilo. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana.

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante Mhe. Ismail Jussa kwa mchango wako sasa nafasi tunampa Mhe. Suleiman Hemed na baadae Mhe. Mgeni Hassan Juma.

**Mhe. Suleiman Hemed:** Mhe. Naibu Spika, sina budi kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaali jioni hii tukawa pamoja hapa kwa kuzungumza mambo ambayo yanalihusu taifa letu.

Lakini la pili, nichukue nafasi hii ya kukushukuru wewe Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi japo kuwa ndogo ya kuweza kuchangia Mswada huu, japo kuwa Mswada huo umeshachangiwa kwa muda mrefu na takriban yalikwisha kuzungumzwa mengi ni yale yale na kasoro zile zile zinazotolewa. Lakini na mimi nitapita katika nyanja zangu nyengine pengine labda huenda tukapata faida ndani yake.

Mhe. Naibu Spika, mimi kitu cha mwanzo ambacho nataka nikujuilishe kwamba hii *tittle* ya Mswada ina matatizo, hii titel yenyewe ina matatizo, yaani haiko wazi hii title. Kwa sababu ukiisoma hii title kuna neno limeingia kati kati jambo ambalo neno hili lilioko katikati halijatoa picha halisi nini linakusudia mpaka uusome huu mswada kwa ndani ndio utakuta hilo neno lililotumika ndio utakuta hilo neno lilitumika ndio utakuta uko katikati linazungumza nini ambao ni kama imeparaganyika paraganyika hivi haikukaa sawasawa, tuusome mswada.

"Kuanzisha sheria ya kupunguza na kukabiliana na maafa Zanzibar".

Hili neno ninalozungumza mimi ni hili neno ambalo limeandikwa hapa "kupunguza" na hasa mswada unasema kuanzisha sheria ya kupunguza, sheria gani unayoisikia wewe ya kupunguza, umepata kusikia sheria ya kupunguza, hakuna sheria ya kupunguza. Sheria hii ni ya Mswada wa Maafa. Sasa ndani ya Mswada huu wa Maafa kutatoka mambo chungunzima ndani yake, lakini hili neno kupunguza lina maana yake litajitokeza huko katika maelezo lakini hapa katika title linakuwa halina maana yoyote.

Lakini mimi nitazidi kuendelea zaidi kwamba ingekuwa iwe sheria ya kukabiliana na maafa yanayojitokeza kwa ghafla na yale yanayotukabili katika *premises* zetu nitachambua yote hii. Yaani huu mswada ni mzuri si kwamba mswada ni mbaya lakini maelekezo ya mswada huu katika sheria kidogo yanahitaji kuwekwa sawa. Na katika hili yale ambayo maafa yanayotukabili kwa mfano yale maafa yanayotukabili katika *premises* zetu na yale maafa yanayotokea ghafla, kwa ghafla ni kwamba kwa mfano umetokezea moto hayo ni maafa ya ghafla. Imetokea meli

kuanguka au kuzama hayo ni maafa ya ghafla. Lakini kuna yale maafa yanayotukabili katika premises zetu, premises ni katika majengo yetu au majumba yetu kwa ufupi.

Sasa hapa panatakiwa uokozi katika majumba yetu. Lakini mimi nilifikiria kwamba huu mswada utajikita katika kujieleza mambo ya maafa ya ghafla na mambo ambayo yanayotutokezea katika majumba yetu. Kwa mfano katika majumba tunao umeme, mara nyingi katika majumba yetu inatokezea shot, sasa inapotokezea shot katika majumba ni masuala mengine yanayotokea katika majumba yetu katika *premises* zetu na ule moto ambao unaotokezea kwenye meli au moto unaotokezea sehemu mbali mbali.

Sasa hapa itakuwa unatumia neno kama ndege imeingia moto au meli imeingia moto ule ndio uokozi utakaokolewa yale yale majanga ya ghafla. Lakini katika kupunguza katika hilo hilo lililotajwa hapo litatumika kwenye majengo ya wananchi kwa kukinga na kupunguza maafa. Sasa lile neno ndio linaingia hapa kwa kupunguza maafa lakini sasa huko lilikotiwa lile neno halifai pale.

Kwa sababu sheria inasema kuanzisha sheria ya kupunguza, sheria gani uliyoisikia wewe ya kupunguza hakuna sheria ya kupunguza hebu iangaliwe ile title sawa sawa, title haiko safi. Kwa sababu hili neno limejitokeza katika kupunguza maafa ambayo katika wakati wa kukinga sasa pale kukinga tutakuja vipi, *'prevention is better than cure'* au sivyo kwa namna hii inatakiwa hapa Serikali ihakikishe kwamba majumba yote ya wananchi hali ya utiaji wa *fitting* za umeme ziko katika hali nzuri ile ndio katika kupunguza, maana yake ajali zisitokee katika majumba yetu.

Sasa hili neno hapa lilipoingia limeingia pabaya, hapo lilipoingia katika kupunguza haiwezekani sheria ya kupunguza. Katika kupunguza maafa wakati tuko katika majumba yetu umeme tumetia katika majumba yetu sasa inataka Serikali ihakikishe kwamba *fitting* ya majumba yetu yote yako katika *condition* nzuri. Sasa Serikali bado haijafanya suala hilo la kuhakikisha kwamba majumba yetu *fitting* zake ziko nzuri ili kupunguza hayo maafa, hili neno ndio ninalitumia hapa ili kupunguza hayo maafa hapa ndio pahala pake pa kuja neno hilo sio katika sheria.

Kwa hivyo, Mheshimiwa majumba tunayoishi ambayo ndio tunatia huo umeme na katika umeme huu tuna vifaa namna kwa namna, tuna *cooking utensil* vifaa vya kupikia, tuna mafriji, tuna mafriza kwa hivyo hapa katika majumba inaweza kutokezea maafa ghafla katika majumba yetu, sasa je hapa katika mswada huu haukueleza kwamba pia na hili litafatiliwa kwamba *fitting* za majumba yatafatiliwa kwa makini sana ili kuhakikisha ajali hii kwa sababu zote ni ajali. Ajali ya moto ni ajali, ajali ya ndege ni ajali ikianguka au ikipata moto, ajali ya majumba watu wakiumia na watoto wakiumia itakuwa zote ni ajali.

Kwa hivyo, iingie hapa katika kupunguza maafa. Kwa hivyo Serikali nataka kumuuliza Mhe. Waziri hapa katika suala hili ambao katika kupunguza maafa kuna utaratibu gani wa kuhakikisha katika mswada huu kwamba majengo ya wananchi yote *fitting* zao zimepitiwa na Serikali kuhakikishwa kwamba *fitting* zile hamtatokezea *shot* na hilo sidhani kama linafanywa, *checking* ya *fitting* na mambo ya umeme ambao uliomo mule ndani. Kwa sababu unatakiwa umeme ni ule *standard* utakaohakikisha kwamba umeme ule hautoleta maafa yoyote.

Halafu katika sehemu ya pili ya majengo ni yale majengo ambayo yaliyokuwa katika mahoteli. Majengo yaliyoko katika hoteli ni lazima majengo yale kwa sababu kuna watu, kuna binaadamu wanaishi katika majengo yale wahakikishe kwamba umeme ulioko katikia majengo yale uko standard hauna matatizo, hautotuleta athari ya kuripuka moto ule ukaanguza watu. Kwa hivyo, katika mambo ya ghafla tukichunguza Unguja hapa maeneo mengi katika majumba yetu au katika maofisi yetu au katika mahoteli, kitu cha msingi na kuwa na *fire extinguishers.* Mheshimiwa *fire extinguishers* ni maneno tu yaliyopo, *fire extinguishers* hata wakipewa watu wakiambiwa wazitumie zile *fire extinguisher* watu hawazijui kwa sababu hakuna elimu ambayo iliyotolewa.

Kwa hivyo, katika majengo ya hoteli ni pahala ambapo pengine kunaweza kukatokezea maafa ya moto pengine utaalamu wa kuzima ule moto haupo, pengine *fire extinguisher* imeshapitwa na wakati, pengine watendaji wanaoshughulikia ile hawajui namna ya *execute* kuitekeleza ile kazi. Kwa hivyo hilo ni moja.

Lakini la pili, katika majumba yetu ambayo tunahitaji katika mswada huu haukueleza kwamba katika majumba yetu ya kisasa tuhakikishe kwamba tuna ngazi kama ni moja ni ya *lift* ya umeme au ngazi ambao ni moja ikitokezea umeme uweze kupita pahala pengine. Kwa mfano jumba la ghorofa kubwa, ghorofa tano au ghorofa sita umeme umo ndani umepata *shot* ghorofa ya tatu katika sita uko kati kati, je tutafanya nini, tutakwenda wapi walio juu kuteremka chini hawawezi na walio katikati hawawezi kutoka na walioko chini wanahaha.

Sasa kwa namna hapa kunahitaji kuwepo ngazi ama itakuwa ya umeme ambayo watu wanateremkia katika majengo yetu ya kisasa au pawe na ngazi nyengine moja au mbili ikikosekana ngazi hii ipatikane ngazi nyengine, hata katika mswada haukueleza vile vile kuonesha namna gani tutapunguza ajali zinazotokezea kwa moto kwa njia ya umeme.

Halafu Mheshimiwa tukenda katika ngazi nyengine ambayo ni ngazi ya vyombo tunazosafiria pwani, Mhe. Naibu Spika, meli zetu tulizonazo hazijafikia kiwango ambacho tunaziona sisi kwa sababu maafa katika meli yanatokezea kila siku. Na tuangalie kipindi hiki tulichochukua tumepata maafa namna kwa namna, tumepata meli zimezama pale penye bandari, meli iko bandarini inazama pale pale uokozi wake ulikuwa ni mgumu sana, vifaa vingi vilipotea na roho za watu zilipotea tena kwenye bandari sikwambii ile ambayo itakuwa iko nje. Sasa mimi ningefikria hapa kwamba Serikali lazima ijikite katika masuala ya kuangalia na kuchunguza meli zetu kuwa meli zetu ni meli za uhakika. Kwanza meli zina umri gani, pili kuangalia mashine za meli zenyewe kwamba pengine inaweza mashine zimechoka ni za muda mrefu zinaleta matatizo wakati wa kusafiri.

Tatu kuhakikisha *capacity* uwezo wa ile meli kwa sababu kwenye meli mambo mengi yanaweza kujitokeza, kama mashine ni mbovu katika meli inaweza ikatokea hata *shot* katika mashine zile za umeme na watu waliomo ndani wakaathirika na wengine wakajitupa kwenye bahari. Kwa hivyo ni lazima Serikali ihakikishe wale wahusika kwenye bodi waangalie kwamba meli zetu ni nzima mashine *fitting* zake za umeme, AC yake ziko sawa na *capacity* ya ile meli inakwenda kwa mujibu wa ile meli yenyewe, lakini matatizo tuliyonayo hivi sasa mameli yetu mengi ni mabovu hayafiki safari na yanayokwenda bila kuangalia mazingira ya nchi hii.

Waheshimiwa nchi yetu imezungukwa na bahari na ndani ya bahari hii kuna maji ya kawaida na kuna maji ambayo si ya kawaida maji ya mkondo, meli zinapita katika maji ya mkondo mkubwa sana na meli hizi zinapata msukosuko mkubwa sana, nyengine zinahimili, nyengine zinarudi njiani. Sasa ni vyema Serikali ikaangalia mazingira, *environment* yetu ya kibahari iko vipi aina gani ya meli ambayo sisi zitatuvaa. Meli zetu ambazo zinazokwenda kwenye *speed boat* nyingi zimerudi njiani, zinakwenda mpaka kwenye mkondo wa maji mengi upepo umekuwa mkubwa meli zinarudi nyumbani.

Kwa hivyo, mimi ningefikiria kwamba Serikali ingeangalia kama usafiri wa kutoka Unguja kwenda Pemba au wasafiri kutoka Unguja kwenda Dar es Salaam ni meli ambazo zimepewa uhakika zina uwezo wa kupambana na mawimbi ya bahari zaidi ya mara mbili au mara tatu meli zetu zimeshindwa kuweza kutoka kule kuja huku. Kwa hivyo mambo mengi yanaweza kutokezea, meli inaweza ikazama, meli inaweza ikapata moto kwa kutokuchunguzwa uhalali wa meli ile na ubora wa meli ile. Kwa hivyo Mheshimiwa tuna mengi ya kuangalia vile vile pamoja na *capacity* ambayo sasa hivi pengine watu wana *over load*.

Mheshimiwa baada ya hilo tuangalie hali ya hewa ambayo tuliyonayo katika nchi yetu sisi labda pengine hapa Zanzibar tunayo ile *weather focus meteorological department* ambayo ya kuangalia hali ya hewa. Meli hizi zetu kwa kunusuru ajali za ndani ya meli taarifa hazitoki za usahihi, itakuwaje meli zitoke zinakwenda mpaka kufika kati kati zirudi, hii *weather focus meteorological department* iko wapi kuwaruhusu watu hawa kuweza kuondoa meli, matokeo yake ajali zinatokezea njiani nani atajibu hoja ile ya meli kuzama, nani atajibu hoja ya meli kupata athari ya kuungua, nani atakaejibu. Kwa hivyo kuna mambo mengi ya kuzingatia katika mswada huu ambao mswada huu lazima uboreshwe ufanywe tena vyengine upitiwe kwa kuangaliwa uhalali wa meli zetu tunazoondoka nazo.

Mhe. Naibu Spika, katika ajali nyengine ambayo inaweza kutokezea, mtetemeko wa ardhi hii imewahi kutokezea mara nyingi mtetemeko wa ardhi ingawa si mkubwa sana unaanzia huko Indonesia unakuja mpaka Zanzibar East Africa, East Africa yote iko katika milima ile ya Kilimanjaro lazima kuna *earthquake* na nini unakuwepo na mtetemeko wa ardhi. Kwa hivyo na Zanzibar ni sehemu ya Zanzibar ya pwani unapatikana mtetemeko wa ardhi, gani Mhe. Waziri katika suala la mtetemeko wa ardhi kiasi gani hatua zake katika mswada huu utachukua haikuelezwa inapotokezea mteremeko wa ardhi.

Hilo ni janga na tunasema yote ni majanga ya kitaifa yanaweza kutokezea wakati wowote. Mtetemeko wa ardhi au mporomoko wa ardhi hapa kiasi Wizara itakuwa imejikita kwenye suala hili. Mheshimiwa Sunami inapotokezea au upepo mkubwa unapotokezea au kudidimia kwa ardhi hapa Zanzibar ishawahi kutokezea kudidimia kwa ardhi na nyumba yote kuzama mpaka chini haikuonekana.

Sasa haya ni mambo mswada huu, mswada huu ni mkubwa, mswada huu una mambo mengi ya kuzingatia na inataka uhalali wa kuzingatia mambo haya. Ardhi imeshadididimia, kimbunga kishawahi kutokezea tumeona pepo

zilivyo kali mapaa ya nyumba yanatolewa haya ni mambo ya *consider* na tuwe *very serious* katika hili jambo. Kama kweli mswada huu kuwasaidia na kuwalinda wananchi ni lazima tuuangalie sehemu zote ambazo tunahakikisha ajali zinaweza zikatokezea. Kwa hivyo kudidimia kwa ardhi hayo yamefanyika Zanzibar, Kimbunga kishawahi kutokezea Zanzibar, majengo kuanguka chini imeshawahi kutokezea Zanzibar, ajali zinazopatikana katika viwanda hakuna mtu anayeangalia ajali ambazo zinazotokezea watu wanashughulika na viwanda vikubwa vikubwa, mambo mengi yanaweza kutokezea katika kiwanda, mswada huu hakuongelea yote.

Sasa katika hayo yote kitu gani ambacho sisi kitatusaidia, nikikumbuka mambo ambayo yaliyotokezea hapa ajali mbali mbali za meli na mambo mengine tuangalie jinsi gani serikali mwanzo ukasema suala hili ni majanga ya kitaifa, kama ni majanga ya kitaifa Serikali imejipanga kiasi gani katika suala hilo. Kwa sababu kipindi kilichopita katika ajali hizi hakuna kifungu cha fedha ambacho kilichowekwa kwa ajili ya ajali ambazo zitatokezea Zanzibar ni pale ambapo ajali ikitokezea inabidi afatwe Waziri wa Fedha kuweza kutusaidia kipindi kile. Hiyo sio sahihi kama kweli tunataka kusaidia maafa ya Zanzibar kwa njia mbali mbali itakayotokezea hatuna budi tuna kifungu au tuna mfuko *special* kwa ajili ya Zanzibar sio tusubiri maafa yakitokezea ndio tukatafute pesa hiyo haiwezekani. Kwa hivyo bajeti zetu zote tuhakikishe kwamba bajeti zetu ziko sawasawa.

Mhe. Naibu Spika, katika masuala ambayo ya ajali katika utoaji wa taarifa za ajali, katika kutoa taarifa za ajali mara nyingi taarifa nyengine zinakuwa za uongo si za uhakika na halafu elimu lazima itolewe, ni mahala gani ambapo wewe mwananchi unaweza kutoa taarifa ya ajali unampelekea nani, unampelekea Polisi, unampelekea JKU unampelekea KMKM au pahala gani mwananchi ajue apeleke taarifa zake tu ikitokezea ajali. Na hizi ajali zinapotokezea mara nyengine zinakuwa ajali za uongo. Kwa hivyo ni lazima tuhakikishe kwamba kila kitu kipo sawa sawa.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine ambalo nataka nilizungumze ni suala zima la kuundwa kwa hii Kamisheni mimi naamini Kamisheni hii kwa sababu hili ni janga la kitaifa waliotiwa katika kuundwa Kamisheni hii ni sahihi ila tu kuna baadhi ya wengine wanahitaji kupunguzwa. Kwa sababu mimi nina wasiwasi wa kitu kimoja. Kuna baadhi ya mambo mengine wanakutana mawaziri wengi kufanya kazi kitu kimoja, lakini utakuta kuna *total failure* wanapokutana Makatibu Wakuu ama Waziri saa nyengine kuna *total failure* na hii nina wasiwasi kwa sababu watu wamekuwa wengi sana mpaka mawaziri wote wanakuwemo na kila mtu anakuwemo. Hawa mawaziri *they have got a lot of work,* wana kazi nyingi sana sidhani wataweza kulifikiria suala hilo tunahitaji watu watatu labda baada ya kamati kubwa ile iweze kuchaguliwa kamati nyengine ndogo ya kuweza kufikiria mambo ambavyo kwenye *suprise* yakitokezea ghafla ghafla.

Lakini kwa hali ya kamati hii ambayo ni Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa kuna wajumbe wa Kamisheni, uwezo wa Kamisheni wote wana uwezo hao kwa sababu wote ni wakubwa. Na tunajua hapa kuna Mkurugenzi Mtendaji ambaye anayeshughulikia mambo haya, kuna vitengo mbali mbali vya Kamisheni ambao hawa kazi yao ni kutoa mawasiliano ya kiutendaji. Kwa hivyo maafa yanapotokezea kwa ngazi mbali mbali ikiwa ngazi ya sekta au ngazi ya Wilaya au ngazi ya taifa wanaweza wakatoa ripoti. Lakini kwa sababu hili suala liko hapa Unguja mjini angalia huko upande wa pili mambo haya yanapokuwa yanatokezea kuna ukweli wa kiasi gani Wilaya zetu au sehemu zetu zilizobakia za Mkoa na Wilaya haya masuala wanayafatilia.

Na hao waliopewa dhamana kufatilia hii maafa yakitokezea, yana utaratibu gani je kuna watu maalum ambao watakaopangwa kuangalia maafa yakitokezea na kuweza kuripoti katika Wilaya au katika Mkoa. Mimi ninafikiri mara nyingi ajali zinatokezea mbali mbali, hata ajali za moto za mtoto kuungua katika nyumba pia ni ajali ya moto, zote hizo ni ajali. Kwa hivyo mimi ninafikiri tunahitaji kujipanga vizuri ili tuweze kuhakikisha kwamba tunafanikiwa ili kuweza kukabiliana na maafa yote.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, huu moto unaweza ukatokezea kwa upande wa raia, huu moto unaweza ukatokezea katika maofisi yetu ya Serikali, huu moto unaweza kutokezea katika misitu yetu tuliyonayo, tunayo ngezi *forest* pale mara nyingi ishaungua ngezi *forest*, lakini angalia mwahala kama humu gari inawekwa Chake Chake au gari inawekwa Wete Mjini ni muda gani hata ikafika kule kwenye Msitu wa Ngezi ambao kule ndio kwenye uhai wa Kaskazini kwa sababu ndiko kwenye msitu, angalia gari iko Wete msitu uko Konde njia ya Makangale. Wakati gani gari hii itafika kwa wakati ili kwenda kunusuru maafa ya moto katika msitu ule?

Kwa hivyo, haya ni mambo ninayasema makusudi kwamba ajali zinapotokea kwa raia ndani ya majumba, au ajali zinaweza kutokea katika ofisi za serikali au ajali zinaweza kutokea katika msitu wetu, au ajali zinaweza kutokea

kwa watoto ambao walioko katika majumba kuungua kwa moto kwenye nguo zao, au ajali nyingine ni hizo za vyombo vya usafiri. Lakini sasa cha msingi hili suala linahitaji fedha ya kutosha haya majanga ni makubwa na *financial position* ya nchi yetu ni ndogo, uwezo wa kutekeleza wa kuweza kuwapatia nyenzo waokoaji hii ni kazi kubwa sana, sijui Mhe. Waziri katika hili atalipanga kiasi gani, bajeti yake katika kuokoa maafa ya kimataifa sijui bajeti yake itakuwa kiasi gani? Kwa hivyo, hili nilitaka kulijua vile kwa Mhe. Waziri hili suala ni suala la msingi hapa hatuzungumzi kwa sababu tunapiga maneno ya lele mama, hatuuzi maneno hapa.

Hapa tunazungumza mambo ambayo ni kwa ajili ya faida ya nchi hii, sasa kama tuko *serious* katika suala la kuokoa maafa ya watu wetu *we have to be serious, how much money* tutakuwa nazo kiasi gani ambazo zitakuwa *allocated* katika Wizara ya Fedha ili kuweza kutoa huduma. Hii ni huduma ambayo serikali ndio itaweza kutoa huduma hii, wananchi wanaweza kusaidia katika kuokoa huduma kama nyumba imeingia moto wanaweza kusaidia kutoa vyombo, kutoa vitu vyingine ndio kazi ya wananchi. Lakini kwa upande wa serikali cha msingi ni kuhakikisha *financial position* fedha, bajeti yetu iwe bajeti nzuri sana, kwa sababu mfuko wa maafa mimi sifikirii kwamba mfuko wa maafa tungojee maafa yatokezee halafu tumfuatie Waziri wa Fedha atwambie sasa hivi njooni mchukue fedha, hiyo haiwezekani. Fedha iwepo tayari tayari ikitokezea janga pale pale inasaidia.

Mhe. Naibu Spika, ninachokifikiria kingine zaidi ni kwamba hizi ajali ni nyingi sana na tunahitaji kutoa elimu kwa watu wetu lazima kitu cha mwanzo ni kutoa elimu watu wote waelewe aina zote za majanga, na vipi kwa upande wao watatoa mchango wao kwa maafa yale na upande wa serikali. Sasa naomba tu kwamba hizi kamati ambazo zilizokuwa zimechaguliwa na nimeshauri kwamba papatikane kamati nyingine ndogo hii itakuwa ina-*high speed* ya kufuatilia mambo.

Kwa sababu haiwezekani wakati ule kama Makamu wa Pili wa Rais ambaye ni Mwenyekiti na wengine wakafatilia lile suala kwa ghafla, hivyo haiwezekani wao watapewa taarifa. Lakini sasa lazima wapatikane wachachagizi wa kulichachagia hili suala haraka haraka ili kulifikisha kwa Makamu wa Pili wa Rais kama ndiye Mwenyekiti, sio wao tena wakafuatilia mambo haiwezekani yeye Makamu wa Pili wa Rais akafutilie mambo hayo, haiwezekani. Yeye anaangalia kama Mwenyekiti likitokezea jambo lolote atafanya vipi, atasaidia vipi, ataongoza vipi lakini ni lazima wapatikane watu wa kuweza kuliokoa hili jahazi.

Kwa hivyo, kwa sababu sisi ni watu ambao tumezungukwa na bahari maafa haya ni mengi sana kutokezea. Kwa hivyo, *let guess* zaidi wakati wowote linaweza kutokezea si jambo la halafu kwa sababu nchi yetu imezungukwa na bahari ajali zinaweza kutokezea wakati wowote, Mwenyezi Mungu atuepushie mbali na ajali hizo.

Mhe. Naibu Spikaa, nafikiri nimezungumza kwa kirefu sana na mimi kwa kunipatia nafasi hiyo ya mchango wangu. Ahsante nakushukuru.

**Mhe. Mgeni Hassan Juma:** Mhe. Naibu Spika, kwanza nichukue fursa hii adhibu nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi na mimi yakuweza kuchangia katika Mswada wetu huu wa Kuanzishwa kwa Kamisheni ya Maafa.

Mhe. Naibu Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma, *jallah wajallall* ambaye ametupa uwezo wa kuja hapa leo kwa ajili ya kufanya shughuli zetu za kawaida.

Mhe. Naibu Spika, vile vile nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri kwa kweli kutuletea mswada huu, mswada ambao kwa muda mrefu tumekuwa tukiusubiri kwa hamu, kwa sababu sisi Zanzibar tunaishi katika dunia ambayo dunia hii tunaona mambo mbali mbali yanatokea hususan masuala ya maafa na kwamba na sisi vile vile tumo ndani ya dunia hii. Sisi sio kisiwa kilichojitenga peke yake ambacho kitakuwa hakipati maafa mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitakwenda moja kwa moja katika mswada huu, nianze tu katika kifungu cha 4 ambacho kinazungumzia suala zima la muundo wa Kamisheni. Mhe. Naibu Spika, mimi nitaungana na wenzangu kwa kuwa na hofu ya wingi wa Wajumbe waliokuwemo ndani ya Kamisheni hii. Sina tatizo na kuwepo kwa Mwenyekiti wala Makamu Mwenyekiti, lakini Mhe. Naibu Spika, nimeona Kamisheni hii na nikapiga hesabu ina wajumbe 28.

Mhe. Naibu Spika, na mimi nilikuwa nataka nijue ni vikao vingapi hasa Kamisheni hii itakuwa inavikaa kwa kipindi cha mwaka mmoja. Na nasema hivyo kwa sababu nikitizama jopo la wataalamu, jopo la Wajumbe wa Kamisheni hii ni jopo kubwa. Mhe. Naibu Spika, gharama ya kuendesha vikao tunaifahamu, lakini ingekuwa vikao hivi vitafanywa labda mara moja kwa mwaka au pale yanapotokea maafa mimi sina tatizo. Lakini nikitizama kwamba kwa kawaida

ya Kamisheni zinakuwa na mfumo wake wa kufanya vikao, na mara nyingi sana vikao vile vinakuwa havipungui zaidi ya vikao vinne katika mwaka, na nikitizama fedha ambazo zitatumika katika mambo mbali mbali ikiwemo malipo ya posho Mhe. Naibu Spika kidogo napata ukakasi. Wajumbe nawaona ni wengi na kwa kweli tuangalie *value for money*. Kwa hiyo, Mhe. Naibu Spika ningemuomba sana waziri aje hapa atueleze hili jopo hasa hawa mawaziri wote, hawa wengine sina matatizo nao lakini hawa mawaziri wote ambao wamo ndani ya Kamisheni hii kwa kweli inanitia wasi wasi mkubwa.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitakwenda katika kifungu cha 6 ambacho kinazungumzia uwezo wa Kamisheni. Katika kupitia vifungu mbali mbali ambavyo vimejieleza humu ndani ya mswada nimeona kwamba Kamisheni haijapewa uwezo wa kutoa taarifa pamoja na elimu inayohusiana na maafa. Sasa najiuliza je Kamisheni haina uwezo huo au kwa nini Kamisheni nayo isipewe uwezo huo wa kuweza kutoa taarifa.

Mhe. Naibu Spika, nitakwenda katika ukurasa wa 304. Mhe. Naibu Spika, katika ukurasa wa 304 katika ibara ya 10 inayozungumzia suala zima la sekretarieti na kazi zake, katika cha (a) inazungumzia suala zima la kuandaa na kufanya utetezi na kujenga uwezo katika ngazi zote ili kujiandaa, kukabiliana na kurejesha hali baada ya maafa.

Mhe. Naibu Spika, ningekuwa mimi hili suala la kujiandaa kukabiliana lingekuwa ni moja ingeingia katika kifungu kimoja, na suala la kurejesha hali baada ya maafa lingekuwa ni suala jengine. Nina hofu kwamba haya mambo huwezi kuyachanganya japokuwa ni suala ambalo linazungumzia maafa, lakini bado ni vitu viwili tofauti. Na kama ni kazi watakayopewa sekretarieti, sekretarieti wanaweza kujigawa katika makundi mawili moja ikashughulikia suala la kukabiliana na jengine likashughulikia suala la baada ya kurejesha hali baada ya maafa. Kwa hiyo, labda watakuja kutueleza kwa nini imewekwa katika sentensi moja.

Mhe. Naibu Spika, lakini vile vile nilikuwa nimeona kuna umuhimu vile vile kwa sababu huku kwenye Kamisheni wamepewa kazi ya kuweza kuhakikisha kuwa sera za serikali, sheria, mipango na kazi za kukabiliana na maafa zinaendana na makubaliano na mikataba ya kikanda na ya kimataifa ya kukabiliana na maafa. Lakini katika kazi ya sekretarieti ambapo sekretarieti hii itafanya kazi pamoja na Kamisheni. Kwa hiyo, katika kazi ya sekretarieti jukumu hili wao hawajapewa. Kwa hiyo, vile vile kungekuwa sekretari ipewe kazi ya kusimamia utekelezaji wa mikataba na makubaliano ya kikanda inaweza kusimamia na kuratibu utekelezaji wa mikataba ya makubaliano ya kikanda na ya Kimataifa ya kukabaliana na maafa. Naona hilo halikujitokeza katika kazi za sekretarieti ambalo lina umuhimu mkubwa, na hasa kwa sababu Kamisheni itakuwa na kazi hiyo.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ni ibara ya 11 ambayo inahusiana na Kamati ya Kitaalamu. Mhe. Naibu Spika, katika kifungu cha 11, ibara ndogo ya (2) inazungumzia katika kifungu (k) wajumbe watatu wa kuteuliwa na waziri kutoka katika Jumuiya zisizo za Serikali, Jumuiya za Kijamii na Taasisi.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilikuwa nashauri kwamba uteuzi wa watu hawa ambao wanatoka katika asasi zisizo za kiserikali ufanywe na wenyewe. Mhe. Naibu Spika, hili ni muhimu sana kwa sababu tunafahamu asasi hizi huwa zina *umbrella* zao, na wao wenyewe wanafahamiana nani mtu ambaye anaweza kuwawakilisha. Kwa hiyo, ningependa zaidi au ningeshauri kwamba kwa kweli kwa upande wa kutafuta watu wanaotokana na asasi za kiraia, basi uteuzi huo ufanywe na wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, la mwisho kabisa ni katika kifungu cha 14 cha ibara ya 2 (k) inazungumzia mwakilishi kutoka Jumuiya za Kiraia. Mhe. Naibu Spika, vile vile hapa ingelizungumzia sana suala la kuwahusisha Asasi za Kiraia.

Mhe. Naibu Spika, idadi ya mtu mmoja kwa kweli ni kidogo sana hususan kwa sababu tunajua mambo mengi ambayo yanafanywa ndani ya jamii yetu, elimu pamoja na mengine mengi na Asasi za Kiraia zinafanya kazi hiyo kubwa sana. Mimi ningeshauri badala ya kuwa nafasi moja basi tuwape nafasi mbili, na kwa sababu mara nyingi Asasi za Kiraia ndio ambazo zinatembea katika maeneo mbali mbali. Miradi yao mingi inakwenda moja kwa moja kwenye jamii, na uelewa wao wa kuifahamu jamii ni mkubwa sana. Kwa hiyo, katika kamati hii ingekuwa vizuri zaidi tukapata angalau basi wawili kutoka katika Jumuiya za Kiraia.

Mhe. Naibu Spika, lakini ambalo nitalizungumza la mwisho kabisa lakini sio kwa umuhimu isipokuwa nalizungumza kwa sababu limejitokeza ndani ya mswada huu. Mhe. Naibu Spika, tangu mwanzo katika kamati tumeona kuna wajumbe ambao nafikiri wajumbe watakaotengeneza Kamisheni watakuwa ni 28. Lakini Mhe. Naibu Spika, kati ya hao 24 ni wa nne tu ndio wanawake wanaingia katika nafasi hii kwa sababu ni mawaziri. Lakini

ukitizama nafasi nyingine zote katika Kamisheni utagundua kwamba hawa ni akina baba, tunakubali mbele tunakokwenda pengine kutakuwa na mabadiliko lakini tuone hali hii sasa hivi, tuione hali hii na tukubali kwamba umefika wakati tuanze kuwafikiria kina mama kwa sababu na wao ni sehemu kubwa ya jamii hii. Tunapokuwa tunawaweka kina mama katika ncha tunakosea pahala pakubwa. Kwa hiyo, Mhe. Naibu Spika, inasema hivyo kwa sababu Kamisheni itakuwa ina wajumbe wanne wanawake kati ya ishirini na nane, sio vizuri.

Mhe. Naibu Spika, kamati, sekretarieti sijajua wajumbe wake watakuwa ni wangapi na jinsi itakavyogawanya ni vipi. Lakini katika kamati vile vile tukiangalia kutakuwa na kamati ambayo itakuwa na Makatibu Wakuu hofu yangu ni kwamba idadi ya wanawake itakuwa ndogo.

Mhe. Naibu Spika, ukitizama katika kamati ambazo zitakuwa za Wilaya nina hakika kutokana na nafasi hizi ambazo zimewekwa, nafasi ya wanawake itakuwa ndogo. Mhe. Naibu Spika, nasema hivyo nataka tu kwamba kusema muone namna tunapofanya uteuzi mbali mbali matokeo yake ni haya bila ya kuangalia jinsi, haya ndio matokeo yake. Serikali ipo inanisikia ningeomba kwa niaba ya kina mama zinapotokea nafasi tuwe makini sana katika kuangalia na ku-*balance* jinsia zote, wanawake wanataka kulijenga Taifa lao. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi. (*Makofi*)

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Naibu Spika, na mimi nachukua nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na uzima na tumeingia kwenye mwaka mpya wa 2015 tukiwa bila shaka na ari kubwa ya kujenga nchi yetu kuelekea uchaguzi mkuu wa 2015.

Mhe. Naibu Spika, na mimi nikiri kwamba mswada huu sijaupitia kwa sababu ya uharaka wake, maana yake umekuwa haraka serikalini, pia umekuwa haraka katika mikono ya wawakilishi. Kwa hiyo, nitazungumza mambo machache sana kwa jumla jumla ili nitoe tahadhari kwa serikali pale watakapoamua wenyewe mswada huu kupitisha basi wawe na *point* ambazo tumewasaidia kwa jumla.

Mhe. Naibu Spika, suala la maafa ni suala la kidunia na ni suala ambalo linahitaji sana mchango wa wataalamu. Maafa watafautishe sana na mwelekeo wa kielimu, na mwelekeo wa suala la afya, na mwelekeo wa suala la ajira. Maafa ni fani moja muhimu ambayo dunia na nchi husika ingejipanga ili kujiweka tayari na suala zima la maafa, iwe yale ya kimaumbile au yale ambayo wanadamu wanaweza wakasababisha.

Kwa hiyo, suala hili Mhe. Naibu Spika, si suala la kuangalia kwa juu juu kama ambavyo nchi yetu imekuwa, nikiangalia kwa juu juu kama ambavyo nchi yetu imekuwa ikiangalia mambo kijuu juu, Wawakilishi wanadhani kwamba mswada huu ungelingana na ule mswada pengine wa kawaida ambao unahusu sheria za kawaida. Mswada huu ni muhimu sana pindipo serikali wangekuwa na umakini wa kuliangalia suala la maafa kama suala la kidunia.

Mhe. Naibu Spika, tunapoangalia suala zima la mswada huu mambo ya kuzingatia lazima yapewe kipaumbele kwanza suala zima la wataalamu.

Mhe. Naibu Spika, leo nchi yetu imeamua kupitisha mswada huu au kufuta sheria ya mwaka 2003 ili kuleta mswada ambao utakwenda na wakati, lakini nchi imesahau kwamba suala la maafa linazingatia sana mchango wa wataalamu. Nina ushahidi wa hili, ukiangalia hizi kamati za wataalamu kuanzia taifa hadi shehia, niigusie ile ya shehia. Wataalamu wake mule ni Katibu wa Shehia, Masheha, Wawakilishi na Baraza la Masheha, ndio hao wanaotegemewa kupanga mipango ya kujikinga na kukabiliana na maafa katika shehia. Kwa hivyo, serikali hili jambo wasilifanye kama suala la kawaida ni suala ambalo linahitaji mchango mkubwa wa wataalamu ambao nchi za wenzetu duniani huwekewa fedha nyingi kwa ajili ya kuandaa wataalamu wanaokabiliana na suala hili.

Mhe. Naibu Spika, kwa bahati mbaya sana kwa Zanzibar hadi hii leo hatujaona umuhimu wa kusomesha wataalamu wa kukabiliana na maafa ili kugundua majanga na mbinu za kukabiliana nayo kwa ajili ya kuwaokoa watu wetu. Kwa hiyo, bado nchi yetu inaona kwamba suala hili la maafa ni suala la kawaida na ndio maana sasa leo mswada unakuja haraka haraka hivi hatujapata mchango wa wataalamu. Leo Wawakilishi wanataka kupitisha sheria ambayo nina hakika sio miaka ya mbele hata kesho itakuwa na athari kubwa kwa wananchi wetu ikiwa hatukuwa makini kwenye kupitisha sheria hii.

Mhe. Naibu Spika, mimi nashauri, Mhe. Waziri akiona kuna haja baada ya mswada huu leo kuchangiwa *weekend* hii ya Jumamosi na Jumapili basi urejeshwe kwenye kamati ili kamati iwaite wataalamu na wadau mbali mbali angalau

wapatiwe *point* muhimu kwa ajili ya kurekebisha mswada huu, vyenginevyo kwa kuachiwa sisi hapa tulipo suala hili nyeti la maafa na tukapitisha kama hivi ambavyo mswada umeletwa, nahisi kwamba hatuwafanyii haki wananchi wetu na bila shaka fani hii ya maafa itakuwa imekwenda kombo mno. Namshauri Mhe. Waziri azingatie umuhimu wa mswada huu kuurejesha kwenye kamati Jumamosi na Jumapili ili waitwe wataalamu wa masuala mazima ya maafa ili waweze kutusaidia mchango. Hii ni kwa manufaa ya Baraza hili na ni kwa manufaa ya nchi yetu na wananchi wake kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, jambo la mwanzo ambalo ningependa lizingatiwe kwenye mswada huu mbali ya kuwepo kwa Kamisheni mbali mbali na kamati, lakini lazima pawepo na kituo maalum cha kukusanyia taarifa na utafiti wa maafa. Serikali iweke kituo maalum kwa ajili ya kupokea taarifa za maafa na taasisi mbali mbali kwa ajili ya taarifa hizo, badala ya kuwaachia Kamisheni na ofisi za serikali kuwa na taarifa kwenye mafaili yake.

Mhe. Naibu Spika, umuhimu wa kituo hiki ni kwamba kutakuwa na mitambo ambayo ina taarifa muhimu kwa ajili ya kuweka kumbukumbu mbali mbali za matukio ya kimaumbile na matukio ya kibinadamu, ili kuwezesha hata utafiti ukifanywa basi uweze kuwa katika kituo maalum kwa ajili ya kupata taarifa ya kimaafa. Kwa hiyo ningeshauri kwamba serikali itoe msaada huu waongeze kifungu maalum kwa ajili ya kuweka kituo maalum cha kukusanyia taarifa za utafiti kuhusu masuala ya maafa yale ya kimaumbile na yale ya kibinadamu, ili wananchi wa Zanzibar na wataalamu mbali mbali wanapohitaji taarifa za nyuma za hali ya mazingira, hali ya tabia nchi na mambo mengine basi waweze kupata taarifa hizo ili iwe rahisi kwa wataalamu wetu kuweza kuzifanyia kazi.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri akikubaliana na hilo naomba basi mswada huu uwe na kifungu maalum kwa ajili ya kuweka kifungu cha kuanzisha ofisi maalum ya kukusanyia taarifa za kimaafa na utafiti juu ya taarifa za kimaafa.

Mhe. Naibu Spika, jengine ningeshauri kwamba Kamati za Wataalamu ziwe kweli ni Kamati za Wataalamu na tuache yale mazowea kwamba kila mtu anafaa kuwa mwana kamati, ziko kamati kila mtu anafaa kuwa mwanakamati lakini ziko kamati lazima kweli tupate wataalamu. Ningeshauri kwamba kamati zote za wataalamu basi ziwe za wataalamu kweli na tuache yale mazowea kwamba kila mtu awe mwanakamati. Kila mtu awe na nafasi kwenye nchi hii, lazima wataalamu wawe wakweli wataalamu kwa ajili ya kuwezesha kazi ya utafiti wa masuala ya majanga yaweze kuwa na ufanisi mkubwa.

Mhe. Naibu Spika, jengine ambalo ningeshauri ni serikali kupitia mswada huu kuwe na Mfuko maalum kama ambavyo tumekubaliana, Mfuko maalum wa kushughulikia suala la maafa. Suala la maafa halitegemei *ceiling*, huwezi kuwa na lengo la kukabiliana na maafa ukategemea na *ceiling* ya serikali lazima kuwe na Mfuko maalum kwa ajili ya kukabiliana na maafa yakitokezea fedha ipo, yasipotokezea fedha inabakia kwa ajili ya kusubiri mipango mingine ambayo hatujui kesho wala keshokutwa.

Kwa hiyo, suala hili la maafa nadhani si suala la kutegemea *ceiling* ya serikali kuwe na Mfuko maalum kwa ajili ya kujiweka tayari wakati wowote ambapo maafa yanaweza kutokea, yale ya kimaumbile na yale ambayo binadamu anaweza akasababisha kwa njia moja au nyengine.

Mhe. Naibu Spika, nitoe mfano mmoja. Kuna Mfalme mmoja wa Misri aliota ndoto kwamba kwenye usingizi wake aliona kuna ng'ombe saba wanene wanaliwa na ng'ombe saba wembamba, akaota kwamba kuna mashuke saba ya nafaka yaliyopea yanaangamizwa na mashuke saba ya nafaka ambayo yamedumaa. Baada ya kuwapelekea wafuasi wake ndoto ile ikateguliwa na Nabii Yussuf kwamba ng'ombe saba hawa wanene wanaoliwa na ng'ombe dhaifu saba, maana yake kuna miaka saba ya neema na miaka saba inakuja ya maafa au njaa. Kwa hivyo, watu wakaombwa wajitayarishe hii miaka saba ya neema wajitayarishe kwa ajili ya kukabiliana na miaka saba ya maafa.

Mhe. Naibu Spika, huo ni utabiri kwa hivyo bila ya kuwa na nyezo za utabiri hatuwezi kukabiliana na maafa. Leo nchi yetu imezidiwa hata na ndege anayeitwa Kwarara, Kwarara akilia watu wote wanajua kwamba kuna mvua inakuja, lakini Zanzibar hatujui hata kutabiri mdudu wa embe. Nchi nzima hii inazidiwa na ndege Kwarara, Zanzibar hatujui utabiri wa embe na wadudu wake, Zanzibar hatujui utabiri wa maradhi ya Manjano, Zanzibar hatujui chochote lakini sheria inakuja ya kukabiliana na maafa.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo bila ya kuwa na wataalamu wa fani hii hatuwezi kukabiliana na maafa wala wananchi wasidanganywe, huwezi kukabiliana na maafa wakati huna wataalamu ndani ya nchi unategemea taarifa uzipate kwa nchi nyengine.

`Mhe. Naibu Spika, nashauri kwamba serikali iwekeze fedha maalum kwa ajili ya kusomesha wataalamu kwenye fani hii ya masuala ya maafa badala ya kutafuta taarifa za maafa kutoka kwa watu mbali mbali. Nadhani ni busara sasa kuwekeza fedha maalum kwa ajili ya kuweka katika mitaala yetu ya kielimu, wanafunzi maalum wa fani ya masuala ya kukabiliana na maafa ili sasa tuwe na msingi wa uimara wa wananchi wetu wenye uwezo wa taaluma ya kukabiliana na maafa. Vyenginevyo itakuwa ni kujidanganya na sheria hii itakuwa haina msingi mkubwa na haitowasaidia wananchi wetu.

Mwisho kabisa niiombe serikali sheria kama hii ambayo ni muhimu sana nadhani ingebidi sio tu kwa semina kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, lakini ingebidi kujifunza kwa nchi ambazo zina uwezo mkubwa wa kukabiliana na maafa. Pengine serikali wao wametembea nchi mbali mbali ili kuona nchi gani zenye uwezo mkubwa wa kujikinga na majanga, lakini kwa masikitiko makubwa sijasikia Mwakilishi gani amekwenda kujifunza fani hizi na semina hizi nchi mbali mbali.

Kwa hivyo, serikali iombe basi isifanye uchoyo pale wanapoona kuna mambo ya kitaifa, wanapata semina za kitaifa ambazo zinahusu mambo kama haya ya majanga nadhani ingewachukua wawakilishi mmoja hadi wawili, watatu ili kupata uzoefu wa nchi mbali mbali, ili wanapokuja hapa wajenge uwezo na uzoefu mkubwa wa kujenga hoja kwenye masuala haya.

Mhe. Naibu Spika, kama mchango wangu huu Mhe. Waziri atauona una maana basi nitaweza kuzingatia hoja ya kuunga mkono mswada huo. Nakushukuru sana.

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante Mheshimiwa nakushukuru, Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea, majadiliano yanaendelea. Mhe. Bikame Yussuf Hamad. *(Makofi)*

**Mhe. Bikame Yussuf Hamad Khamis:** Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa kuweza kunipa na mimi fursa hii nikaweza kutoa mchango wangu mdogo sana katika mswada huu wa kuanzishwa Sheria ya Kupunguza na Kukabiliana na Maafa Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutujaalia uzima na afya ili tukaweza kukutana hapa tukaendelea na shughuli zetu katika mkutano huu.

Mhe. Naibu Spika, nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri na serikali kwa ujumla kwa kuweza kufikiria kuleta Mswada huu wa Kupunguza na Kukabiliana na Maafa Zanzibar. Hili limekuja kwa sababu fulani ya matokeo mbali mbalia ambayo yamejitokeza na ndio ukaweza kuletwa mswada huu, kitu ambacho ni kuchelewa kidogo. Mana tumesubiri matoke yashatokea ndio sasa tunajipanga katika kupunguza au kukabiliana na haya maafa.

Mhe. Naibu Spika, mimi nadhani kwamba serikali kama inafanya kazi zake kikamilifu basi tusingefikia hapa. Kwa sababu maafa ni suala la maumbile ambalo hutokezea katika mitihani mbali mbali ya binadamu yawe ni ya moto, yawe ni ya kuzama, yawe ni ya maradhi, yawe ya chochote kile. Kwa hiyo, kwanza tumuombe Mwenyezi Mungu atuepushe na haya maafa ili yasitutokee majanga makubwa makubwa kama nchi za wenzetu, tumuombe sana Mwenyezi Mungu na tumuogope.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka niingie kwenye suala hili la tafsiri, kupunguza vihatarishi vya maafa. Maana yake ni dhana ya utekelezaji wa kupunguza mambo yanayosababisha maafa kwa kufanya uchambuzi na kudhibiti visababishi vya maafa ikiwa ni pamoja na kupunguza uwezekano wa kutokea majanga, uwezekano wa kuathiriwa kwa watu na mali, usimamizi mzuri wa ardhi, mazingira, kuimarisha maandalizi kwa ajili ya kukabiliana na matukio na majanga ya maafa.

Lakini ya 3 maafa yanayosababishwa na binadamu, kaeleza hapa Mhe. Waziri kuwa ni migogoro ya kijamii, vurugu, uchafuzi wa mazingira, vita na mafuriko, maradhi na miripuko.

Mhe. Naibu Spika, haya ni masuala ambayo kama serikali ilijipanga basi kulikuwa leo hakuna haja ya kupanga timu hii ambayo kuwa timu hii inayopangwa hapa ni ya kuendesha vikao, tathmini na mambo mengine. Lakini kama serikali ilijipanga hii iliyo na wizara hazipungui 16 na yote haya yanatokana ndani ya Taasisi zetu za Serikali.

Mhe. Naibu Spika, kwa mfano, tuna vikosi vingi Zanzibar ambavyo tunaambwia vikosi hivi ni kulinda raia na mali zao, lakini je, ndivyo vinavyofanyika? Sivyo vinavyofanyika kwa sababu ukienda kwenye vikosi hivyo vinavyolinda raia na mali zao ukifika kwenye hizo taasisi zao watakapokuelezea changamoto zao basi huzanii kama vikosi vile ni vya serikali.

Kwa mfano, kama vikosi vilivyotajwa humu KMKM na Kikosi cha Zimamoto ambao ndio waokozi wakubwa wa maafa haya yanayotutokea huku nyuma. Lakini leo ukienda kwenye Kikosi cha Zimamoto ile Pemba nzima pengine kuna vituo viwili, kweli watakabiliana na majanga hayo yatakayotokea kama ni ya moto? Sasa ni kukosa kujipanga ili tukaona yatakapotokea majanga haya tutakabiliana nayo vipi, lakini leo hawawezeshwi kwa sababu wapo. Ukienda vikosi hivi wao wamegeuka kama nyoka wanasubiri zile nyumba wanazohama watu wende wakapenyezwe wao, wanaonesha huruma, wanaonesha imani kiasi fulani. Sasa kama hawa hawakuwezeshwa hao watakaokabaliana na majanga ni nani?

Sasa mimi naona huu muundo wa Kamisheni ni kuandaliwa kwa kuratibu vikao tu hakuna jengine. Jengine kama tunalitaka tukabiliane na maafa kwanza ni kutafuta vile vikosi ambavyo vipo kwamba vya serikali vikaweza kuimarishwa, ndio watakabiliana na hayo majanga. Lakini kama hivi vitakuwa haviwezi kuimarishwa leo ukienda KMKM wana malalamiko yao tele, lakini serikali haiwatizami sasa nani atakayekabiliana na majanga?

Suala jengine kuna suala hapa katika haya ya tafsiri migogoro ya kijamii, vurugu, uchafuzi wa mazingira yote yanatoka kwenye taasisi zetu hizi za serikali. Kwa sababu ipo wizara inayoshughulikia suala la mazingira lakini ukiendelea miti inakatwa na bahari inakuja juu, sasa hii wizara ina kazi gani.

Lakini tukienda kwenye migogoro ya kijamii leo Waziri wa Katiba na Sheria kuna watoto wamezaliwa tangu mwaka tisini na ngapi huko hawana vyeti vya kuzaliwa, tukienda wilayani tunaambiwa hakuna magamba, hakuna nini, vurugu hazitatokea, vurugu zitatokea. Lakini sasa ajipange yeye ili watu wasisumbuke tuondoe hii migogoro ya kijamii. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, ukienda kwenye suala la vitambulisho watu hawapatiwi vitambulisho vurugu halitatokea? Sasa serikali ijipange itafute chanzo cha yale wanayoyasema humu, lakini tumeletewa mswada, kutaundwa Kamisheni sijui nani hao, hawa ni watu watakaoratibu kwenda kwenye vikao tu, wakitoka kikao hiki wende kikao hiki, wakitoka hiki wende hiki, inayotumika hapo ni pesa. Lakini vikosi ambavyo kuwa ni kulinda raia na mali zao havishughulikiwi mambo mengine tunayo wenyewe tusitafute mchawi. Serikali tuiendeshe vizuri mambo mengine tuyapunguze, Waziri wa Katiba na Sheria kama hataki kutokee vurugu atuletee magamba wilayani kwetu tusifanye vurugu, lakini wataoonekana ni raia tu ambao wanafanya hivyo wakubwa hawaonekani, wanafanya nini wao?

Sasa naiomba serikali mambo mengine wasiyatie katika mambo ya maafa hayaingiliani kabisa na masuala ya maafa. Kwa sababu kama hamtotupa vitambulisho watu watafanya fujo kama vyeti vya kuzaliwa watu wanakaa miaka mitatu tutafanya fujo. Sasa haya mambo mengine ni mambo ya kawaida.

Lakini suala jengine Mhe. Naibu Spika, katika huu muundo wa Kamisheni. Muundo wa Kamisheni sijaona hapa wametajwa watu watakaounda hiyo kuna mawaziri wote wa serikali hao Mwanasheria Mkuu, Katibu Mkuu Kiongozi na watu wengine. Lakini sijaona watu wa utabiri wa hali ya hewa humu. Sasa tutajuaje hayo matokeo yatakayotokea mengine. Kwa hiyo Mhe. Waziri uje utueleze au kama kuna uwezekano basi na wao ni watu wa kuingizwa ili wakaingia humu kukabiliana na hayo maafa mengine, basi watutabirie angalau utabiri wao wa hali ya hewa. Lakini naona mengine ni mambo ya kujitakia sisi wenyewe. Kwa hiyo, lazima tuweze kujirekebisha.

Lakini kuna kazi za Kamisheni kazi moja kasema ni kuanzisha na kuzielendeleza ghala za vifaa vya makabiliano ya maafa katika kazi za Taifa na Wilaya. Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri isijekuwa kuwa kuziendeleza ghala hizi ni sawa na sawa na ile Wizara ya Kilimo walivyosema kuwa wana ule mradi wa uhakika ule wa chakula na lishe mpaka leo hii tunasubiri maghala hayo yakarabatiwe mpaka leo hii hayajaonekana yalipo. Baada ya hayo macheche Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, mimi nilikuwa sitaki niseme lolote kwa sababu huu Mswada nilikuwa nauunga mkono mia kwa mia kwa sababu umepita katika kamati yangu, kwa hivyo mambo yote nilikwisha kuyasema huko.

Lakini nitakachofanya sasa hivi kwa sababu inaonekana *audience* hii wengi sijui wamefilisika au wameridhika na mswada huu mimi naona nitie nyalio tu kidogo.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema naunga mkono mia kwa mia mswada huu lakini nitatia nyalio kidogo tu kwamba hapa kwenye madhumuni ya mswada. Madhumuni ya mswada huu kwa mujibu wa tulivyoelezwa huku ndani ya mswada ni kwamba sheria hii itajulikana kama ni Sheria ya Kukabiliana na Maafa Zanzibar ya mwaka 2015. Mimi nadhani Mhe. Naibu Spika, ingenoga zaidi sheria hii kama tungesema kama ni sheria ya kukabiliana pamoja na kujikinga na maafa kwa sababu *Prevention is better than cure.* Kuna maafa ambayo hatuwezi kuyakinga lakini kuna maafa baadhi ya maafa Mhe. Naibu Spika, yamo katika mikono ya binaadamu uwepo au kutokuwepo kwake Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, tukiangalia maafa tunaweza tukaangalia yamo katika maeneo mawili makubwa. Kwanza ni katika maeneo haya ya ardhi, maafa tunayoyategemea hapa zaidi ni moto, harakati za kijamii kwa mfano kama vile kasa alivyoleta maafa kasa katika kijiji cha Micheweni na kule kwetu Vitongoji pamoja na maafa yaliosababishwa na viashiria mbali mbali vikiwemo serikali vinasababisha Taasisi za Kiserikali nyengine zinaweza kusababisha maafa. Kwa mfano, yale maafa tunayoyapata siku za uchaguzi mara nyingi yanayosababishwa na *ZEC* haya viashiria vyake vinaanza kujitokeza hivi sasa.

Sasa Mhe. Naibu Spika, baada ya kuangalia sana kwamba haya maafa katika ardhi tunataka kukabilaian nayo tu lakini kujikinga nasema hii sheria haijajikita katika kujikinga. Kwa mfano hivi juzi tulipata maafa Micheweni ya moto. Lakini ile gari ya zima moto iko Chake Chake tena moja na halafu haina mafuta, yaani kuitoa gari tu Chake Chake mpaka ukaifikisha Micheweni ni karibu saa moja kamili inandoka pale ikiwa na mafuta je haina mafuta utafute mafuta ukisha uitie gari mpaka ukifika Micheweni basi maafa yameshaathiri sana.

Sasa ndiyo nikasema kwamba sheri hii tunayotaka kuipitisha sasa naomba sana na Waheshimwa Wajumbe tuipitishe hii ziadi imejikita katika kukabiliana na maafa lakini sio katika kujikinga. Kwa hivyo, naomba serikali kabla hatujapitisha hii sheria lazima iwe na adha ya kuwezesha utekelezaji wa hii sheria kwa maana ya kupanua bajeti ya kuweza kukabiliana na kujikinga na hayo maafa.

Mhe. Naibu Spika, vile vile isitoshe kwamba wakati ninazungumza sasa hivi kuna *Marine Disasters* ambazo nyingi tunakumbana nazo hapa Zanzibar yaani maafa ya baharini. Hapa nashukuru katika muundo wa Kamisheni katika kifungu cha nne pale wako hawa Makamanda wa Vikosi vyetu vya KMKM, JKU, KZU sijui alimuradi vikosi vyote vya Zanzibar vimo.

Kwanza nichukuwe nafasi hii kuwapongeza hawaz Vikosi. Kwa kweli wamejitahidi sana katika suala zima la kukubiliana na maafa pale yanapotukabili. Lakini Mhe. Naibu Spika, pamoja na kuwaweka hawa tumewaweka hawa ndio Mwenyezi Mungu tunusuru ikitoke watatoa amri vikosi vifanye kazi, lakini sasa uwezo hawawezeshwi vikosi hivi.

Sasa mimi nadhani kabla hatujenda katika bajeti ya huku lakini vile vile hivi vikosi tuvione kwa mfano Mhe. Naibu Spikia, ukienda sasa hivi pale KMKM wale ndio wanaotusaidia sana kuzamia mameli kufunga meli ikiwa imezama tumepiga kelele sana kwamba *Diver* wetu pale wana tatizo zile *Diving suit* ni kidogo walizonazo pamoja na kuna mashime moja imeshaharibika pale KMKM. Hata ikitokea *Marine Disaster* itakuwa si rahisi wale kuwa na uwezo mkubwa kwa sababu *Diver* akienda chini akipata tatizo kuna mashine wanamtia pale limeharibika lile mashine mimi jina lake nimeshalisahau Mhe. Naibu Spika. Lakini kuna mashine akipata tatizo akitoka chini ya bahari aingie yule *Diver* atiwe kwenye lile mashine ndiyo atapata puumzi na kuweza kufanya shughuli zake za uokozi lakini hilo mashine halipo.

Sasa wakati tunaunda sheria hii tunamuweka Kamanda wa KMKM hapa lakini uwezo wa *Diver* wake ni mdogo kwa sababu hawana vifaa vya kutosha. Sasa mimi nadhani wakati sisi tunataka kupitisha sheria hii kwa upande mmoja, lakini kwa upande mwengine nashukuru Mtendaji Mkuu wa Serikali hapa Makamu wa Pili wa Rais yupo kuna umuhimu sana wa kuviwezesha hivi vikosi vyetu kuweza kukabiliana na maafa kwa kuviwesha kwa vifaa, hivi hao JKU hawasemwi unamkutaje JKU anakwenda kazini hata ile buti ana *Pair* moja hiyo hiyo ikichanika ndiyo tatizo. Hebu tuone ma- *Disaster* yote yanayotokea vikosi vinakuwa mbele. Kwa hivyo, tunaomba sana ili tuweze kuweza kufanikisha vizuri baada ya kutunga hii sheria ni vyema sana tukaweza hivi vikosi kuvisaidia katika vifaa.

Mhe. Naibu Spika wanasema kwamba tone moja la maji ikiwa halikuangaliwa vyema linaweza likatela gharika katika nchi. Usemi huu unakwenda sambamba na ule usemi unaosema kama "Cheche moja ya moto kama haikudhibitiwa inaweza kuunguza mji mzima".

Mhe. Naibu Spika, mimi nadhani kuna majanga mengine tunajitakiwa sisi hapa, kuna majanga ambayo tunaweza kuyatatua hapo awali nilisema yako katika sehemu za serikali pamoja na kwa wananchi wenyewe. Wakati tuko katika kipindi hichi cha kuelekea uchaguzi Mkuu Mhe. Naibu Spika, inaonekana kuna viashiria vya maafa huko mbele.

Hivi inabidi tuvizibiti kabla hayajatufika. Kuna kipindi hapa ilitokea maafa watu wengi walikufa na wengine wakaathirika sana kwa sababu hatukuweza kudhibiti viashiria vya maafa, wakati kama bado miezi nane, tisa hivi kuingia katika Uchaguzi Mkuu tayari kuna viashiria kwamba yale maafa ambayo hutokezea kipindi cha uchaguzi yanataka kujitokeza tena.

Sasa naomba sana Mhe. Naibu Spika, kama tutapitisha sheria hii tuweze kudhibiti vile viashiria vya maafa. Kwa mfano hivi wakati sasa hivi naongea juzi wananchi wasiopungua 50 wa jimbo la Chonga katika Shehia ya Matale wakiwa na *Certified Copy* za *Birth Certificate* zao wamekwenda pale kutafuta nadhani *ID* na Sheha akawaahidi kwamba nyinyi njooni Ofisini kwa Mkuu wa Wilaya mkufika nitawatilia saini muende mkachukuwe vitambulisho vyenu pale, la kusikitisha Sheha yule alikimbia wale vijana wakahangaika sana na wakababaika mno.

Sasa mimi nadhani vijana kabla hawajaja juu katika kudai haki zao ambayo ni viashiria vya maafa basi Sheha yuko mikononi mwa serikali wakati anafanya vile sisi tukaripoti serikalini hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa Mhe. Naibu Spika, sasa hii inaonesha wazi kwamba kabla mambo hayajaanza maafa hayo yanataka kusababishwa na Ofisi ya Mkuu wa Vitambulisho, Maafa hayo yanataka kusababishwa na Ofisi ya Bwana Abubakari Khamis Bakar pale kwa sababu watu hawapewi vyeti vya kazaliwa.

Sasa nadhani mimi haya maafa ambayo tunaweza kuyadhibiti kwa kumuonyoeshea mkono tu Sheha basi anyoshewe ili atowe idhini kwa watu waliokuwa na vile vyeti, waliokuwa hawana asiwape. Mimi nakuhakikishia Mhe. Naibu Spika, kwamba tunapitisha sheria hii lakini *ZEC* yaani Tume ya Uchaguzi Zanzibar Ofisi ya Idara ya Vitambulisho inatutatyarishiwa maafa mazito.

Kwa hivyo, mimi nadhani ili kuepuka maafa haya sheria tunaipitisha hii Tume ya Uchaguzi iko katika mikono ya serikali, hawa Ofisi ya Idara ya Vitambulisho iko katika mikono ya serikali waangalie uwezekano wa kujikinga na maafa kabla hayajatufika.

Baada ya nyalio hizo chache Mhe. Naibu Spika, kwa sababu mswada huu umepita katika kamati yangu nimeamua moja kwa moja Mhe. Naibu Spikia, kuunga mkono mswada huu mia kwa mia ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante Mheshimiwa nakushukuru. Waheshimiwa Wajumbe naona michango imekamilika. Lakini Mhe. Waziri kapata hoja nzito kwa hivyo kaomba majumuisho tuyafanye kesho baada ya maswali. Sasa kwa muda uliobakia namuonba Mhe. Mwanasheria Mkuu atoe hoja ili tuweze kuakhirisha Baraza letu.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa muda wa kumaliza Kikoa cha Baraza haukumalizika na kwa kuwa shughuli zilizopangwa leo zimekwisha naomba kwa kutumia kifungu cha 23 tuakhirishe Kikao cha Baraza mpaka kesho saa 3:00 asubuhi naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa hoja imetolewa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja wanyooshe mkono, waliokataa, waliokubali wameshinda. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wajumbe kwanza niwashukuru kwa ushirikiano wenu wa tangu asubuhi hadi jioni hii na hivi sasa naakhirisha kikao hichi hadi kesho siku ya Ijumaa tarehe 23/01/2015 saa 3:00 asubuhi barabara.

*(Saa 12. 55 jioni Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 26/01/2015 saa 3:00 asubuhi)*